

10 APRILI, 2013

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Pili - Tarehe 10 Aprili, 2013

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Na.10

Matatizo yanayozikumba Shule za Sekondari za Kata

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE aliuliza:-

Wananchi wa Tarime wamejithadi kujenga shule za Sekondari za Kata, lakini shule hizo zinakabiliwa na matatizo makubwa ya upungufu wa vyumba vyaya madarasa, nyumba za walimu, ukosefu wa maabara, maktaba, vitabu, upungufu wa walimu, umeme, maji na miundombinu ya barabara.

- (a) Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya matatizo haya?
- (b) Je, ni lini Serikali itaunga mkono juhudii za wananchi za kuezeka maboma ambayo wananchi wameshindwa kuyatimiza?

(c) Je, ujenzi wa shule ya kisasa ya bweni ya wasichana ya Borega utaanza na kukamilika lini?

NAIBU WAZIRI,OFISI YA WAZIRI MKUU,TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ina mikakati mahsusiy ya kukabiliana na changamoto mbalimbali katika shule za sekondari kuititia Awamu ya pili ya Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES II). Kuititia mpango huu Serikali imeanza ujenzi na ukamillishaji wa Sekondari 264 ili kuzifanya kuwa na miundombinu yote muhimu ikiwemo maabara, maktaba, vyoo, umeme na maji.

Jumla ya shilingi bilioni 56.3 zitatumika kwa mwaka 2012/2013 na Halmashauri ya Wilaya ya Tarime inakamilisha taratibu za zabuni ya shilingi milioni 484 kutekeleza mradi huu katika shule za Sekondari Nyawanga na Kurumwa. Ununuzi wa vitabu unafanyika kuititia 50% ya fedha za uendeshaji (*Capitation Grants*)ambazo kwa mwaka 2012/2013 shule za sekondari zilitengewa shilingi millioni 214 hadi Machi,2013.

Aidha, kwa kushirikiana na sekta binafsi, Serikali imeongeza udahili wa walimu katika vyuo na walimu wanaohitimu wataendelea kuajiriwa na kuwapanga katika Halmashauri ili kuwa na walimu wa kutosha katika shule zote ifikapo 2014. Mwezi Februari, 2013 Serikali imewapanga walimu 12,973 katika shule za sekondari nchini na Wilaya ya Tarime ilipangiwa walimu wa sekondari 184.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inathamini na kuunga mkono juhudzi za wananchi katika miradi mbalimbali ikiwamo kukamilisha maboma kwa kutenga fedha kuititia mipango, Bajeti na vipaumbele vya Halmashuri.

10 APRILI, 2013

Kwa mwaka 2012/2013, Serikali ilitenga shilingi bilioni 74 kuititia mipango na Bajeti za Halmashauri kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa miundombinu ya shule za sekondari ikiwemo nyumba, maabara, maktaba na vyoo.

Aidha, Serikali imeshatumia jumla ya shilingi bilioni 9.3 kukarabati shule za sekondari Kongwe nchini ikiwemo shule ya sekondari Tarime iliyopatiwa shilingi milioni 100.

Pia shilingi bilioni 3.6 zimetolewa katika Halmashauri kwa ajili ya ununuzi wa maabara hamishika. Halmashauri ya Wilaya ya Tarime ilipatiwa shilingi milioni 24.

(c) Mheshimiwa Spika, ujenzi wa shule ya wasichana Borega umetokana na juhudzi za Halmashauri kuwa na shule za wasichana ili kutoa fursa zaidi kwa watoto wa kike katika kupata elimu. Ujenzi unatakiwa kuanza rasmi mwezi Juni, 2013 na kukamilika ifikapomwezi Novemba, 2014. Halmashauri kuititia mapato ya ndani imechangia shilingi milioni 28, eneo la ujenzi limeshapimwa na kwa sasa taratibu za kutangaza zabuni zinaendelea. (*Makofii*)

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimi Spika, kwanza nimpongeze mheshimiwa Waziri kwa majibu yake ambayo yanatia matumaini kidogo pamoja na hilo nina maswali mawili ya nyongeza. Lakini kabla kuuliza maswali shule ile inaitwa Nyawaga na siyo Nyawaga.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Naibu Waziri amesema kuwa kufikia mwaka 2014, tatizo la walimu katika nchi yetu litakuwa ni historia ninaomba kauli ya Serikali mtuambie mmejpanga vipi kuhakikisha kuwa mmeandaa walimu wa kutosha wa masomo ya Sayansi katika shule za Sekondari kwa ajili ya somo la Hisabati, Fizikia, Kemia na Biolojia? Masomo haya ni tatizo kwa sababu hayana walimu nchi nzima.

10 APRIL, 2013

Swali la pili, ninaipongeza sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis kwa kupeleka walimu 184 katika Wilaya ya Tarime lakini Waziri unafahamu kuwa kuna baadhi ya walimu wakipangwa katika Halmashauri ambazo zina shule za Kata vijiji ambako hakuna umeme wala maji, hawaendi. Je, Serikali imejipanga viyi kuhakikisha kuwa hawa walimu wanaenda katika shule hizo? (Makof)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU,TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kujibu swali, kila mmoja anapofanya jambo jema ni vyema kumsifu, wakati Serikali inafanya jitihada kusambaza vitabu nchini Mheshimiwa Nyambari Nyangwine ni Mdau mkubwa katika eneo hilli na taarifa nillizo nazo kutoka Tarime ni kwamba ameweza kuichangia Wilaya yake ya Tarime vitabu vya jumla ya milioni 12 ambavyo viro kule Ruangwa na nimeona pia kule Ifakara kwa Mheshimiwa Mteketa endelea na jitihada zako. (Makof)

Mheshimiwa Spika, ninataka ku- *declare interest* kuwa Wilaya ya Ruangwa nayo imefaidika sana kwa michango yake kwa jumla ya shillingi milioni 12 ambavyo viro kule Ruangwa na nimeona pia kule Ifakara kwa Mheshimiwa Mteketa endelea na jitihada zako.

Serikali imejipanga kukabiliana na walimu wa masomo ya Sayansi na njia ya kwanza ambayo tumeitumia ni ile ya kuweza kutoa mikopo kwa vijana ambao wanamaliza Vyuo Vikuu kwenda kuingia katika Elimu ya Vyuo Vikuu kwa kuwapa mikopo ili tuweze kupata idadi kubwa ya vijana ambao wanasoma masomo ya Sayansi ili waende kufundisha katika shule zetu za Sekondari. Hiyo ni njia mojawapo ambayo tunaitumia.

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika eneo hili tunajitahidi kuhamasisha kutoka katika ngazi ya shule zetu za Sekondari kwa kupeleka maabara hamishika ili vijana walioko mashulen i waweze kusoma masomo ya Sayansi kwa vitendo na wafanye mitihani kwa vitendo, ili wafaulu vizuri na waendelee na masomo ya juu mpaka Vyuo Vikuu, ili waweze kurudi tena kufundisha wenzao kwa masomo ya Sayansi. Jitihada hizi zitaendelea na tunaendelea kuandaa utaratibu mwingine iko timu inafanya *study* ya namna ya kuboresha sekta hii na baadaye tutakuja kuwajulisha Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni baadhi ya walimu ambao hawaendi vijijini; kwamba tunatumia utaratibu gani ili kuhakikisha changamoto hii inakamilika na walimu waweze kwenda maeneo ya vijijini. Eneo hili ninataka kuwaambia Watanzania kuwa ellmu yetu ya msingi na Sekondari shule zake ziko katika mazingira hayo ya vijijini na shule za Kata yako kwenye Kata na katika Kata zote ndiko ambako sisi tumetoka.

Kwa hiyo, Serikali pamoja na jitihada za kuboresha miundombinu kama vile nyumba za kuishi na kuongeza vyumba vy ya madarasa ambavyo watafanyia kazi ili kuboresha mazingira hayo ni bora wakaona kuwa tunakowapeleka ndiko ambako wanapaswa kufanya kazi kwenye maeneo hao.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo tumeanza mpango wetu huu wa fedha ambazo nimezitamka hapa za kuboresha miundombinu iliyokamilika ni pamoja na umeme na maji. Kwa hiyo jitihada hizi zitawafanya walimu wetu kwenda kuishi maeneo yale na kuendelea kufanya kazi.

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Spika, ninakushuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja. Kwanza niipongeze Serikali kwa taarifa nzuri na juhudzi zinazochukuliwa katika kuimarisha elimu.

10 APRIL, 2013

Lakini liko tatizo la wazi kama tuliviyoliona mwaka huu kuwa matokeo ya mitihani yamekuwa mabaya sana. Serikali ina mpango gani wa makusudi kwa sababu dalili zinaonyesha kuwa elimu inaendelea kushuka Serikali ina mpango gani wa makusudi katika kuimarisha pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri?

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa maabara, ujenzi wa madarasa na kuna shule katika Jimbo langu la Lushoto ambalo kwa kweli tunahitaji sana msaada sana wa Serikali. Je, Serikali inatoa kauli gani ya kutoa *time frame* kuondoa tatizo hili la kushuka kwa elimu?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, suala la ufaulu hafifu wa mwaka huu nisingependa kutumia nafasi kutoa majibu kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu alishaunda Tume ambayo inafanya mapitio kwa ujumla wake, ili kuweza kubaini udhaifu wote ambao umejitokeza uwe ni wa mwaka huu, lakini pia utafiti utakaofanywa na timu ile unaweza pia kubaini changamoto ambazo tunatakiwa kuzikabili katika eneo hili.

Kwa hiyo, tuache Tume iendelee kufanya kazi yake tupate mapendekezo yao na yatatangazwa na Serikali. Pia itaweza kufanya jitihada za kuhakikisha tunakamilisha yale yote ambayo yamependekezwa na Tume ile ili tupate matokeo mazuri hapo baadaye.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, na mimi ninashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na matatizo mengi tuliyo nayo katika elimu yetu, Idara ya Ukaguzi Elimu mashulen ni kama imesahauliwa Wakaguzi wako wamekaa tu hawana wanachokifanya. Je, Serikali haioni kuwa kuiacha Idara ya Ukaguzi Mashulen bila nyenzo, bila msaada wowote ni moja kati ya mambo yanayosababisha kiwango cha elimu nchini kushuka?

10 APRILI, 2013

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, suala la ukaguzi ni mionganoni mwa yale ambayo yanaendelea kutafutwa na ile Tume yetu, na utaratibu wa namna gani kuboresha sekta hiyo na kuifanya ifanye kazi zake vizuri ni mionganoni mwa yale ambayo yatabolewa mapendekezo na ile Tume yetu. Kwa hiyo, hili ninaomba tuliache kwa kuwa liko katika maeneo ambayo yamepelekea pia kushuka kwa kiwango cha elimu na hivyo mapendekezo ya Tume ndiyo ambayo yatafanyiwa kazi.

SPIKA: Tumetumia dakika 13 kwa swali moja kwa hiyo, ninamwita Msemaji mwingine Mheshimiwa Suleiman Nchambi na kwa niaba yake Mheshimiwa Mwigulu Nchemba.

Na. 11

Fedha za Kumalizia Hospitali ya Wilaya Kishapu

MHE. MWIGULU L. N. MADELU (K.n.y. MHE. SULEIMAN M. N. SSULEIMAN) aliuliza:-

Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu haina uwezo wa kumalizia mradi wa jengo la Hospitali ya Wilaya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza ujenzi huo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Suleimani Nchambi, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali iliridhia ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kishapu ili iweze kutoa huduma za rufaa kwa wakazi wa Wilaya hii. Serikali imefanya jitihada nyingi kuhakikisha kuwa hospitali hiyo inakamilika na kutoa huduma kwa wakazi wa Wilaya ya Kishapu.

10 APRILI, 2013

Jumla ya shilingi milioni 544.9 zimekwisha kuidhinishwa na Serikali katika Bajeti ya 2008/2009, 2010/2011, 2011/2012 na 2012/2013 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali hiyo ambapo shilingi milioni 444.9 ziliidhinishwa kutoka mfuko wa *LGCDG* na shilingi milioni 100 kutoka mapato ya ndani ya Halmashauri.

Fedha hizi zilitumika kujenga jengo la wagonjwa wa nje (*OPD*) na wodi mbili. Wodi moja ya wanawake na nyingine ya wanaume, ambapo shilingi milioni 362.9 zilitumika kukamilisha jengo la *OPD* na shilingi milioni 182 zilitumika kukamilisha ujenzi wa wodi hizo mbili.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2013/2014 Halmashauri imewasilisha Hazina maombi maalum ya shilingi bilioni 2.7 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa hospitali hiyo ambapo Hazina imetoa idhini ya shilingi milioni 400.

Aidha, Halmashauri imetenga katika Bajeti yake shilingi milioni 318.9 toka fungu la *LGCDG* na milioni 200 kutoka katika makusanyo ya ndani, ili endapo Bunge lako Tukufu litaridhia, fedha hizo ziweze kutumika katika ujenzi wa Hospitali hiyo basi utendaji kazi wake utaendelea.

MHE. MWIGULU L. N. MADELU: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri Serikali imeanzisha miradi maalum katika Hospitali nyingi za Wilaya ikiwemo ile ya Iramba kwa kujenga jingo kwa ajili ya akina mama wajawazito kujifungulia hospitalini badala ya vijiji na katika zoezi hilo akina mama wamehamasika sana kiasi kwamba wanakosa mahali pa kupata huduma hiyo na pia Wilaya hiyo inachukua akina mama wengi mpaka Wilaya mpya ya Mkalama ambayo haina Hospitali.

Je, ni lini Serikali itatoa kipaumbele kwenye majengo ambayo ilihamasisha kwa kauli yao ili kuweza kumalizia miradi ya namna hiyo na wananchi kuweza kupata huduma katika Wilaya mbalimbali?

10 APRILI, 2013

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Serikali na hasa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) inaendelea kuhamasisha Halmashauri zetu kuona umuhimu wa kuboresha miundombinu katika Halmashauri zetu, na tunapotoa uhamasishaji maana yake ni kuwa Halmashauri husika kupitia Mabaraza ya Madiwani yaweke utaratibu wake na Bajeti katika kuhakikisha kuwa yanaboresha eneo ambalo lina mapungufu katika Hospitali zao.

Mheshimiwa Spika, utaratibu tunaotumia katika Bajeti zetu ambazo unajua Halmashauri nydingi tumezihamasisha na kuridhika na jambo hili tukishapata taarifa ya mchango wenu wa mapato ya ndani na ambavyo mmeamua kukamilisha jengo lile yale mapungufu mkituandikia tunaweza kuona namna ya kutoa nyongeza ya eneo hilo ili kukamilisha miundombinu hiyo. (*Makofii*)

MHE.ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa sina tofauti na huyu mwuliza swali la msingi ni kwamba Wilaya yetu ya Misenyi ni Wilaya mpya na inalo tatizo hilo hilo na kwa upya huo hatuna uwezo wa kuweza kumalizia jengo letu la Hospitali.

Je, Serikali iko tayari kutusaidia?

SPIKA: Jibu litakuwa ni lilelile siyo? Swali ni hilo hilo na jibu ni hilo hilo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mshama ambalo linaonekana ni lilelile na majibu ni yale yale, lakini sasa tuweze kuboresha tu kuwa Wilaya zetu zote mpya zina mpango na ndiyo zinazopewa kipaumbele.

Kwa sasa ninadhani itakuja kujititokeza pia kwenye Bajeti hii ambayo itakuja kusomwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwenye maombi ya mwaka 2013/2014.

10 APRIL, 2013

MHE. RAHEL M. ROBERT: Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kishapu kuna Mgodi wa Almasi wa Mwadui na inatia aibu sana kuona Hospitali ya Wilaya mpaka sasa hivi hajakamilika.

Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu wa kukaa na wale wenye Mgodi ili waweze kusaidia kujenga Hospitali hiyo?

SPIKA: Haya mjihadhari kuwa na maswali mapya kuliko ya zamani.

AIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa tumetambua kuwa Hospitali yake na Hospitali zingine zina matatizo ambayo pia yanahitaji kuboreshwa na kuchangiwa na wadau ikiwemo wadau hao walioko pale pale Kishapu. Kwa hilo tunachofanya sasa ni kufanya mazungumzo nao lakini ninaisihi Halmashauri kuanza mazungumzo hayo kwa ngazi yao na pale ambapo wanaona kuna haja ya kuongeza nguvu kutoka ngazi ya Wizara basi tutaungana nao ili kuweza kutoa msukumo wa Wadau hao kuchangia sekta hizo mbalimbali ikiwamo na sekta ya Afya.

Na. 12

Muuguzi Mkuu wa Serikali Kutengewa Bajeti

MHE. ROSWEETER F. KASIKILA aliuliza:-

Muuguzi Mkuu wa Serikali anatakiwa kuwafikia Wauguzi wote nchini ikiwa ni pamoja na maeneo ya Kirando, Kasanga, Matai, Laela, Mtowisa na Sehemu nydingine Mkoani:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kutomtengea Bajeti Muuguzi huyu ni sawa na kudhoofisha kazi yake?

(b) Je, Serikali inaahidi nini juu ya kutenga Bajeti ya Muuguzi huyu kwa mwaka 2013/2014?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rosweeter Faustine Kasakila, Mbunge wa Viti Maalum, swali lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, fedha za Serikali katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii hugawiwa kwa watendaji wake kupitia Idara mbalimbali. Kabla ya mwaka 2011/2012, Bajeti ya Muuguzi Mkuu wa Serikali ilikuwa inakasimiwa chini ya ofisi ya Mganga Mkuu wa Serikali. Aidha, baada ya mabadiliko ya kimuundo katika Wizara yaliyofanyika mwaka 2012, Bajeti ya ofisi ya Muuguzi wa Mkuu wa Serikali ilitengwa kupitia Idara ya Uhakiki Ubora wa Huduma za Afya na Ustawi wa Jamii. Kiasi cha shilingi 1,265,253,308/= zilitengwa 2012/2013 na katika mwaka ujao wa fedha 2013/2014 kiasi cha Tshs.1,201,495,000/= zimetengwa ili kutekeleza shughuli mbalimbali za Idara hiyo zikiwemo kazi za ofisi ya Muuguzi Mkuu wa Serikali.

(b) Mheshimiwa Spika, kulingana na muundo wa Wizara kwa sasa ofisi ya Muuguzi Mkuu wa Serikali iko chini ya Idara ya Uhakiki Ubora wa Huduma ya Afya. Kwa hiyo, Bajeti yake imepangwa katika idara hiyo. Aidha, yapo mapendekeweza kuifanya mabadiliko ya muundo wa Wizara ambayo yamependekeweza kuundwa kwa Idara mbili mpya za Uuguzi na Famasia. Taratibu za Muundo zikikamilika Bajeti ya ofisi ya Muuguzi Mkuu itatafutiwa kasma yake kwa kuzingatia taratibu na miongozo ya Serikali.

MHE. ROSWEETER F. KASIKILA: Mheshimiwa Spika nakushukuru sana kwa nafasi hii, naomba kuuliza maswali mawili tu ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, hili suala la uundai wa Idara ya Uuguzi ili kurahisisha kazi za kiuuguzi na kuleta mafanikio tumelizungumzia kwenye Bajeti ya mwaka jana na Serikali iliahidi kwamba iko mbioni kuunda idara hii, lakini sasa tumeshamaliza mwaka mzima idara haijaundwa.

10 APRIL, 2013

Je, ni taratibu gani hizo ngumu zinazofanya Idara isiundwe mapema na taratibu hizi zitakamilika lini maana tunaambiwa kwamba taratibu zinaendelea, zitakamilika lini tunaomba *timeframe* ili mwakani tuweze kuuliza tena swali hili? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:

Mheshimiwa Spika, kwanza tulitoa ahadi na nimeeleza katika jibu la msingi kwamba muundo unapitiwa na katika kupitiwa ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na yenyewe hivi sasa inashughulikia. Kwa hiyo, baada ya kukamilika zoezi hilo taarifa zitatolewa na kufanya mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, muundo siyo kitu ambacho unaweza ukakifanyia mabadiliko siku moja, muundo unaangalia maeneo ya kazi, maeneo ambayo yanakusudiwa kupatikana yaani malengo na namna ambavyo yataweza kuonesha ubora na ufanisi wa idara badala ya kuweza kuweka pingamizi ya utekelezaji wa idara.

MHE. DEUSDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Katika Wilaya ya Nkansi pamekuwepo na upungufu mkubwa sana wa Wauguzi na katika jitihada za kupunguza upungufu huo, wapo Watumishi ambao wamekuwa wakijendezea kutoka ngazi ya chini na kupata nafasi ya juu zaidi, lakini Serikali imekuwa haitambui nafasi zao baada ya kujijendezea katika suala zima la maslahi.

Je, Serikali haioni kwamba inafifisha jitihada hizo za watumishi hawa ambao ni wachache sana?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, miundo ya utumishi inashughulikiwa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Tulishahuisha muundo wa Utumishi wa Walimu na sasa hivi tupo kwenye jitihada za kuhuisha miundo mingine ili wafanyakazi wanaojendezea katika fani husika waweweze kubadilishwa kuingia katika daraja la juu badala ya kushushwa chini. Kwa hiyo, suala hilo linafanyiwa kazi kwa kada zote na siyo kada ya afya peke yake.

10 APRILI, 2013

MHE. MOZA A. SAIDY: Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nimwuulize Waziri swali la nyongeza.

Kwa kuwa, katika sekta ya afya Muuguzi Mkuu ndiye Muhimili Mkuu katika kuiongoza sekta nzima ya afya, ni lini Baijeti yako hii itawezeshwa na kumpa vitendea kazi Muuguzi Mkuu aweze kufika hata katika Wilaya ya Kondoa kwenye matatizo makubwa ya sekta ya afya ili aje awasikilize wafanyakazi wale na wananchi wote kwa ujumla ili kujua matatizo yanayowakabili ya kiafya katika Wilaya?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, kwanza Idara ya Uhakiki Ubora kama nilivyosema katika jibu la msingi imetengewa kiasi cha shilingi bilioni 1.2. Ndani yake kuna watalaan mbalimbali akiwemo Muuguzi Mkuu wa Serikali na wamepanganya kiasi cha shilingi milioni 300 kwa ajili ya kusafiri ndani ya nchi fedha ambazo Muuguzi Mkuu ana fursa nazo kuzitumia kama Watumishi wengine waliomo katika Idara.

SPIKA: Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge sasa twende Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Mheshimiwa Khatib Said Haji, atauliza swali hilo linalofuata.

Na. 13

Usumbuu Mkubwa wa Kupata Visa

MHE. RASHID ALI ABDALLAH (K.n.y. MHE. KHATIB SAID HAJI) aliuliza:-

Kumekuwa na usumbuu mkubwa kwa Watanzania wanapohitaji Visa katika baadhi ya Balozi kama vile Marekani na Uingereza:-

Je, Serikali inatoa kauli gani kwa Balozi hizo juu ya malalamiko hayo ya wananchi?

10 APRILI, 2013

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII (K.n.y. WAZIRI
WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Mheshimwia Spika, ni kweli kuwa kumekuwepo na malalamiko kutoka kwa wananchi juu ya usumbufu wanaoupara wakati wa kuomba *Visa* kwenye baadhi ya Balozi ikiwemo Marekani na Uingereza. Ni kweli pia masharti ya upatikanaji wa *Visa* yamekuwa magumu katika Balozi hizo. Wizara imejitahidi na bado inaendelea kuzisihi Balozi na nchi husika kulegeza masharti yao ya *Visa* kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, maombi ya *Visa* ya Uingereza na Marekani yamekuwa na usumbufu mkubwa kwa sababu nchi hizo mbili ni kati ya nchi ambazo zimeendelea kukabiliwa na matishio makubwa ya ugaidi duniani. Itakumbukwa kwamba tangu miaka ya 1990 baada ya vita ya Marekani na Iraq na baada ya shambulio la kigaidi la Septemba 11, mwaka 2001, Marekani wameimarisha mikakati yao ya kufuatilia na kudhibiti wageni wanaoingia nchini mwao. Hali hii siyo tu kwa raia wa Tanzania bali pia kwa raia wa nchi nyingine nyingi Duniani. Wizara imehakikishiwa kuwa, pale tu hali ya amani na usalama itakapotengemaa na matishio ya ugaidi kupungua nchi hizo zitalegeza masharti yake ya upatikanaji wa *Visa*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Uingereza Wizara imefanya mawasiliano na Serikali ya nchi hiyo ili *Visa* zitolewe katika Jiji la Dar es Salaam badala ya Nairobi kama ilivyo sasa. Serikali ya Uingereza imeahidi kulifanyia suala hili kazi.

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Spika nakushukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza Mtanzania anapoomba *visa* katika Ubalozi wa Uingereza analipia gharama kubwa, lakini anaponyimwa *visa* hiyo fedha hizo hazirejeshwi. Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya ubadhilifu huu?

Pili; katika jibu la msingi la Waziri anasema Serikali ya Uingereza imeahidi kulifanyia kazi. Katika Bajeti ya mwaka jana Wabunge baada ya kupiga kelele za nguvu sana Serikali ilisema kwamba itakuwa ni historia suala hili litapatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Je, tabia hii mbaya ya Serikali ya kupotosha Bunge ni lini itakoma?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Spika, taratibu za *refund* kama zinavyoitwa wakati mwombaji anaomba *visa* kwenye nchi husika zimekuwa kimsingi zimewekwa na nchi husika na ni kweli kwamba kama Waziri wa Mambo ya Nje aliviyolijibu Bunge katika kipindi kilichopita majadiliano haya yamekuwa yakiendelea kwanza kwa suala zima la gharama kubwa ambazo wananchi wengi wa kawaida wamekuwa hawazimudu na wakati mwingine zimekuwa kama adhabu.

Kwa hiyo, nakubaliana sana na Mbunge juu ya hili suala la gharama kubwa na uwezekano wa pale ambapo *visa* hajatolewa basi wahusika wafanye *refund*. Niseme tu kwa upande wa Serikali majadiliano haya bado yanaendelea. (*Makofii*)

Pili; kimsingi kama vile Tanzania tunavyofanya, nchi hizi kama nilivyosema kwenye swalii msingi zimeweka masharti na vigezo na kutokana na matatizo waliyopata Wamarekani mwaka 2001 na kutokana na changamoto zilizopo za ugaidi duniani na kutokana na watu wengi amba wanaenda kujilipua katika nchi za wenzao, na ugaidi huu unaendelea kuja hapa kwetu Tanzania, nchi zote Duniani ikiwemo Tanzania tumeongeza masharti ya wageni kupata *visa* kuja nchini kwetu ili kujihakikishia usalama wa wananchi

10 APRILI, 2013

wetu na mali zao. Kama nilivyosema Serikali ya Tanzania na Waziri wa Mambo ya Nje mwenyewe Mheshimiwa Benard Membe, amekuwa akifanya mazungumzo na Balozi husika, Ubalozi wa Uingereza wamemhakikisha Waziri kwamba wanafanya majadiliano mapya tena na nchi yao baada ya uamuvi wao kwamba *Visa* zote za nchi kadhaa zitolewe Nairobi waangalie uwezekano wa kuipatia hapa Dar es Salaam. Moja kwa sababu ya ukubwa wanchi ya Tanzania, na pili kwa sababu ya historia ya uhusiano wetu na Uingereza. Yamkini basi *visa* hizo ziweze kutolewa katika Jiji la Dar es Salaam.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa, Watanzania wengi wanakosa *visa* za Uingereza na Marekani kwa kushindwa kuelewa vigezo na mahitaji za *Visa* hizi, ni lini sasa Wizara itaanzisha kitengo cha *orientation* kwa sababu ya kuwaelimisha Watanzania wote wanaotaka kusafiri nje ya nchi? (*Makof*)

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA): Mheshimiwa Spika, utaratibu mpya ambao nchi nydingi duniani zinatumia ikiwemo Marekani na Uingereza wakati mwananchi anapoomba *visa* ni kuomba *visa* hizo kupitia mtandao wa *internet*. Nakubaliana sana na Mheshimiwa Leticia Nyerere kwamba kwanza kutokana na kutokupatikana mtandao huu wa *internet* nchi nzima mwananchi aliyepo pale Magu au pale Songea inamwia vigumu sana na utaratibu mzima unachukua muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, tunasisitiza na hapa ningeomba sana Wabunge waisaidie Serikali pamoja na Halmashauri zetu kuhakikisha kwamba tunaongeza wigo wa matumizi ya *internet* ili wananchi waweze kuwa na *access* tu ya mtandao huu wakati wanajiantaa kuomba *visa* katika nchi husika.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nashukuru sana kwa wazo lake.

10 APRILI, 2013

Na. 14

Ubovu wa Barabara ya Kibiti- Lindi

MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI (K.n.y. MHE. CLARA D. MWATUKA) aliuliza:-

Barabara ya Kibiti - Lindi eneo la Muhoro - Somanga bado linapitika kwa shida na hupoteza muda mwingi wa wasafiri na mabasi kukwama:-

Je, tatizo hili litakoma lini ili watu wasafiri kwa uhakika na kwa muda muafaka?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kibiti – Lindi ina urefu wa kilomita 317, ambapo takribani kilomita 260 kati ya hizo tayari zimejengwa kwa kiwango cha lami. Sehemu iliyobaki yenye urefu wa kilomita 60 ipo katika hatua mbalimbali za ujenzi kwa kiwango cha lami. Sehemu ambayo Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka ameitaja Muhoro – Somanga yenye urefu wa kilomita 29.5 ni sehemu ya mradi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Ndundu – Somanga yenye urefu wa kilomita 60 ambapo kwa sasa ujenzi wake unaendelea. Hadi sasa kilomita 30.5 zimekamilika kwa kiwango cha lami. Maendeleo ya jumla ya mradi wa ujenzi wa barabara ya Ndundu – Somanga kwa kiwango cha lami ni zaidi ya asilimia 83.

Mheshimiwa Spika, hivyo, napenda kulifahamisha Bunge kuwa sehemu ambayo haijawekwa lami yenye urefu wa kilomita 29.5 ipo katika hatua mbalimbali za ujenzi na kandarasi alikwishaagizwa na Wizara akamilishe sehemu hii mapema ili kuwaondolea matatizo ya usafiri wananchi wanaotumia barabara ya Kibiti – Lindi.

10 APRILI, 2013

MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI: Mheshimiwa Spika nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, sasa ni takribani miaka minane barabara hii haikamiliki kila siku tunaahidiwa, na tatizo kubwa ni Serikali kutolipa pesa kwa wakati kwa mkandarasi ili barabara hii iishe.

Je, Serikali haioni aibu kila siku kuwaahidi watu wa Kusini kuhusu barabara hii ambayo haikamiliki? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni kwamba *TANROAD* na Mkandarasi hawafanyi marekebisho kwa wakati kwa ile *diversion* wakati ambao barabara inakuwa imeharibika na kusababisha usumbufu mkubwa sana kwa watumiaji wa barabara, wakati mwagine huwa wanalala njiani. Je, Serikali inasemaje kuhusu hili?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli barabara hii imechukua muda mrefu lakini zipo sababu ambazo zimesababisha tuweze kufikia hapo. Kwanza kabisa barabara hii yule Mkandarasi ambaye alikuwa amepewa ilitokea bahati mbaya akafariki dunia. Kwa hiyo, tukawa na tatizo unajua ikishakuwa Mkurugenzi mwenyewe amefariki ni lazima utekelezaji wake utakuwa na tatizo.

Pili, tulikuwa na makubaliano na *OPEC Fund* kwamba wangeweza kusaidia kufadhili mradi huu, sasa imebidi tujenge barabara hii kwa kutumia fedha zetu za ndani. Kwa hiyo, hii ndio sababu ambayo imechangia.

Mheshimiwa Spika, lakini tunao mkataba, Mkandarasi anapokuwa amechelewesha tutatoa tozo mwisho atakapomaliza kazi hii. Kwa hiyo tuna mahali ambapo na sisi Serikali itapata fidia. Kwa hiyo Serikali haiwezi kusema inaona aibu kwa sababu barabara nzima kilomita 317 tayari tumeshajenga kilomita 260 hii ni hatua nzuri. Nilitegemea Mbunge utupongeze kwamba Serikali imeanza kufanya kazi ambayo ipo nzuri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, la pili, suala la *TANROAD* kufanya matengenezo wakati inajengwa barabara hilo ni la msingi, tutawaelekeza waendelee kuwa wanafuatilia, wahakikishe kwamba barabara hii inapitika muda wowote na hasa kipindi cha masika. Kwa hiyo, suala hilo tutalishughulikia.

MHE. SELEMAN S. JAFO: Mheshimiwa Spika ahsante sana. Kwa kuwa barabara hii ya Ndundu - Somanga ndiyo inaenda Kusini na ukifika Rufiji ukija Dar es Salaam kuna barabara inayopita Mloka kuja Kisarawe mpaka inaingia Dar es Salaam na kwa kuwa, barabara ya Kisarawe, Maneromango ya kilomita 54 imefanyiwa upembuzi yakinifu tayari. Ni nini *commitment* ya Serikali kuhakikisha kwamba katika mwaka huu wa Bajeti inatenga Bajeti kwa ajili ya kujenga ile barabara ya kilomita 54 kutoka Kisarawe mpaka Maneromango?

SPIKA: Haya, mimi nilifikiria ni barabara hiyo hiyo kumbe iko nytingine, Majibu Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimwombe Mheshimiwa Selemani Jafo kwa sababu sasa ndiyo tupo kwenye mpango wa kuandaa mipango ya mwaka unaofuata, suala la barabara ya Maneromango kwenda Kisarawe litazingatiwa kwenye mpango huo.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza. Napenda kumwuuliza Waziri kwamba wakati wa ziara ya Rais, Novemba mwaka jana, alitoa ahadi ya barabara ya Ndundu – Somanga, kukamilika kabla ya mwezi Juni, 2013. Hivi sasa tunavyozungumza ni mwezi Aprili, 2013 inakaribia kufika katikati. Je, ahadi ya barabara hii kukamilika, iko palepale au unawaambia nini wananchi kupitia Bunge hili? Kwa sababu, mpaka sasa kipande cha kutoka pale Muhoro kwenda Somanga, hata tuta bado halijaanza kukamilika na utengamavu hakuna.

10 APRIL, 2013

Mheshimiwa Spika, na hiyo ni *status* ambayo ipo wiki moja kabla ya Bunge kuanza. Wabunge wote wa Kusini tulikuwa huko na tumeona hiyo hali. Sasa sisi hatutaki kupewa hadithi, tuambieni barabara itakamilika lini?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mangungu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kulikuwa na ahadi ya Rais, kama alivyotamka kwamba, barabara hii ingekamilika inapofikia juni. Lakini nikwambie kitu kimoja kwamba, katika utekelezaji wa barabara kuna mazingira mengi ambayo huwa yanatokea. Serikali, imeingia mkataba na sisi tunasisitiza kwamba, barabara iishe kulingana na mkataba. Sasa inapokuwa Mkandarasi labda anachelewa, sisi tunachukua hatua ya kuchukua tozo, ndio nafasi ambayo tunayo. Tuna *option* nydingine tunaweza kusema basi Mkandarasi amalize Juni tumfukuze, lakini tukimfukuza ujue tutakaa miaka miwili hatujapata mkandarasi na barabara hii haiwezi kukamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni vizuri tumbane Mkandarasi, amalize kazi hii katika mwaka huu wa 2013, ili tuweze kupata barabara, halafu sisi Serikali, itachukua tozo kwa sababu, amechelewesha muda ambao tunakubaliana. Kwa hiyo, tutachukua hatua hiyo kuhakikisha barabara hii inaisha mwaka huu, 2013.

Na. 15

UJENZI WA DARAJA LA JUU (FLYOVER BRIDGE) MWANZA

MHE. MARIA I. HEWA aliuliza:-

Ni muda mrefu sana Wananchi wa Mabatini – Nyamagana, Mwanza wanateseka sana na uvukaji wa barabara waendapo na kutoka maeneo ya sokoni. Je, ni lini ujenzi wa daraja la juu (*Flyover Bridge*) utaanaza:-

10 APRILI, 2013

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu tayari imeliona tatizo la wavuka barabara sehemu ya Sokoni Mabatini – Nyamagana, Mwanza na tayari hatua za kutatua taizo hilo zimeanza kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, katika kutatua tatizo hilo, Wizara yangu kupitia *TANROADS*, imesaini Mkataba wa ujenzi wa daraja la juu la waenda kwa miguu tarehe 2 Machi, 2013 na Mkandarasi anayeitwa *Nordic Construction Limited* wa Dar-es-Salaam. Katika Mkataba huo, Mkandarasi atajenga daraja hilo kwa gharama ya shilingi milioni 888.5 na daraja linatarajiwa kukamilika katika muda wa miezi 6.

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Spika, nipende kutoa shukrani kwa jibu zuri ambalo limetolewa na Wizara hii ya Ujenzi. Jibu ambalo linatupa matumaini watu wa Jimbo la Nyamagana.

Mheshimiwa Spika, nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa vile jibu linasema gharama hizi za milioni 888.5 na daraja hili litajengwa katika miezi 6 ijayo.

Je, hii miezi 6 ndio kusema kwamba, gharama hizi za 888.5 ziko ndani ya Bajeti ya mwaka huu 2012/2013 au 2013/2014?

Mheshimiwa Spika, la pili. Kuna watu ambao wako karibu sana na eneo hilo ambao na wenyewe wako pale kwa muda mrefu.

Je, kuna utafiti uliofanyika kwamba, hawa watu watalipwa gharama za fidia ya kuhama pale, kama itajitokeza hivyo? (*Makofii*)

10 APRIL, 2013

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nipokee shukrani ambazo Mheshimiwa Mbunge, amezitoa. Na mimi ninampongeza pia kwa kuweza kuwatetea wananchi wa Mwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, nimhakikishie tu kwamba, fedha za mradi huu tutaziweka kwenye Bajeti ambayo tutaipitisha ya 2013/2014, kuhakikisha kwamba katika miezi 6 mradi ukikamilika, Makandarasi wanaweza kulipwa.

Mheshimiwa Spika, pili suala la fidia. Suala la fidia liko katika Sheria, kama itabidi kwamba, kuna mtu ambaye ataathirika na ujenzi wa daraja hilo, atalipwa fidia kulingana na Sheria ambayo ipo.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Spika, naomba kumwuliza Waziri wa Ujenzi, kama ilivyo kule Mwanza, kuna ahadi ambayo ilitolewa na Serikali, ni ahadi ya Rais, lakini pia hapa aliyekuwa Naibu Waziri kipindi hicho, Mheshimiwa Mwakyembe, aliahidi kuwa, ujenzi wa daraja la mto Magara, tayari michakato imeendelea, ramani zote zimepatikana na ilitengwa milioni 400 mwaka wa kwanza na milioni karibu 700 mwaka wa pili. Lakini sasa hivi hata kwenye hii Bajeti haipo tena na kule kwenye *Road Board* tumeambiwa kwamba, lile daraja sasa halipo kwenye mpango.

Mheshimiwa Spika, ni lini sasa Serikali, itatekeleza ahadi ya kujenga hili daraja la mto Magara, ambalo wananchi wengi wanaathirika kuvuka? Kipindi hiki Mto wa Mbu ilipopata matatizo, ndio barabara hiyo ilitumika. Tayari *TANAPA* kwa upande wake baada ya kupata ahadi ya Serikali, kujenga daraja, wameshafungua geti kwa upande wa Babati; geti la kuingiza watalii na kutoka kwa hiyo, Serikali, itatimiza lini ahadi hiyo?

10 APRILI, 2013

SPIKA: Unajua, swali hili ni lingine kabisa. Mkijibiwa nusunusu mkubali. Nilikuwa naogopa, suala la Nyamagana na huko Babati, wapi na wapi? Kwa hiyo, naomba Naibu Waziri, nadhani unayajua hayo yote. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Soni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nilihakikishie Bunge hili kwamba, ahadi zote za Rais, ahadi zile ambazo ziko kwenye llani na ambazo Rais pamoja na Viongozi wa Kitaifa wamesema, tutazitekeleza. Ndio maana sasa hivi Wizara yangu inajenga karibu kilometra 11,174 za barabara, hizi ni zote ambazo ziko kwenye llani pamoja na ahadi za Viongozi wa Kitaifa. Kwa hiyo, nikuhakikishie kwamba, daraja hilo ambalo Mheshimiwa Rais aliliagiza, litatekelezwa.

Kwa hiyo, naomba sana uiunge Bajeti yetu ya Wizara ya Ujenzi tutakayoipitisha, tuweze kuona ni namna gani tutajenga daraja hilo.

Na. 16

Utafiti Kwenye Kilimo Kwanza

MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE aliuliza:-

Serikali, hutilia mkazo sana suala la "Kilimo Kwanza, kama ukombozi kwa mkulima. Na ili kufanikisha azma hiyo, ni lazima Serikali, ifanye utafiti wa kutosha kwa kila Wilaya, ili kujua aina ya udongo, mbolea na mbegu inayohitajika:-

(a) Je, Serikali, inatoa kauli gani kuhusu wakulima walionyimwa pembejeo Wilayani Karatu kwa kisingizio cha kwamba, ni lazima wachukue seti nzima ya pembejeo (*Package*) wakati Wataalam wamethibitisha kuwa udongo wa Karatu hauhitaji mbolea ya Minjingu?

(b) Je, nini nafasi ya Maafisa Ugani katika maeneo yetu kama ushauri wao hausikilizwi na Serikali?

(c) Je, Serikali, ina dhamira ya dhati ya kumkomboa mkulima kwa dhana ya "Kilimo Kwanza" ikiwa wananchi wa Karatu walioomba pembejeo ni 43,077 na waliopata ni 250 tu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA
alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Israel Yohana Natse, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo , Chakula na Ushirika, hutoa Waraka wa Utekelezaji wa Mpango wa Ruzuku kwa utaratibu wa Vocha kila msimu wa kilimo. Waraka huo, pamoja na mambo mengine, unasisitiza kila Kaya itakayonufaika kupatiwa seti (*Package*)ya Vocha tatu, kama ifuatavyo:-

(1) Vocha moja ya mbegu bora za mahindi yaani Chotara au mbegu mchanganyiko.

(2) Vocha moja ya mbolea ya kupandia *DAP* au Minjingu Mazao.

(3) Vocha moja ya mbolea ya kukuzia.

Mheshimiwa Spika, lengo la kuwapatia Wakulima Vocha tatu, ni kukamilisha mahitaji halisi ya uzalishaji wa mazao kwa tija kwa kila ekari itakayopandwa kwa kufuata Kanuni bora za kilimo. Taarifa za kiutafiti kutoka katika Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha Seliani, kilichopo Arusha, zimethibitisha upungufu wa madini ya "*Phosphorus*" katika udongo, Wilayani Karatu.

Hivyo, ili kuleta tija na kuongeza uzalishaji ni lazima mbolea za kupandia, ikiwemo Minjingu Mazao, zitiliwe mkazo. Aidha, hakuna uthibitisho kisayansi kwamba, mbolea aina ya Minjingu Mazao, haihitajiki katika Wilaya nzima ya Karatu.

(b) Mheshimiwa Spika, ushauri wa Maafisa Ugani, unafuatwa na kufanyiwa kazi na wakulima, lakini ushauri huo unatakiwa kuendana na tafiti za mara kwa mara kwani, hali ya udongo huwa inabadilika kutokana na shughuli na matumizi ya ardhi.

Aidha, inashauriwa Maafisa Ugani na wadau wengine wa kilimo, wafanye mawasiliano ya karibu na Watafiti, ili kupata Taarifa mpya za utafiti na kuzipeleka kwa wakulima pamoja na watafiti, ili kuhakikisha kuwa matokeo ya tafiti zao yanawafikia Maafisa Ugani na wakulima kwa ujumla, ili yatumike kuboresha kilimo.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali, ina dhamira ya dhati kumkomboa mkulima kupitia mipango na mikakati mbalimbali ikiwemo Dira na Dhana ya KILIMO KWANZA. Mojawapo ya mipango hiyo, ni utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya pembejeo za wakulima.

Aidha, katika kipindi cha miaka 5 kuanzia 2008 hadi 2013, jumla ya Kaya 91,250 zilinufaika na utaratibu huu wa ruzuku ya pembejeo za kilimo katika Halmashauri ya Wilaya ya Karatu. Hata hivyo, kwa mwaka 2012/2013 ni Kaya 250 tu, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, ndizo zilizonufaika na pembejeo za ruzuku, kutokana na Kaya nyingine kukataa kuchukua seti tatu za vocha, kama Waraka wa utekelezaji wa Mpango wa Ruzuku, unavyoelekeza.

MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Sheria inataka *package*, lakini *package* ni kitu kimoja na hali halisi katika *site* ni kitu kingine. Ili kutaka kujua uhalisia mwaka 2009/2010 *TFA* ina tani

10 APRILI, 2013

30 za mbolea, mifuko 30,000 na baadhi ya Ofisi za Vijiji. Pale inapoonekana mbolea hii inalazimishwa, wananchi wamekuwa wakiiza au wakiweka kutegea maji katika maeneo ya Eyasi.

Mheshimiwa Spika, swalii. Je, Serikali, haioni kwamba, kuna haja ya kutoa pembejeo ya ruzuku kwa kuzingatia hali ya rutuba ya eneo husika na kiwango cha mvua katika eneo husika?

Mheshimiwa Spika, la pili. Je, ni lini Serikali, itafanya utafiti wa kina katika Wilaya ya Karatu, Vijiji vyake na Kata zake, ili kutoa pembejeo stahiki katika eneo hilo, badala ya kuwaadhibu wananchi wangu?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:
Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mchungaji Natse, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi, kabla ile mbolea hajijatolewa, tathmini ya mahitaji, kwa maana ya ile mbolea yenyewe kule inaenda kutoa mchango gani kwenye kurutubisha ardhi, lazima ifanyike, vinginevyo huwezi kupeleka mbolea bila kuangalia hiyo.

Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Natse kwamba, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi Kituo chetu cha Seliani, kimeshafanya kazi utafiti kwenye Wilaya ya Karatu na maeneo ya Babati na maeneo mengine yote yale na wamekuja na tathmini ya namna ya kuongeza tija katika ardhi, lakini kwa matumizi bora ya mbolea.

Mheshimiwa Spika, na ndio maana tumehimiza kwamba, katika matumizi bora ya mbolea, ni lazima Wagani na wananchi na sisi wote kwa pamoja kama Viongozi, tushirikiane kuhakikisha kwamba, ile mbolea ikienda ni lazima iende na matumizi bora. Ile mbolea hata ukipeleka magunia mangapi, kama haina matumizi bora, tutakuwa hatupati kitu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nimsihi tu Mheshimiwa Natse kwamba, Kituo cha Seliani na Kituo chetu cha Mlingano, kimefanyia kazi mahitaji ya *soil fertility* ya Wilaya ya Karatu. Tunaendelea kuyafanyia kazi kwa sababu, mahitaji ya mbolea yanaendelea kubadilika kwa sababu ya matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie tu kwamba, hali hiyo inaendelea kufanyika na mbolea ile imethhibitika. Isipokuwa inataki matumizi bora ambayo sisi kwa pamoja wote, tunatakiwa tusimamie matumizi yake.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, tatizo la vocha limekuwa ni kero kubwa sana kwa kule Korogwe Vijijiini, watu wengi wanapelekewa vocha za mbegu, lakini zikipandwa hazioti.

Je, Serikali, ina mpango gani wa kurudisha gharama za wale ambaao wamepewa vocha ambazo zikipandwa mahindi hayaoti?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba nijibu swalii la Mheshimiwa Profesa Maji Marefu Ngonyani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo la kwamba, mbegu hazioti, hili ni tatizo lingine kabisa wala halihusiani na mfumo wa vocha. Inawezekana kwamba, katika ugawaji wa mbolea, mbegu hizi zilizotolewa ni mbegu ambazo hazikufuata utaratibu wa kuwa ni mbegu bora na kwamba, zimepita katika mfumo huo kwa namna ya ajabu ajabu.

Mheshimiwa Spika, sisi Wizara ya Kilimo tuna taasisi inaitwa *Tanzania Official Seed Certification Institute (TOSCI)*, ambayo kazi yake ni kuhakikisha kwamba, mbegu zinazowafikia wakulima ni mbegu bora. Tulichoomba kwenye Bajeti ya mwaka huu, na Waziri atakapokuja wiki ijayo atakuja kuomba hilo kwamba, tupatiwe fedha zakutosha kwa ajili ya kuiimarisha *TOSCI* waweze kufika mpaka kwenye maeneo

10 APRIL, 2013

haya ya wakulima, kuhakikisha kwamba, mbegu iliyotolewa ni ile sahihi na haikupita kwa wajanja wajanja ambao wanafikisha mbegu zisizokuwa na ubora kwa wakulima wetu.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko makubwa sana kuhusiana na ubadhirifu kwenye mfumo mzima wa mbolea ya ruzuku. Bunge lako Tukufu, liliomba *CAG* afanye ukaguzi maalum katika Bajeti nzima ya mbolea ya ruzuku na Serikali, ilikubali. Ni lini Serikali, italeta Taarifa hiyo Bungeni, ili iweze kujadiliwa?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli, tumeshamwomba *CAG* afanye ukaguzi wa kina kuhusu suala hilli maana liko katika Mikoa mingi hapa Tanzania, kwa hivi sasa, yako mambo mengine ambayo yanazidi kuongezeka. Sasa niseme kwamba, zoezi hili bado halijakamilika na ninadhani ni kutokana na ufinyu wa Bajeti.

Mheshimiwa Spika, lakini hata juzi, nilikuwa naongea na *CAG* mwenyewe ni kwamba, zoezi hili linaendelea kufanyiwa kazi na litakapokamilika, Taarifa Kamili itatolewa. Lakini pamoja na zoezi hili kuendelea, wale ambao wamebainika kuwa wameshiriki katika ubadhirifu, wameendelea kuchukuliwa hatua kila wakati, inapobainika.

Mheshimiwa Spika, zoezi hili linafanyika ili kutusaidia kujua mfumo mzima unavyofanya kazi, ni wapi kuna mianya ya kufanya ubadhirifu? Maana mianya iko katika ngazi zote, kuanzia kwa mkulima ambaye, mara nyingine anarubuniwa, lakini pia na kwa Watendaji. Kwa hiyo, *CAG* yeye ana-audit mfumo mzima; itakapokamilika naahidi kabisa *CAG* atatoa Taarifa hii.

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Mheshimiwa Spika, kwa vile zao la mpunga limeanguka bei, hasa Mbarali, kutokana na Serikali, kuagiza mchele kwa wingi kutoka nje ya nchi.

10 APRILI, 2013

Wananchi wa Mbarali na wakulima ambao waliweka zao la mpunga kwa wingi stoo, ili kusubiria bei walao iongeazeke, sasa hawana chakufanya.

Je, Serikali, iko tayari kuwasaidia wananchi hawa na wakulima hawa kupata soko la zao la mpunga nje ya nchi?

SPIKA: Mheshimiwa Kilufi, lilikuwa swali la vocha na mbolea, sasa nikadhani umeweka mbolea mbaya kwa hiyo, bei imeshuka? Sasa naomba usijibiiwe hilo swali, liko nje kabisa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Josephat Kandege, swali linalofuata?

Na. 17

Bei Mahindi

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE aliuliza:-

Bei ya mahindi inayotolewa na Serikali, mara nyingi haitabiriki kwani wakati mwingine inakuwa ikitolewa kwa kuchelewa sana na kutomnufaisha mkulima.

(a) Je, Serikali, ina mpango gani wa haraka wa kumhakikishia Mkulima Mdogo bei, kwani wakati mwingine hulazimika kuyauza mahindi yakiwa bado shambani?

(b) Mkulima wa mahindi Rukwa, aliuza gunia la mahindi la *Kg 100* kwa *35,000/=*; lakini alilazimika kulinunua gunia hilo hilo kwa *75,000/=* mpaka *92,000/=* kwa maeneo mengine. Je, Serikali, inasema nini kwa hali kama hiyo kwa lengo la kumkomboa Mkulima?

(c) Je, Serikali, iko tayari kutafiti bei halisi ya soko la mahindi, hasa ikitiliwa maanani bei ya kilo ya unga imefikia hadi *1,300/=*?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Chakula, Kilimo na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephat Kandege, Mbunge wa Kalambo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa mkulima mdogo wa mahindi anapata soko la uhakika la mazao yake na wakati mwingine asilazimike kuuza mahindi yake yakiwa shambani Serikali, inatengeneza mikakati mbalimbali ikiwemo kuondoa zuwio la kuuza mazao nje ya nchi kuanzia mwezi Januari, 2012 limeanza kutekelezwa na kuwaruhusu wakulima wadogo na wafanyabiashara wa kati na wakubwa, kuuza mazao yao nje ya nchi kwa bei nzuri, bila usumbufu wowote.

Mheshimiwa Spika, katika azma nzima ya kumsaidia mkulima kupata bei nzuri ya mazao yake Serikali, inaendelea kuimarisha mfumo wa stakabadhi za maghala kwa mazao yanayohifadhi, ikiwa ni hatua muhimu ya kuingia kwenye soko la mazao (*Commodity Exchange*).

Aidha, katika kuhakikisha mkulima ananufaika na mazao yake Viongozi wa Mkoa na Wilaya, wamehimizwa kusimamia na kudhibiti tabia ya baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu ya kununua mazao ya wakulima yakiwa shambani au maeneo yasiyo rasmi kwa ajili ya ununuzi wa mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa tofauti za bei zinazojitokeza wakati wa mavuno na wakati wa uhaba Serikali itaendelea kuwajengea wakulima uwezo na mbinu bora za kuhifadhi mazao ili waweze kuhifadhi chakula cha kutosha kwa ajili ya mahitaji ya kaya zao kwa mwaka mzima na ndipo wauze ziada inayobaki.

Aidha makundi yote ya wananchi ikiwemo walaji hasa katika maeneo yenye uhaba wa chakula wataendelea kuhamasishwa kuhifadhi chakula na kuzalisha mazao mbadala kulingana na mahitaji ya kaya zao kwa matumizi ya mwaka mzima ili kuondokana na shida ya chakula hasa katika kipindi ambacho bei imepanda sana.

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara wasio na maadili pia wamekuwa wakichangia kupanua pengo baina ya bei anayopata mkulima na bei anayouziwa mlaji wa mwisho. Wizara yangu inajipanga kutengeneza mikakati ya ufuatiliaji wa biashara za mazao kwa karibu zaidi ili kuweza kudhibiti tabia hii mbaya ambayo inachangia kupanda kwa gharama za maisha.

Mheshimiwa Spika, ni kweli bei ya unga imepanda katika maeneo mbalimbali nchini, Wizara yangu inafanya kazi ya kutathmini mwenendo wa bei za vyakula kuititia idara ya usalama wa chakula katika kuboresha mfumo wa usimamizi na tathmini ya kazi tuliojiwekea ambapo majukumu haya yanafanyiwa maboresho makubwa.

Aidha kwa kushirikiana na wadau wengine kwa wakati huu Wizara pia inafanya utafiti wa bei halisi ya soko la mahindi na unga wa sembe ili kuainisha sababu za kupanda kwa bei ya unga na kushauri hatua muafaka za kuchukuliwa ili kuhakikisha mkulima wa mahindi anapata bei nzuri ya mahindi yake na wakati huohuo walaji wanapata unga wa sembe kwa bei watakayoimudu. (*Makofii*)

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

10 APRIL, 2013

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake amekiri kwamba katika kuondoa zio tangu 2012 imetokea.

Je, Serikali inanihakikishia na kulihakikishia Bunge hili kwamba zio hilo litakuwepo kwa kudumu au lilikuwa kwa muda mchache tu.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwa kuwa mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba bei ya sembe imepanda mpaka kufika shilingi 1300/=.

Je, Serikali itakuwa tayari kupandisha bei ya mahindi walau kufika nusu ya bei hiyo.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakiula na Ushirika napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephat S. Kandege, maswali ya nyongeza kama ifuatavyo.

Mheshimiwa spika, mkakati wa kuondoa zio ili wakulima waweze kuuza mahindi yao kwa upana zaidi lengo lake lilikuwa ni kuhakikisha kwamba mahindi yale yanapata ushindani. Kwa hiyo, bei ikaongezeka na kweli iliongezeka. Lakini nia ya kuweka zio ilikuwa pia ni nia ya kwamba bei ikiongezeka sana wakulima walikuwa wanauza mahindi yao yote na akiba ilikuwa haibaki ndani matokeo yake baada ya mahindi yote kutoka nje ya nchi Serikali ilikuwa inalazimika tena kuleta mahindi mengine kwa ajili ya njaa.

Mheshimiwa spika, kwa hiyo hili zio litabaki kwamba wakulima watapata nafasi hiyo ya kuuza mazao yao kadiri itakavyoonekana inafaa lakini wakati huo huo pia Serikali kama nilivyosema itaendelea kuhimiza kwamba wakulima kwamba lazima waache akiba ili kuondokana na tatizo la baadaye tena kurejea Serikali mahindi hayo hayo yanarejea huko huko kwa wakulima kwa ajili ya kukidhi tatizo la njaa.

Mheshimiwa spika, hili tatizo la bei ya sembe ni kubwa, ni kweli kwamba kwa sisi Serikali ilikuwa inanunua mahindi imejipanga kununua kwa bei ya kama shilingi 400/= tukaishia kununua kwa shilingi 600/= kwa sababu wafanya biashara walikuwa wanunuwa mahindi, wengine walikuwa *wan-hedge* kwa maana walikuwa wanahifadhi ili mahindi yapande bei sana matokeo yake mahindi yamepanda bei na unga umepanda bei.

Tulichofanya Serikali ni kwamba tumetoa mahindi kwa bei nafuu ili unga ushuke bei, bado wafanyabiashara wamefanya ndivyo sivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nimhakikishie Mheshimiwa Kandege na wazalishaji wote wa mahindi kwamba tutaendelea kuhakikisha kwamba mahindi yanauzwa yananunuliwa kwa bei nzuri kwa maana mwaka huu tunataka tuanje na bei ya juu kidogo lakini pia tutaendelea kuhimiza uwajibikaji ili bei ya mahindi isipande kuwapa manufaa kwa wafanyabiashara wasio na uaminifu. (*Makofi*)

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Spika, nashukuru moja ya tatizo kubwa linalompata mkulima wa mahindi ni uhifadhi wake kwa maana ya kwamba hakuna maghala ya kutosha katika vijiji na hasa katika jimbo la Mbanga Mashariki na kwa mantiki hiyo tumeanzisha vikundi vyta wakulima. Nilitaka kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kama anaweza kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mbanga katika kuongeza uwezo wa maghala kwa maana ya kuyajenga katika Wilaya ya Mbanga.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa naomba ujibu kwa kifupi tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gaudence K. Kayombo, Mbunge wa Mbanga, kama ifuatavyo.

10 APRIL, 2013

Mheshimiwa Spika, ni kweli anavyosema kwamba kwenye maeneo yake ya Mbinga hii hoja ya kwamba Serikali iangalie namna ya kupanua mfumo wa kuhifadhi kwa kushirikiana na Halmashauri limetufikia na tunalifanyia kazi.

Jambo ambalo tutakavyokwenda ni kwamba kwenye maeneo yote haya tutahimiza ujenzi wa *silos* hizi za gharama nafuu ili kwa hatua ya kwanza mkulima aweze kuhifadhi mazao yake pale katika utaratibu ambao utasajili mazao yako pale kabla hayajanunuliwa. Kwa namna hiyo hata upotevu wa mazao utakuwa ni mdogo sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni jambo ambalo linafanyiwa kazi kwa Halmashauri zote ambazo zinazalisha mahindi kuwa na huu utaratibu wa Silos au hifadhi hizi za vihenge vyenye bei nafuu. (*Makofii*)

SPIKA: Tuendelee na Wizara ya uchukuzi Waheshimiwa.

Na. 18

Usafiri wa Ndege Dar es Salaam – Dodoma

MHE. CATHERINE V. MAGIGE (K.n.y. PINDI H. CHANA)
aliuliza:-

Serikali hutumia gharama kubwa sana kusafirisha Maafisa wa Serikali na Mawaziri kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma wakati wa vikao la Bajeti.

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kuwa kunakuwepo na ndege kutoka Dar es Salaam – Dodoma ili kupunguza gharama za mafuta na muda.

10 APRILI, 2013

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika , kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa ya usafiri wa anga kati ya Dar es Salaam na Dodoma ambao ni wa ratiba yaani *scheduled air services*ni upatikanaji wa abiria na mizigo ya kutosha ili kuyawezesha makampuni ya ndege kutoa huduma kati ya miji hii na kutoza nauli ambayo wasafiri wataimudu na itakayoyawezesha makampuni hayo kupata faida. Kwa sasa huduma ya ndege kati ya Jiji la Dar es Salaam na Dodoma hutolewa na ndege ndogo ndogo za mashirika binafsi ya *Coastal Aviation Flight Link*.

Mheshimiwa Spika, huduma ya usafiri wa anga kati ya Dar es Salaam na Dodoma pia hutolewa na kampuni zingine kwa kukodisha. Aidha kuwepo kwa usafiri wa barabara wa kuaminika kati ya Dar es Salaam na Dodoma kumechangia kupungua kwa abiria na mizigo kati ya miji hii kwani wengi wanatumia usafiri huu wa barabara.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kubuni mikakati ambayo itauwezesha mji wa Dodoma kuunganishwa na Jiji la Dar es Salaam na miji mingine kwa kujenga kiwanja kipycha Msalato na kuimarisha viwanja vyta ndege katika miji mingine nchini.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru pamoja na majibu ya Naibu Waziri nina swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali kwa muda mrefu ilitoa ahadi ya kujenga kiwanja cha ndege cha Msalato cha hapa Dodoma na hadi sasa ujenzi huu haujaanza. Je ni lini Serikali itaanza rasmi ujenzi wa Kiwanja hiki cha ndege cha Msalato.

10 APRILI, 2013

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Catherine Magige, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, uwanja wa ndege wa Msalato ni mionganoni mwa viwanja kumi ambavyo kwa sasa tumepata fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na tathmini ya mazingira ili tuweze kujua mahitaji ya kifedha na baadaye tukishakamilisha zoezi hilo tuweze kuomba fedha kwa njia ya Bajeti au namna nyingine ya kuanza ujenzi wa uwania huo.

MHE. SALUM K. BARWANY: Mheshimiwa Spika, hapana swali la mwisho ndiyo nitauliza swali la nyongeza.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa swali la msingi limegusia gharama kubwa za kusafirisha maafisa wa Serikali pamoja na Mawaziri kuja Dodoma. Sasa swali langu ni kwamba pamoja na gharama za usafirishaji wa hawa viongozi wa Serikali na Mawaziri kuna gharama nyingine pia ambazo zinaiingizia Serikali fedha nyingi kwa mfano gharama za makazi. Mawaziri na maafisa wa Serikali wana nyumba Dar es Salaam na wana nyumba Dodoma hizo pia ni gharama ambazo zinaongeza mzigo mkubwa kwa Serikali.

Je, Serikali sasa haioni ni wakati muafaka wa kuamua aidha Makao Makuu ya Serikali yawe Dodoma au Dar es Salaam ili kupunguza gharama hizi nyingine, ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Swali halihusiani, lakini unaweza kujibu ukitaka, jibu tu ukitaka.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo.

10 APRILI, 2013

Mheshimiwa Spika, uendeshaji wa Serikali kwa vyovyote vile unakuwa na gharama hata kama ni Dar es Salaam au Dodoma.

Kwa hiyo, kwamba mazungumzo ya gharama ipo kwa sababu Serikali inaendeshwa hapa Dodoma sidhani kama ni la msingi sana lakini la msingi tu ni kwamba Serikali inachukua kila hatua inayoweza kuhakikisha kwamba azma yake ya kuhamishia Makao Makuu Dodoma na shughuli zote za Serikali kuendeshewa hapa inatekelezwa.

MHE. ENG. MOHAMED H. J. MNYAA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Suala la uwanja wa ndege wa Dodoma na usafiri kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma limezungumzwa miaka saba iliyopita bila mafanikio kwa bahati nzuri hivi sasa zipo ndege ndogo ndogo kama jibu lako Mheshimiwa Waziri kwamba zinakuja Dodoma lakini bei ni kubwa mno kiasi ambacho kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma ni 500,000/= kuja tu na kuna ndege nyiningine ni 300,000/=.

Je, Mheshimiwa Waziri Wizara yako inaingilia kati namna gani mambo haya ya bei na kwa masafa ya kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma hata kukawa kuna-variation kubwa ya namna hiyo?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Mnyaa la nyongeza kwamba namwomba tu awe na subira ya dakika moja kwa sababu swali linalofuaata linaulizia jambo hili hili naomba nitumie nafasi hiyo kuyajibu yote kwa pamoja.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri unaruhusiwa, tunaendelea na swali linalofuata.

10 APRILI, 2013

Na. 19

Chombo Kinachosimamia Bei za Usafiri wa Anga Nchini

MHE. MHONGA S. RUHWANYA aliuliza:-

Serikali imekuwa ikisimamia bei za usafiri nchini kuitia SUMATRA kwa usafiri wa majini na barabarani. Je, ni chombo gani kinasimamia bei ya usafiri wa anga nchini?

WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mbunge wa viti maalum kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, chombo ambacho kinasimamia bei ya nauli za ndege nchini ni Mamlaka ya Usafiri wa Anga yaani Tanzania *Civil Aviation Authority*. Mamlaka hiyo ilianzishwa mwaka 2003 kwa Sheria ya usafiri wa anga ya mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, kimsingi nauli za ndege kama zilivyo nauli nyingine za vyombo vyta usafiri hapa nchini zinapangwa na mashirika ya ndege kulingana na ushindani katika soko.

Hata hivyo mashirika hayo huwasilisha mchanganuo wa gharama na mapendekezo ya nauli kwa mamlaka ya usafiri wa anga kabla ya kuanza kutumika.

10 APRILI, 2013

Mheshimiwa Spika, mikataba ya huduma za usafiri wa anga kati ya nchi na nchi yaani *Bilateral Air Service Agreement* (BASA) na miongozo mbali mbali ya shirika la Dunia la usafiri wa anga *The International Civil Aviation Organisation* inaelekeza kwa pamoja utaratibu wa kusimamia mashirika ya ndege na watoa huduma wengine wa usafiri wa anga.

Hivyo ni kwa mantiki hii nauli na viwango vya huduma husimamiwa na mamlaka yetu ya usafiri wa anga.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi ushindani katika soko ndiyo sababu kubwa ya kupanga na kushuka kwa nauli za usafiri wa anga. Pale ambapo kuna ushindani thabitii na ulishuka na pale kwenye ushindani dhaifu nauli huwa juu.

Mheshimiwa Spika, endapo malalamiko yatatokea kuashiria kuvunjwa kwa taratibu na miongozo iliyopo Mamlaka ya Usafiri wa Anga huingilia kati na wakati mwingine Kamisheni ya ushindani huchukua hatua.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante *Tanzania Civil Aviation Authority TCAA Act* ya 2003 inasimamia usalama wa usafiri wa anga lakini kanuni zilizotungwa mwaka 2009 kipengele kidogo cha 5 (6) (1) kinataka mashirika yote ya ndege yakae na wasafiri wapange nauli halafu ndiyo wapeleke *TCAA* kwamba wamepanga nini.

Kitu ambacho hakijafanyika na ndiyo maana inapotokea shirika moja linatoa huduma nchini inakuwa *monopoly* wanapanga bei wanavyotaka hali ambayo inamwumiza Mtanzania.

Je, Serikali haioni kwamba kuna haja sasa ya kuangalia kama inawezekana *SUMATRA* washiriki katika kusimamia bei za ndege ili kuondoa ile mabadiliko ambayo yanakuwa ya bei za juu ambazo Mtanzania wa kawaida hawezikumudu au Sheria ibadilishwe kwa sababu inatoa *loop hole* kwa mashirika haya ya ndege kufanya wanavyotaka? Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nimesema hicho hicho ambacho amekisema kwamba Mashirika haya kabla ya kuanza kutumia nauli wanazopendekeza hutoa mchanganuo wa gharama watakazoingia na kupeleka mapendekezo hayo kwa Mamlaka yetu ya usimamizi wa Usafiri wa anga *TCAA*.

Lakini kwa sababu ya usafiri wa anga kuwa na masharti mengi ya kimataifa ambayo sisi pia Tanzania ni tunaridhia makubaliano hayo ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, suala la ku-*impose* bei kama au kuweka viwango vya juu na chini khalitumiki sana kwa sababu tofauti na ilivyo katika tuseme usafiri wa barabara. Usafiri wa barabarani ni huduma ya msingi kama vile yalivyo maji au umeme ambao Watanzania wengi asilimia karibia 100 wanautumia.

Kwa hiyo, katika huduma hii ya msingi ndiyo *regulation* inapoweka *series* za nauli. Sasa kwenye usafiri wa anga soko lenyewe kama nilivyosema lina *regulate*.

Tumeona mfano *Fast Jet* wamekuja *monopoly* iliyokuwapo ya wale *Precision* na kampuni nyingine imepungua nauli zake hivyo hivyo watoa huduma wakiongezeka kwa vyovyyote vile nauli zitashuka, watoa huduma wakipungua nauli zitaongezeka ziko sababu zingine ndogo ndogo ambazo zinasababisha bei za *ticket* za ndege kwenda mahali kwingine kuwa kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kama uwanja wa ndege ambako mtoa huduma anataka kwenda hauna tuseme jambo moja tu mafuta. Kwa hiyo, ndege kutoka Dar es Salaam kwenda kwenye uwanja ule inabidi ijaze mafuta mengi kwa ajili ya kufanya safari ya kwenda na kurudi ambavyo ingekuwa kwenye uwanja ule kuna mafuta ndege ingeenda na mafuta kidogo ya kuifikisha ikabeba abiria wengi zaidi ili iweke mafuta kule irudi na abiria wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sababu hizi zinamfanya sasa *oparetor* yule aongeze nauli kidogo ili ku-cover hizo ghamara anazozitumia wakati wa kwenda na kurudi.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuwa zamani bei zilikuwa zinapanda za nauli za mabasi kwa sababu ya barabara nydingi zilikuwa mbovu lakini sasa hivi Serikali ya CCM imejitahidi sana kuwa na barabara za lami nydingi.

Je, kutokana na hiyo kwa nini Serikali isidhibiti bei za usafiri wa barabara kuliko inavyoenda holela holela sasa hivi?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, sijui kama nimelipata sawa sawa swali la nyongeza la Mheshimiwa Diana Chilolo kwamba barabara nzuri kwa nini bei hazishuki?

10 APRIL, 2013

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge anaweza kuuliza tena, uliza swali tena mheshimiwa Diana M. Chilolo.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, zamani nauli za mabasi zilikuwa kubwa kwa sababu barabara zilikuwa mbovu, mabasi yalikuwa yanatumia muda mrefu kusafiri, kwa mwendo wa masaa manne ilikuwa masaa nane. Lakini sasa hivi sasa serikali ya CCM imefanya kazi nzuri kutengeneza barabara kwa kiwango cha lami, kwa nini sasa bei zisishuke wakati safari sasa ni fupi?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Diana Chilolo kwanza kwa kuipongeza serikali kwa kazi nzuri kubwa inayofanya. Mheshimiwa Spika, ni kweli anachokisema kwamba barabara zikiwa nzuri, muda wa kusafiri hupungua na hivyo wenye kutoa hiyo huduma hawapaswi kupandisha sana nauli za tiketi.

Jambo moja tu ambalo kwa sasa linachangia kupanda kwa tiketi za mabasi ni ongezeko la gharama za mafuta, kwa sababu gharama za mafuta zinaendelea kupanda karibu kila siku. Hata kima cha chini cha mishahara ya watumishi katika mabasi haya kinaongezwa. Kwa hiyo, kama maongezeko haya mawili yanatokea wenyewe mabasi wanalazimika pia na wao kupandisha nauli angalau kuka-cover hizo nyongeza za gharama za uendeshaji zinazojitokeza.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha, tumezidisha muda tu kwa sababu tu kwamba shughuli nyingine hazipo sana. Nina tangazo la kazi, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Andrew J. Chenge, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo saa saba watakuwa na kikao chao katika ukumbi wa Pius Msekwa B.

Mheshimiwa Katibu wa Wabunge wa *CUF*, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, anaomba niwatangazie Wabunge wote wa *CUF* kuwa kutakuwa na kikao cha leo, mchana baada ya Kuahirisha Kikao cha Bunge. Nadhani

10 APRILI, 2013

baada ya Kuahirisha Kikao cha Bunge, watakuwa na Kikao chao kwenye chumba Namba 227.

Tangazo kutoka kwa Katibu wa Wabunge wa Kanda ya Ziwa, Mheshimiwa Dkt. Titus M. Kamani, anasema Wabunge wote wanaotoka Mikoa ya Mara, Simiyu, Mwanza, Shinyanga, Geita na Kagera, wanaombwa kukutana katika ukumbi Namba C. wa Pius Msekwa, leo sa saba mchana. Anasema ni muhimu mfike kwa wakati ili mmalize kikao chenu mapema. Kwa hiyo hawa watu watahusika kama wanavyostahili. Baada ya kusema hivyo, Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Katibu tuendelee. (*Makofii*)

HOJA ZA KAMATI

KAMATI YA KANUNI ZA BUNGE

Azimio la Marekebisho ya Kanuni za Bunge

MHE. JOB Y. NDUGAI - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KANUNI ZA BUNGE: Mheshimiwa Spika, naomba kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, mapendekezo ya kufanya mabadiliko katika Kanuni za Bunge. Awali ya yote napenda kukupongeza kwa juhudzi zako ulizozifanya katika kufanikisha mapendekezo ya Bunge hili Tukufu ya kuwa na mchakato mpya wa Bajeti ya Serikali.

Vilevile napenda kuwashukuru viongozi pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa kukubali na kuwa tayari kutekeleza mapendekezo ya kuwa na mchakato mpya wa Bajeti ya Serikali.

Napenda pia kuishukuru Kamati ya Kanuni za Bunge, kwa kuandaa mapendekezo ya marekebisho ya Kanuni za Bunge ninazo ziwasilisha leo kwa ajili ya kuitishwa na Bunge hili Tukufu. Ikumbukwe kwamba Waheshimiwa wabunge tumehusishwa katika hatua mbalimbali za kuchambua na kukubaliana kuhusu nini hasa kibadilishwe na kiwekwe sawa katika Kanuni zetu.

Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Bunge, chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge, pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa kutoa ushauri na kufanya maandalizi muhimu ya kuhakikisha utekelezaji bora wa Bunge wa mchakato mpya wa Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mchakato mpya wa Bajeti utaanza kwa Bunge kukaa kama Kamati ya Mipango katika Mkutano wake wa mwezi Oktoba-Novemba kwa kila mwaka, badala ya mwezi Februari, kama ilivyo hivi sasa. Aidha, Mkutano wa Bunge wa Bajeti utaanza mapema mwezi Aprili kwa kila mwaka, kama tutakavyofanya mwaka huu na kuhitimishwa kabla au ifikapo tarehe 30 Juni, kwa kila mwaka na kazi za Bunge za *oversight* kuititia Kamati zake, zitaendelea kufanyika kama kawaida, kama ilivyokuwa kabla ya mabadiliko yanayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, sababu za kuwa na mchakato mpya wa Bajeti. Kwa mujibu wa utaratibu uliokuwepo kabla ya mabadiliko haya yanayopendekezwa, mjadala wa Hotuba ya Bajeti ya Serikali unapomalizika, Spika alikuwa analihoji Bunge litoe Uamuzi wake wa kuitisha au kutopitisha Bajeti ya Serikali, kwa ajili ya kukidhi matakwa ya Ibara ya Katiba, ibara ya 90(2) (b).

Baada ya kutoa Uamuzi wa kuitisha Bajeti ya Serikali, Bunge lilikuwa linaendelea kujadili utekelezaji wa Wizara zote, lakini mjadala huo ulikuwa hauna tija yoyote, kwa sababu haukuwa unatoa mchango katika kuboresha Bajeti husika, kutokana na Bajeti hiyo kuwa imekwishapitisha na Bunge.

Vile vile, mjadala huo ambao ulikuwa unaendelea hadi mwishoni mwa mwezi Agosti, ulikuwa unainyima Serikali fursa ya kuanza kukusanya mapato kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na shughuli zinginezo kulingana na Bajeti iliyopitishwa na Bunge. Aidha, kwa mujibu wa utaratibu huo, utekelezaji wa Serikali wa Bajeti ambao ulipaswa kuanza tarehe 1 Julai, mara tu mwaka mpya wa fedha unapoanza, ulikuwa unachelewa kuanza, na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo. (*Makofii*)

Kutokana na hali hiyo, ni dhahiri kwamba, hatua za kubadilisha utaratibu huo zilikuwa ni muhimu kwa ajili ya kuleta tija kwa Serikali na kwa Bunge katika utayarishajii, uwasilishajii Bungeni, na utekelezaji wa Bajeti ya Serikali, kwa ajili ya maendeleo ya wananchi na Nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, faida za mchakato mpya wa Bajeti, mchakato mpya wa Bajeti utaiwezesha Serikali kuanza utekelezaji wa miradi ya Maendeleo, kama vile ujenzi wa miundombinu ya barabara, mapema zaidi kuliko hali ilivyo hivi sasa ambapo, utekelezaji wa miradi hiyo huathiriwa na kipindi cha mvua.

Mchakato huo vilevile utawezesha Kamati za Bunge kutembelea miradi kabla ya kuanza kujadili Taarifa za utekelezaji wa kila Wizara kuhusu Bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata, kabla ya kuanza kujadili Bajeti ya Serikali na kuipitisha.

Mchakato huo pia utawezesha mijadala ya Taarifa za utekelezaji wa kila Wizara kuhusu Bajeti kuwa na tija, kwa kutoa mchango wa kuboresha Bajeti ya Serikali, kupitia Majumuisho yatakayofanywa kati ya Serikali na Kamati ya Bunge ya Bajeti baada ya mijadala hiyo kuhitimishwa.

Mchakato huo vilevile utatoa fursa kwa Serikali, ya kutafakari na kufanya majumuisho kuhusu hoja muhimu zitakazojitokeza kwenye mijadala ya Bunge ya kuchambua Taarifa za utekelezaji wa Wizara kabla ya Hotuba ya Bajeti Kusomwa Bungeni.

Aidha, mchakato huo, utaliwezesha Bunge kupitisha Bajeti ya Serikali, Muswada wa Sheria ya Fedha za Matumizi (*Appropriation Bill*) na Muswada wa Sheria ya Fedha (*Finance Bill*), kabla ya au ifikapo tarehe 30 Juni ya kila mwaka, na hivyo kuiwezesha Serikali kuanza utekelezaji wa Bajeti tarehe 1 Julai, mwaka mpya wa fedha unapoanza.

10 APRILI, 2013

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya marekebisho ya Kanuni za Bunge, ni dhahiri kwamba, utekelezaji wa Mchakato mpya wa Bajeti unahitaji baadhi ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007 zifanyiwe mabadiliko. Eneo mahsusi ambalo la Kanuni hizo linalohitaji kufanyiwa mabadiliko ni sehemu ya Tisa inayohusu, Utaratibu wa Kutunga Sheria Kuhusu Mambo ya Fedha. Naomba kurudia hapa, eneo mahsusi ambalo linafanyiwa mabadiliko, ni Sehemu ya Tisa inayohusu, Utaratibu wa Kutunga Sheria Kuhusu Mambo ya Fedha peke yake.

Mapendekezo ya Kamati ya Kanuni za Bunge kwa ajili ya kuifanyia marekebisho Sehemu hiyo ya Kanuni, yamewasilishwa chini ya Kiambatanisho "A" cha Hotuba hii. Aidha, Ratiba inayoonyesha utekelezaji wa mchakato mpya wa Bajeti, pamoja na maelezo ya utekelezaji wake, kwa Bunge na kwa Serikali.

Pia vimeonyeshwa kwenye Kiambatanisho "B" cha Hotuba hii. Waheshimiwa Wabunge, katika kiambatanisho "A" mtaona kuna mambo mengi yanayohusiana na utaratibu.

SPIKA: Kiambatanisho mtapewa dakika chache zijazo, kwa sababu hawa ndiyo wanaingia kutokana na maagizo yenu jana, inakuja kabla hajamaliza.

MHE. JOB Y. NDUGAI - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KANUNI ZA BUNG: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, muda si mrefu mtapata kiambatisho, zinadurufiwa kwa haraka sana, yanazingatia maoni ambayo miliyatoa jana Waheshimiwa Wabunge, katika mabadiliko ambayo yalikuwepo mwanzo kuhakikisha kwamba kinachokuja ni kile ambacho tulikubaliana hapa mapema. Kwa hiyo, kwa ujumla wake, Kanuni hizi zinashughulika na masuala ya utaratibu kuhusu mambo ya fedha kama nilivyoeleza.

Kwa mfano, fungu la tisini na nne, linalohusu kupokea, kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na serikali wa mwaka unaofuata.

Utaratibu wake wa namna ambavyo mpango huo utawasilishwa kwa Katibu, kwa Bunge, kwa Kamati zake na namna gani suala zima la Mpango wa Taifa utakapojadiliwa ndani ya Bunge, katika kipindi kile cha mukutano wa Oktoba – Novemba.

Fungu la tisini na tano linabaki kama liliyyo, fungu la sitini na sita linazungumzia utaratibu wa ratiba na kuwasilishwa kwa dondo na makadirio ya mapato ya matumizi ya Wizara Mbalimbali, kwa ofisi ya Bunge na utaratibu wake kwa ujumla wake, na namna gani Kamati zitakaa baada ya hapo.

Fungu la tisini na saba linazungumza kwa jumla yake namna ya kazi na mpango mzima utakavyofanyika, kati ya Kamati ya Bajeti na Kamati za Bunge na majukumu ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha anakuwa nayo wakati wa Bajeti.

Fungu la tisini na nane linatoa mamlaka kwa kamati za Bunge kwenda kukagua miradi ya maendeleo iliyotekelvezwa katika mwaka uliopita kabla ya Waheshimiwa Wabunge hamjaja Dodoma, kwa ajili ya Bunge la Bajeti.

Fungu la tisini na tisa, linashughurika na majadiliano ya utekeleza jiji mbalimbali ya Wizara mbalimbali, yatakayofanyika, kabla ya hutuba ya bajeti na utaratibu utakaofuatia, katika uendeshaji wa shughuri za Bunge, ambapo mjadala wa Wizara moja moja utaanziwa na hotuba ya bajeti ya ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, na kufuatiwa na Wizara nyingine zote. (*Makofii*)

10 APRILI, 2013

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo mwanzo, mabadiliko mengine yoyote ni yale kwa kweli ki msingi tulisha shirikishana na mtapata nakala zake muda siyo mrefu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Kanuni ya 152(1) inaelekeza kwamba, Bunge linaweza kupitisha Azimio la kufanya mabadiliko katika Kanuni yoyote kutokana na mapendekezo ya Kamati ya Kanuni za Bunge.

Kwa kuzingatia Kanuni hiyo ya Bunge, napenda kuwasilisha Azimio la Bunge kwa ajili ya kufanya mabadiliko katika Kanuni za Bunge, kwa mujibu wa mapendekezo ya Kamati ya Kanuni za Bunge yaliyowa-silishwa chini ya Kiambatanisho "A" cha Hotuba yangu, kama ifuatavyo:-

KWA KUWA, Kamati ya Kanuni za Bunge imewasilisha mapendekezo ya marekebisho ya Kanuni za Bunge chini ya Kiambatanisho "A" kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 152(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007;

NA KWA KUWA, mapendekezo hayo yamewasilishwa na mimi Naibu Spika, kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 152(2) ya Kanuni hizi;

KWA HIYO BASI, napendekeza Bunge liazimie kwamba, likubali kupitisha mapendekezo ya kufanya mabadiliko katika Kanuni za Bunge, kama yalivyowasilishwa, kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 152(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa Hoja. (*Makofii*)

10 APRILI, 2013

KIAMBATANISHO "A"

MAREKEBISHO YA KANUNI ZA KUDUMU ZA BUNGE, TOLEO LA 2007 [Chini ya Kanuni ya 152(2)]

Kamati ya Kanuni za Bunge inapendekezo kwamba, Sehemu ya Tisa ya Kanuni za Kudumu za Bunge ifanyiwe marekebisho kama ifuatavyo:-

SEHEMU YA TISA

UTARATIBU WA KUTUNGA SHERIA

KUHUSU MAMBO YA FEDHA

94.(1) Bunge kukaa kama Kamati ya Mipango. Katika Mkutano wake wa mwezi Oktoba – Novemba kwa kila mwaka, Bunge kwa siku zisizopungua tano, litakaa kama Kamati ya Mipango ili kukidhi matakwa ya Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba, kwa kujadili na kuishauri Serikali kuhusu mapendekezo ya utekelezaji wa Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika mwaka wa fedha unaofuata.

(2) Katika Mkutano huo, Bunge pamoja na mambo mengine, litafanya shughuli zifuatazo:-

(a) Kupokea, kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali;

(b) kupokea, kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu vyanzo vya mapato ya Serikali; na

(c) kupokea, kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu mapendekezo ya utekelezaji wa Mpango wa Serikali na vipaumbele kuhusu Mpango huo.

(3) Kwa madhumuni ya utekelezaji wa masharti yaliyomo katika fasili ya (1), Serikali itawasilisha kwa Katibu mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali na nakala zitapelekwa na kumfikia kila Mbunge siku saba kabla ya tarehe iliyopangwa kujadili mapendekezo hayo.

(4) Kabla ya mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kuwasilisha Bungeni, mapendekezo hayo yatajadiliwa na Kamati ya Bajeti.

(5) Mjadala kuhusu mapendekezo ya mpango wa Taifa:-

(a) Utatanguliwa na maoni ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti iliyochambua mapendekezo hayo, na maoni ya Kambi ya Upinzani Bungeni;

(b) Utaendelea kwa siku zisizozidi mbili; na

(c) Utahitimishwa na Serikali kwa kutoa maelezo ya ufanuzi katika maeneo mbalimbali yaliyotolewa maoni na ushauri na Wabunge.

(6) Mjadala wa mapendekezo ya Mpango wa Taifa utahusu mambo ya jumla na Wabunge watachangia na kuishauri Serikali kuhusu utekelezaji wa sera za kiuchumi, za kifedha, za kodi na vipaumbele katika mpango wa Bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha unaofuata.

95. Masharti kuhusuMswada, hoja na maombi ya fedha. Bunge halitashughulikia Muswada, hoja au ombi lolote lilitotolewa na Mbunge au Kamati ya Kudumu ya Bunge endapo Mwanasheria Mkuu wa Serikali atathibitisha kwamba, matokeo ya Muswada, hoja au ombi hilo yatakuwa ni:-

(a) Kuweka masharti yanayoanzisha au kuongeza kodi yoyote yanayoweza kuongeza kiwango cha matumizi ya fedha zitakazotolewa kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina

ya Jamhuri ya Muungano au yanayofuta au kupunguza deni lolote linalodaiwa kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano; au

(b) Kubadilisha mishahara, marupurupu au masharti ya utumishi, ikiwa ni pamoja na likizo, usafiri na kupandishwa cheo kwa mtumishi yeyote wa umma au kufanya mabadiliko katika Sheria, Kanuni au taratibu zinazohusu pensheni, kiinua mgongo au marupurupu mengineyo ya mtumishi wa umma au ya mjane, watoto wanaomtegemea au wawakilishi wake.

96.(1) Kuwasilisha dondoona randama za vitabuvya Bajeti. Kila ifikapo tarehe kumi ya mwezi Machi kila mwaka, kila Wizara itawasilisha kwa Katibu nakala za dondoo za vitabu vya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha unaofuata, pamoja na nakala za randama za Makadirio hayo kulingana na idadi ya Wajumbe wa Kamati, kwa ajili ya kuziwezesha Kamati za Bunge kufanya uchambuzi wa makadirio hayo.

(2) Kwa mujibu wa fasili ya (1), iwapo tarehe kumi ya mwezi Machi itakuwa si siku ya kazi, uwasilishwaji huo utafanywa tarehe inayofuata ya siku ya kazi.

97.(1) Kuwasilisha mapende-kezoya mpangona Bajeti. Tarehe kumi na moja ya mwezi Machi ya kila mwaka au tarehe ya siku nyingine ya kazi inayofuata iwapo tarehe hiyo itakuwa si siku ya kazi, Waziri anayehusika na masuala ya mipango atawasilisha kwa Wabunge, mapendekezo ya Serikali ya mpango kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(2) Kwa mujibu wa fasili (1), siku hiyo pia, Waziri anayehusika na masuala ya fedha, atawasilisha kwa Wabunge mapendekezo ya Serikali ya kiwango na ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(3) Katika hatua ya uwasilishwaji kwa mujibu wa faili ya (1) na ya (2), hakutakuwa na mjadala wowote kuhusu

mapendekezo ya mpango na kiwango cha ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(4) Baada ya mapendekezo ya mpango na kiwango cha ukomo wa Bajeti ya Serikali kuwasilishwa kwa mujibu wa fasili ya (1) na (2), Spika atawasilisha mapendekezo hayo kwenye Kamati ya Bajeti ili yafanyiwe uchambuzi na Kamati hiyo itazishauri Kamati za Bunge za Kisekta pamoja na Serikali kuhusu mapendekezo hayo.

98.(1) Kamati kukagua utekelezaji wa miradi. Baada ya kuwasilishwa kwa mapendekezo ya mpango na kiwango na ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata kwa Wabunge, Kamati za Bunge za Kisekta zitatembelea na kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha, kwa muda wa siku zisizozidi saba.

(2) Baada ya kutembelea miradi, Kamati za Bunge za Kisekta, kwa kipindi kisichozidi siku tisa, zitafanya vikao vyta kuchambua taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozismamia kwa mwaka wa fedha unaoisha, kwa ajili ya kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(3) Siku moja kabla ya kufanya majumuisho kwa mujibu wa fasili ya (4), Kamati ya Uongozi itafanya kikao cha mashauriano na Kamati ya Bajeti kuhusu mambo muhimu yaliyojitokeza kwenye Kamati za Kisekta wakati wa kujadili utekelezaji wa Bajeti za Wizara kwa mwaka wa fedha unaoisha na Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(4) Katika kipindi cha siku tatu kabla ya Mkutano wa Bajeti kuanza, na wakati Kamati za Bunge za Kisekta zikiendelea na shughuli zake, Serikali kwa kushauriana na Kamati ya Bajeti, itafanya majumuisho kuzingatia ushauri wa Kamati za Bunge za Kisekta kuhusu utekelezaji wa Bajeti za Wizara kwa mwaka wa fedha unaoisha, na maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(5) Baada ya Kamati ya Bajeti kushauriana na Serikali kwa mujibu wa fasili (4), Kamati ya Uongozi itafanya kikao na Kamati ya Bajeti kwa ajili ya kupata taarifa ya matokeo ya mashauriano kati ya Kamati hiyo na Serikali.

99.(1) Kujadili utekelezaji wa Wizara. Katika Mkutano wa Bunge wa Bajeti utakaoanza mapema mwezi Aprili kwa kila mwaka, jumla ya siku zisizozidi hamsini na nane zitatengwa kwa ajili ya Bunge kujadili utekelezaji wa Wizara zote wa Bajeti kwa mwaka wa fedha unaoisha, pamoja na Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(2) Mjadala katika Bunge la Bajeti kwa kila mwaka utaanza na Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, na kufuatiwa na Hotuba za Bajeti za Wizara nyingine zote, kwa utaratibu utakaopangwa na Spika, baada ya kushauriana na Kamati ya Uongozi.

(3) Shughuli za Bajeti zitapewa nafasi ya kwanza kabla ya Shughuli nyingine yoyote, na zitawekwa kwanza kwenye Orodha ya Shughuli za kikao kila siku hadi pale zitakapokuwa zimemalizika, isipokuwa kama Bunge litaamua vinginevyo.

(4) Kabla ya taarifa za utekelezaji na Makadirio ya Matumizi ya Wizara kujadiliwa Bungeni, zitachambuliwa na Kamati za Bunge za Kisekta, kwa utaratibu uliowekwa na fasili ya 98(2) ya Kanuni hii, na pia katika Nyongeza ya Nane ya Kanuni hizi.

(5) Asubuhi ya siku ambayo Waziri amepangiwa kuwasilisha hoja ya Makadirio ya Wizara yake, Waziri, Mwenyekiti wa Kamati inayohusika au mijumbe yeyote atakayeteuliwa kwa niaba yake, na Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara husika Wataweka Mezani nakala ya taarifa zao kwa kuzingatia mpangilio wa Shughuli za Bunge.

(6) Pamoja na kuwasilisha mezani nakala ya Hotuba ya hoja ya Makadirio ya Wizara, Waziri atawasilisha pia nakala 10 za randama ya makadirio hayo, siku moja kabla ya siku ambayo Hotuba yake imepangwa Kusomwa Bungeni.

(7) Wakati utakapofika wa kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara inayohusika, hoja itatolewa kwa maneno yafuatayo:-

"Kwamba sasa Bunge likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara yangu."

(8) Isipokuwa kwa Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, muda wa Waziri anayewasilisha Hotuba ya Bajeti utakuwa ni dakika zisizozidi sitini.

(9) Baada ya Waziri kuwasilisha Hotuba ya Bajeti kwa mujibu wa fasili (1), Mwenyekiti wa Kamati iliyopitia Makadirio husika na Msemaji wa Kambi ya Upinzani watatoa maoni yao kwa muda usiozidi dakika thelathini kila mmoja.

(10) Wakati wa kujadili Makadirio ya Matumizi ya Wizara, muda wa Wabunge kuchangia utatolewa kulingana na uwiano wa idadi ya Wabunge kutoka katika kila Chama.

(11) Idadi ya Wabunge watakaopewa nafasi ya kuchangia Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa mujibu wa fasili (10) utaamuliwa na Spika.

(12) Mbunge anayejadili Makadirio ya Matumizi ya Wizara ataruhusiwa kusema kwa muda usiozidi dakika kumi.

Isipokuwa kwamba, Kambi za Vyama zinaweza kupendekeza kwa Spika kugawa muda huo kwa Wabunge wasiozidi wawili, mapema kabla ya mjadala huo kuanza.

(13) Endapo Spika ataona kuwa muda uliotengwa kwa ajili ya kujadili Bajeti ya Wizara inayohusika umekaribia kwisha, atafunga mjadala ili kumpatia Waziri mtoa hoja nafasi ya kujibu ndani ya muda wa dakika sitini.

(14) Bila ya kuathiri masharti ya Kanuni ya 154, maneno yoyote ya utangulizi, utambulisho, salamu za pole, pongezi au shukrani, pamoja na kutaja majina ya Wabunge waliochangia hoja havitaruhusiwa kwa Mbunge au Waziri wakati wa kujadili Hotuba ya Bajeti.

100. Kamati ya Matumizi. Mjadala wa jumla kuhusu Makadirio ya Matumizi kwa Wizara utakapomalizika, Bunge litaingia katika Kamati ya Matumizi ili kuitisha Makadirio ya Wizara husika kifungu kwa kifungu.

101. (1) Mjadala katika Kamati ya Matumizi. Katika Kamati ya Matumizi, Mwenyekiti atawahoji wajumbe kuhusu kifungu kimoja kimoja cha Makadirio ya Matumizi, na kila kifungu kitaafikiwa peke yake.

(2) Mbunge ye yeyote anaweza kuomba ufanuzi au maelezo zaidi katika kifungu chochote cha Fungu linalohusika, wakati kifungu hicho kitakapofikiwa na Kamati ya Matumizi.

(3) Mbunge atakaye amua kutumia kifungu chenye mshahara wa Waziri, ataruhusiwa tu iwapo ataomba ufanuzi wa suala mahsusil la sera na hatazungumzia zaidi ya jambo moja.

(4) Kwa kuzingatia masharti ya fasili ya (3), Kamati za Vyama zitawasilisha kwa Spika majina ya Wabunge watakaoomba kupata ufanuzi wa suala mahsusil la sera, na Spika atatoa nafasi kwa Wabunge kwa kuzingatia uwiano.

(5) Muda wa kusema katika Kamati ya Matumizi kwa ajili ya kuomba au kutoa ufanuzi hautazidi dakika tano.

102. (1) Kubadilisha Makadiriotika Kamati ya Matumizi. Katika Kamati ya Matumizi, Mbunge ye yeyote anaweza kutoa hoja ya kutaka kufanya mabadiliko katika Makadirio ya Matumizi ya Serikali iwapo mabadiliko hayo hayatabadili madhumuni ya Fungu.

(2) Endapo hoja iliyotolewa kwa ajili ya kupunguza kifungu fulani katika Fungu lolote haijapitishwa, hoja nyingine bado inaweza kutolewa kwa madhumuni ya kupunguza kifungu kingine cha Fungu hilo hilo.

(2) Endapo hoja iliyotolewa kwa ajili ya kupunguza kifungu fulani katika Fungu lolote haijapitishwa, hoja nyingine bado inaweza kutolewa kwa madhumuni ya kupunguza kifungu kingine cha Fungu hilo hilo.

103.(1) Hoja ya kuondoa shilingikwenyeMakadirio. Kwa kuzingatia utaratibu wa majadiliano uliowekwa na Kanuni hizi, Mbunge ye yeyote anaweza kuomba ufanuzi au maelezo zaidi katika kifungu chochote cha Fungu linalohusika, wakati kifungu hicho kitakapofikiwa na Kamati ya Matumizi.

(2) Vilevile Mbunge ye yeyote anaweza kutoa hoja ya kuondoa shilingi moja katika kifungu chochote cha Fungu hilo.

(3) Madhumuni ya hoja ya aina hiyo ni kumwezesha Mbunge allyeitoa aweze kueleza kutoridhika kwake na utekelezaji wa jambo fulani mahsus ambalo dhahiri linahusika na kifungu hicho.

(4) Hoja ya aina hiyo itatolewa kwa muda usiozidi dakika tano.

(5) Wabunge wanaweza kuchangia hoja ya kuondoa shilingi moja iliyoanzishwa kwa mujibu wa fasili ya (2) kwa muda usiozidi dakika tatu kila mmoja.(6) Waziri anayehusika atapewa nafasi ya kutoa majibu ya hoja hiyo.

(7) Mbunge aliyetoa hoja ya kuondoa shilingi ndiye atakayefunga mjadala wa hoja hiyo(8) Muda utakotumiwa na Waziri na Mbunge kwa mujibu wa fasili ya (6) na (7) utaamuliwa na Spika.

(9) Endapo Mbunge atashikilia hoja yake ya kuondoa shilingi moja katika kifungu hicho, basi kura itapigwa kwa kuhoji wanaoafiki na wasioafiki hoja hiyo.

(10) Endapo hoja ya kuondoa shilingi moja katika kifungu chochote itakubalika, basi kifungu hicho kitakuwa kimepitishwa kikiwa pungufu ya hiyo shilingi moja.

(11) Endapo hoja iliyotolewa kwa ajili ya kuondoa shilingi moja 1atika kifungu chochote cha Fungu linalohusika imekataliwa, hoja nyingine yenye madhumuni ya kuondoa shilingi moja katika kifungu kingine cha Fungu hilo hilo bado inaweza kutolewa.

104.(1) Kukamilikamjadala katika Kamati ya Matumizi. Iwapo zimesalia dakika kumi kabla ya kufikia muda wa kuahirisha kikao cha Bunge na Kamati ya Matumizi bado haijamaliza kuitisha mafungu, Mwenyekiti anaweza kuongeza muda usiozidi dakika thelathini bila kuihoji Kamati ili kukamilisha Shughuli ya kuitisha mafungu yaliyobaki.

(2) Iwapo zimesalia dakika kumi kabla ya kumalizika muda ulioongezwa chini ya fasili ya (1) na Kamati bado haijamaliza kuitisha mafungu yote, Mwenyekiti atafunga mazungumzo yanayoendelea na papo hapo atawahoji Wajumbe kuhusu mafungu yaliyosalia, kama yapo.

(3) Baada ya Kamati ya Matumizi kumaliza kazi ya kuitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara na Bunge kurudia, waziri mtoa hoja atatoa taarifa kwamba:-

(a) "*Mheshimiwa Spika, Bunge lako likikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake*"; na kuomba kwamba:

(b) "*Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge*"; na atahitimisha kwa kusema: "*Naomba kutoa hoja*".

(4) Spika atawahoji Wabunge kwa kuuliza, "*Wanaofiki waseme Ndiyo*", na "*Wasioafiki waseme Siyo*".

105.(1) Hotuba ya Bajeti ya Serikali Kusomwa Bungeni. Baada ya Bunge kukamilisha mjadala wa Makadirio ya Wizara zote, ndani ya siku sita kabla ya Hotuba ya Bajeti Kusomwa Bungeni, Serikali kwa kushauriana na Kamati ya Bajeti itafanya majumuisho kwa ajili ya kuzingatia hoja zilizojitokeza wakati wa kujadili utekelezaji wa Bajeti za Wizara kwa mwaka wa fedha unaoisha, na Makadirio ya Matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(2) Katika kipindi cha kufanya majumuisho kwa mujibu wa fasili ya (1), Bunge litaendelea na shughuli zake nyingine kama zitakavyokuwa zimepangwa na Spika baada ya kushauriana na Kamati ya Uongozi.

(3) Wakati Serikali ikifanya majumuisho kwa mujibu wa fasili ya (1), wajumbe wa Kamati ya Uongozi kwa nafasi zao, watakuwa wajumbe wa Kamati ya Bajeti.

(4) Makadirio ya Fedha za Matumizi ya Serikali yatawasilishwa Bungeni na Waziri anayehusika na masuala ya fedha kwa Hotuba kuhusu Makadirio hayo itakayoitwa "Hotuba ya Bajeti ya Serikali" ambayo itasomwa Bungeni kabla ya tarehe ishirini ya mwezi Juni kila mwaka.

(5) Muda wa kusoma Hotuba ya Bajeti ya Serikali utaamuliwa na Spika kadri atakavyoona inafaa.

(6) Hoja ya kuwasilisha Makadirio hayo itakua katika maneno yafuatayo:-

(5) "*Kwamba Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa*"

(7) Siku ya kuwasilisha Bungeni Hotuba ya Bajeti ya Serikali, nafasi pia itatolewa kwanza kwa Waziri anayehusika na mipango au uchumi kutoa maelezo kuhusu hali ya uchumi kwa ujumla.

(8) Hotuba ya Bajeti ya Serikali na ya Waziri anayehusika na mipango, zitafuatiwa na hotuba za Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge inayohusika na masuala ya Bajeti, na Msemaji wa Kambi ya Upinzani.

(9) Muda wa kusoma maoni ya Kamati na ya Kambi ya Upinzani, utakuwa dakika zisizozidi thelathini kwa kila hotuba.

106. (1) Mjadala kuhusu Hotuba ya Bajeti. Mjadala kuhusu Hotuba ya Bajeti ya Serikali utaendelea kwa siku zisizozidi saba, ambapo dakika zisizozidi kumi zitatolewa kwa kila Mbunge anayetaka kuchangia Hotuba hiyo.

(2) Katika hatua hii, majadiliano yatahusu mambo ya jumla kuhusiana na hali ya uchumi, na Mbunge yejote hararuhusiwa kupendekeza mabadiliko katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali.

107. (1) Utaratibuwa kuidhinisha Bajeti ya Serikali. Mjadala kuhusu Hotuba ya Bajeti ya Serikali utakapomalizika, Spika atalihoji Bunge litoe Uamuzi wake wa kupidisha au kutokupitisha Bajeti ya Serikali ili kukidhi matakwa ya Ibara ya 90(2)(b) ya Katiba.

(2) Uamuzi wa Bunge wa kupidisha au kutokupitisha Bajeti ya Serikali utafanywa kwa kupiga kura ya wazi kwa kuita jina la Mbunge mmoja mmoja.

108. (1) Muswada wa Fedhaza Matumizi. Kabla ya tarehe 30 ya mwezi Juni kwa kila mwaka, baada ya Bunge kukamilisha kazi ya kujadili na kupidisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka unaohusika, Muswada wa Sheria ya Fedha za Matumizi utawasilishwa Bungeni na kupidishwa mfululizo katika hatua zake zote.

(2) Kwa madhumuni ya Kanuni hii, "*Muswada wa Fedha za Matumizi*" maana yake ni Muswada wa Sheria ya Fedha za Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(3) Muswada wa Fedha za Matumizi hautapelekwa kwenye Kamati yoyote ya Kudumu wala Kamati ya Bunge Zima, na masharti kuhusu Miswada Kusomwa Mara ya Kwanza hayatatumika.

10 APRILI, 2013

(4) Muswada wa Fedha za Matumizi hautatangazwa kwenye *Gazeti* kabla haujawasilishwa Bungeni.

109. (1) Muswadawa Sheria ya Fedha. Baada ya Bunge kukamilisha kazi ya kuitisha Muswada wa Fedha za Matumizi, Muswada wa Sheria ya Fedha utajadiliwa na kuitishwa kwa kuzingatia mashati yaliyowekwa na Sehemu ya Nane ya Kanuni hizi.

(2) Marekebisho au mabadiliko ya kupunguza kiwango cha kodi katika lbara yoyote ya Muswada wa Sheria ya Fedha yatakayopendekezwa na Mbunge ye yoyote hayatakubaliwa iwapo hayatatoa mapendekezo mbadala yanayaziba pengo linalotokana na punguzo linalopendekezwa.

110. Makadirio ya Matumizi ya Nyongeza. Mapendekezo yoyote kwa ajili ya Matumizi ya Nyongeza ya Fedha za Serikali au kwa ajili ya kutoa fedha yoyote ya nyongeza zaidi ya Fedha za Matumizi ya Mwaka huo:-

- (a) Yataitwa Makadirio ya Nyongeza ya Matumizi;
- (b) Yatapelekwa kwenye Kamati ya Matumizi kufuatana na masharti ya lbara ya 99 ya Katiba; na
- (c) yatafuata masharti ya Kanuni zote zinazohusu Makadirio ya Mwaka ya Matumizi ya Serikali."

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Spika naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Hoja hiyo imeungwa mkono, sasa naomba muiamue, Mheshimiwa Anna Abdallah.

MHE. ANNA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kwanza ya kuchangia hoja hii. Mabadiliko yaliyowekwa mbele ya Bunge hili Tukufu, yana lengo la kubadilisha kama alivyowasilisha mtoa hoja, mabadiliko katika Ibara ya Tisa, Sehemu ya Tisa ya Kanuni zetu za Bunge. Ni mambo yanayohusu kutunga sheria kuhusu mambo ya fedha. Utaratibu mpya unaopendekezwa, unalipa Bunge uwezo wake wa Kikatiba wa kusimamia na kuishauri Serikali hasa katika mambo ya fedha.

Mabadiliko haya yanatoa nafasi kubwa kwa Bunge letu, kushauriana na Serikali katika hatua mbalimbali za mpango mzima wa bajeti na mambo yanayohusiana na fedha. Kwa kupitia Kamati ya Bajeti ya Bunge letu Tukufu, tunaweza sasa kushauriana kwa kina na SERIKALI kuhusu mapendelekezo yanayoletwa hapa Bungeni hasa katika kipindi hiki cha bajeti. Kama tulivyokwisha kuanza, Kamati mbalimbali zimepitia randama mbalimbali za Wizara zilizo chini ya Kamati hizo na maoni tayari yamepelekwa kwenye Kamati hiyo na kwamba Kamati sasa itazungumza na Serikali kuhusu maoni ya Bunge, kabla hatujapitisha bajeti, kama ilivyokwisha kuelezw. Huko nyuma, ilikuwa ni jambo tulilokuwa tunalifanya kwa mazoea, lakini kwa kweli ilikuwa haitoi nafasi kwa Bunge kutoa maoni yake kabla Bajeti hajapitishwa.

Katika utaratibu huu mpya ambao unapendekezwa, wa utaratibu mzima wa Bajeti, licha ya kwamba tutamaliza kabla ya mwaka wa fedha kuanza, lakini Bunge litakuwa na uwezo pia wa kushauriana na Serikali, kuhakikisha kwamba, yale mambo ya vipaumbele ambayo yameonekana kwenye Kamati mbalimbali; kwa kupitia Kamati ya Bajeti yatafikishwa ndani ya Serikali na Serikali nayo itapata nafasi ya kutoa maoni yake, kabla ya mwisho wa mchakato mzima wa Bajeti.

Hili ni jambo muhimu sana katika kutoa nafasi ya Bunge katika wajibu wa kusimamia Serikali. Kwa kweli, tulichokuwa tunafanya, tulikuwa tunapitisha bajeti halafu tunakaa mwezi mzima sijui na zaidi hivi tunazungumza bajeti

za Wizara mbalimbali, wakati bajeti tulikwishakuikubali; kidogo ilikuwa inatunyima meno, sisi Bunge kuiambia Serikali kwamba tunataka jambo hili liwekwe mkazo hapa na pale. Tulikuwa tunazungumza kwa maneno, sasa si tu tutazungumza kwa maneno, lakini tunaweza tukaiambia Serikali punguza fedha katika fungu hili peleka katika fungu hili; uwezo huo tunapewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwaombe Wabunge wenzangu na Wabunge wote, tuyaunge mkono mapendekezo haya; na kwa kuwa tumeyazungumza kwa muda katika vikao vyote nya mashauriano, ni vyema na furaha tu kwamba, mambo yote yaliyokubaliwa na Wabunge yameingizwa katika Kanuni. Kwa hiyo, nawasihi Wabunge wenzangu, tushirikiane, tukubaliane tuyapitisha mapendekezo haya ili yaweze kufanya kazi. Naomba pia nisilizite kwamba, Kanuni zetu zinahitaji mabadiliko mengi ya msingi, lakini leo tumeshughulikia tu haya yanayohusu Sheria ya Kutunga Kanuni ya Mambo ya Fedha.

Kwa hiyo, nawaomba sana, katika kumalizia Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tusaidiane kuyapitisha mabadiliko haya ili yaweze kufanya kazi. Tuutumie muda tuliopewa kutokea sasa tunapoanza kujadili Bajeti za Wizara mbalimbali mpaka kufikia bajeti yenyewe, katika kupitisha fedha ambazo tutaidhinisha ili zitumike katika mwaka wa fedha ujao. Siyo hilo tu, tumekuwa tukilalamika hapa na sisi tukishughulikia tu suala la matumizi ya bajeti, lakini nafikiri nafasi tuliyopewa hivi sasa katika mchakato wote wa mabadiliko haya, tunayo pia nafasi ya kuiambia Serikali, maeneo ambayo tunadhani haikusanyi kodi.

Kamati ya Bajeti itaiambia Serikali maeneo haya hamkusanyi kodi tunataka mkusanye. Hili ni jambo zuri sana. Wakati tunazungumza tu huku mwisho, wakati Bajeti tumeipitisha. Kwa hiyo, nawaombeni Waheshimiwa Wabunge, tukubaliane na mabadiliko haya ili shughuli hii kubwa ya kuisimamia na kuishauri Serikali, kweli iwe ndiyo jukumu kubwa tulilopewa Bunge kwa niaba ya Wananchi wa Tanzania.

Kwa maneno hayo machache, napenda kukushukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Spika, naomba na mimi nichangie hoja iliyoko Mezani na nianze kwa kusisitiza alichokisema Mheshimiwa Naibu Spika kwamba, marekebisho ya Kanuni ambayo yameletwa leo, yanahuusu tu Sehemu ya Tisa ya Kanuni zetu za Kudumu, inayohusu utaratibu wa kutunga Sheria kuhusu mambo ya fedha. Kwa hiyo, marekebisho pekee ambayo Bunge hili linaombwa kuyaridhia leo ni hayo yanayohusu utaratibu wa kutunga Sheria za Masuala ya Fedha peke yake, Masuala ya Bajeti *and so on.*

Mheshimiwa Spika, marekebisho haya hayahuusu, na yasije yakawa yamechukuliwa kwamba yamehusu marekebisho mengine yaliyokuwa yamependekezwa, lakini baadaye yakaondolewa kwenye Kamati ya Kanuni kuhusiana na masuala mengine yasiyokuwa kwenye Sehemu ya Tisa ya Kanuni za Bunge. Hii maana yake ni kwamba, hakuna marekebisho yoyote kuhusiana na utaratibu wa kuchagua Viongozi wa Kamati. Bunge halijapitisha mapendekezo hayo, kwa sababu hayako kwenye Sehemu ya Tisa. (*Makofi*)

Masuala yanayohusu *composition* za Kamati, uongozi wake utakuwaje, yapo kwenye sehemu ya kumi ambayo haipo kwenye mjadala huu. (*Makofi*)

Tusije tukaambiwa, aaah mlipitisha; hilo ni jambo ambalo linahitaji kuwekwa wazi sana.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kwamba, kwa vile tunajadili masuala yanayohusu Sehemu ya Tisa ya Kanuni hizi, ni muhimu hii inayoitwa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, ikajulikana kwamba hajapitishwa na Bunge hili. Yaliyoko humu hayajapitishwa na Bunge hili na kwa sababu hiyo itakuwa vizuri wala Waheshimiwa Wabunge wasipewe nakala za hii, wapewe nakala ya Kanuni baada ya Azimio la

Bunge hili, kwa sababu yaliyoko humu, yako tofauti kabisa na Azimio ambalo liko mbele ya Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maangalizo hayo mawili, naomba sasa nichangie kwenye vipengele mahususi vilivyoko katika mapendekezo haya yaliyoko mbele ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, imeelezwa na Mheshimiwa Naibu Spika, Mtoa Hoja, kwamba, moja ya faida za mapendekezo haya itakuwa ni kuongeza tija katika mijadala inayohusu bajeti, kwa sababu zamani tulikuwa tunaletewa Bajeti Kuu tunaipitisha halafu kinachofuata kinakuwa ni kufanya mchezo wa kuigiza. Tunaambiwa kwamba, mapendekezo haya yatatuwezesha Bunge hili kuweza kufanya mabadiliko katika Bajeti pale Bunge litakapoona kwa busara zake kwamba inafaa, na hilo ni jambo jema.

Isipokuwa kama nia ndiyo hiyo, basi naomba hili pendelekezo kwamba, mapendekezo ya Kanuni ya 96(2), (3) na (4), yanayoweka ukomo wa Bajeti, yanayompa Waziri mamlaka ya kuweka ukomo wa Bajeti, yaangaliwe upya. Maana yake ni kwamba, kama tukiwekewa ukomo wa Bajeti itakuwaje; tutakuwa tuko palepale tulipokuwa kabla ya mapendekezo haya, hatutaweza kujadili kuongeza nje ya ukomo wa Bajeti uliowekwa na hiyo maana yake tutarudi palepale. Kwa hiyo, napendekeza Waheshimiwa Wabunge, hivyo vifungu vitatu vya Kanuni ya 96 viangaliwe upya. Vifungu vingine vya kuangaliwa upya ni vifungu vya 97(1) na (2), ambavyo vilevile vinazungumzia ukomo wa Bajeti.

Ijulikane kwamba, Bunge hili liwe na mamlaka ya kuitisha Bajeti, ya kubadili mapendekezo ya Serikali na kubadilisha ukomo vilevile kama Bunge litaona kwa busara zake inahitajika kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naomba nizungumzie masuala ambayo yametutatiza sana; masuala yanayohusu uwiano ndani ya Bunge katika mijadala na muda wa kujadili.

Mheshimiwa Spika, hili ni Bunge la Vyama Vingi, na kwa sababu ni la Vyama Vingi, lazima kuwe na *compromises; you win some you lose some*. Mapendekezo ambayo yameletwa leo kwenye Bunge hili Tukufu, yana-reflect huo ulazima wa *compromises*. Hakuna anayeweza kupata kila kitu, hakuna anayeweza kukosa kila kitu. Wote tumechaguliwa na Wananchi hapa, endapo tutakosa kila kitu hapatakalika. Vilevile, kuna haja ya kukubali kwamba, hatuwezi tukapata kila kitu tunachokitaka na vilevile hatuwezi tukakosa kila kitu.

Haya mapendekezo kwamba, kuwe na uwiano katika mijadala ni *compromise* hiyo ninayoizungumza, kwa sababu ni Bunge la Vyama Vingi. Wape walio wengi nafasi ya kutawala, wape walio wachache nafasi ya kusema. *Give the majority a sway, give the minority a say*. Kwa maoni yangu hii ndiyo *spirit* ya hii *compromise* tunayoljadili hapa leo. Inawapa walio wengi nafasi ya kufanya maamuzi ya kutawala, kwa sababu ndiyo wengi, inatupa wachache nafasi ya kusema; na kwa sababu hiyo, kwa kuwa inatupa nafasi ya kusema, kuna haja kwa maoni yangu ya kuiunga mkono.

Jambo la pili, kuhusu muda wa kuzungumza, tumevutana sana juu ya suala la kuwa na dakika 15 au kuwa na dakika 10, na mimi siku zote nimeshikilia msimamo kwamba, Bunge ni mahali pa kuzungumza, tusije tukapunguza muda wa Bunge kuzungumza, kwa sababu ukipunguza muda wa Bunge kuzungumza, unalifanya Bunge kuwa mhuri wa kugonga maamuzi yanayofanyika mahali pengine. Hii haitakuwa sawasawa kwa nchi kama ya kwetu, inayotaka kujenga Bunge lenye uwezo wa kutimiza wajibu wake wa kuisimamia Serikali kwa mujibu wa Katiba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tuna Wabunge zaidi ya 350 huku, kama ukitaka kila mwenzetu aliyeko humu ndani apate fursa ya kuzungumza, maana yake ni kwamba, hili Bunge basi tulibadilishe, badala ya kuwa Bunge la muda, *a part time Parliament paid full time salary, liwe a full time Parliament paid a full time salary*.

Sasa kwa utaratibu wa Kikatiba tulionao leo, *we are a part time parliament even though we are paid a full time salary*, na kwa sababu *we are a part time parliament*, lazima huu muda tulionao tujue namna ya kuugawana. Vilevile, kama nilivyo sema ni suala la *compromises, you win some, you lose some, you don't win everything and others don't lose everything*.

Kwa hiyo, pendekezo la kubadili muda wa mjadala kutoka dakika 15 hadi dakika 10, pamoja na kwamba inapunguza muda wa Wabunge kujadili, angalau litawezesha Wabunge wengi kupata fursa ya kujadili. Kwa sababu ya hiyo haja ya kuwa na *compromises*, kwa maoni yangu hili pendekezo linahitaji kuungwa mkono. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba nisisitize hapa kwamba, ule muda wa Waheshimiwa Wabunge kuomba ufanuzi kwenye masuala ya Kisera, umebakipale pale kama ulivyo dakika tano, muda wa kushika mshahara wa Waziri umebakipalepale dakika tano, muda wa kufunga mjadala kwa mtoa hoja aliyeshika mshahara wa Waziri umebakipale kama ulivyo kwa mujibu wa Kanuni za sasa. Kwa maoni yangu, kinachotakiwa ni kwamba Waheshimiwa Wabunge lazima tujifunze namna ya kufanya kazi zetu humu ndani kwa kuzingatia haya mabadiliko.

Hakuna mlango ambao umefungwa moja kwa moja, hakuna haki ambayo imenyakuliwa moja kwa moja, *we have lost some, we have gained some*, lakini ili tufanye kazi kwa ufanisi, inabidi tufahamu haya matakwa mapya ya hizi Kanuni tunazopitisha leo. Tunahitaji kujifunza kufanya kazi katika mazingira tuliyonayo.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, hili nalielekeza kwako moja kwa moja; Kiti chako kina nguvu sana na baadhi yetu tunadhani kwamba mamlaka yako ni makubwa. Pendekezo ninalotaka kukupa ni kwamba, kuna maeneo mengi ambayo Bunge linaweza likaokoa muda kama Kiti chako kitatumia Kanuni hizi kama zilivyo.

Tumegombana sana juu ya suala la pongezi, pole na nini, lakini kwa maoni yangu, wala halikuwa na haja ya kuja kwenye Kamati ya Kanuni leo, kwa sababu Kanuni kama zilivyo, Kanuni ya 152 nafikiri, inaweka utaratibu wa miaka yote.

SPIKA: Kanuni ya 151.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Kanuni ya 151, utaratibu wa salamu za pongezi na pole. Mamlaka hayo miaka yote yamekuwa kwenye Kiti cha Spika, lakini hayatumiki, kwa hiyo, watu wanapoteza humu siyo kwa sababu nydingine, ni kwa sababu Spika aidha unaogopa au unasita ama unaruhusu kifungu cha mia moja hamsini na ngapi kinachohusu salamu za pongezi kuvunjwa. Naomba Kiti chako, baada ya yote haya, kisaidie kuokoa muda wa Bunge hili, tuzungumze mambo ya maana.

Kama Kanuni inasema Spika atatoa pole kwa niaba ya Wabunge, basi na iwe hivyo, kama Kanuni inasema kwamba Waziri Mkuu atatoa pole kwa niaba ya Serikali, basi iwe hivyo. Utaratibu ukifuatwa, Bunge hili litapata muda. Katika mazingira haya ya watu wengi na muda kidogo, Bunge litapata muda wa kufanya kazi yake sawasawa.

Mheshimiwa Spika, baada ya yote hayo, naomba niunge mkono hoja hii kwa hayo ambayo nimeyasema. Nashukuru sana. (*Makofii*)

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Namshukuru vilevile, Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati ya Kanuni ambapo na mimi ni mmoja kati ya Wajumbe, kwa kuwasilisha mabadiliko haya muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, Wabunge ni mashahidi kwamba, kitendo kinachofanyika leo ni mabadiliko makubwa sana katika uhai wa nchi yetu. Miaka yote Bunge lako la Jamhuri ya Muugano wa Tanzania, lilikuwa linapitisha Bajeti na halafu mjadala unaendelea. Kwa maana hiyo, Bunge linaonekana

kama ni *rubber stamp* tu, hakuna lolote linalobadilika. Wakati mwingine tumeshuhudia hata katika Bunge lilitlopita, Wabunge walikuwa wanatoa mawazo ya kubadilisha baadhi ya mambo nje ya utaratibu, lakini ilibidi Serikali ikubali kwa sababu ndiyo hali halisi.

Sasa tumerudi katika uhalisia, ningeomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tukubali mabadiliko haya, ni muhimu sana na tukupongeze Mheshimiwa Spika na Serikali kwa kukubali mabadiliko haya makubwa. Hili ni badiliko kubwa sana na linahitaji Bunge hili kupongezwa kwa kazi hii nzuri tunayoifanya.

Kwanza, tunabadilisha Sehemu ya Tisa ya Kanuni zetu, ambayo inazungumzia suala zima la utaratibu wa matumizi ya fedha, mapato na matumizi. Huko nyuma ilikuwa Waziri wa fedha anasoma Bajeti tunapitisha halafu tunaanza mjadala. Leo kwa mara ya kwanza kabisa, Watanzania watashuhudia Bunge lao likipata fursa ya kuwasikiliza Mawaziri wote.

Kamati za Bunge zitapata fursa ya kuchambua na kuititia mapendekezo ya Serikali na hivyo kutekeleza kikamilifu matakwa ya Kikatiba ya Bunge kuishauri Serikali na kuisimamia Serikali. Kwa maana hiyo, mchakato mzima sasa wa Bajeti utapata fursa ya Wabunge kutoa michango na michango yao iweze kusikilizwa.

Huko nyuma tulikuwa tunasema hatuna uhakika kwamba, michango yetu itaweza kusikilizwa, sasa tumepeata fursa hiyo, ningeomba Waheshimiwa Wabunge, tuitumie vizuri. Tunaitumia wapi fursa hii, katika mabadiliko haya utakuta kwamba, ukiacha mwaka huu ambao tumechelewa kidogo, lakini kwa mwaka ujao, Kamati za Kisekta zitapata fursa ya kuititia mapendekezo ya Serikali na hatimaye Kamati ya Bajeti itapata fursa ya kukaa na Wenyeviti wa Kamati za Bunge ili kuona katika Sekta mbalimbali yale waliyoyapitia kama kweli wameridhika nayo au hawakuridhika nayo. Hiyo ni hatua muhimu sana.

Kwa hiyo, sasa Kamati za Bunge zitakuwa zimeshirikishwa kikamilifu na mpango mzima wa Serikali, lakini kubwa zaidi ambalo linatokea ni katika Mpango wenye.

Kwa kawaida, Mipango inaletwa na Serikali tunaijadili lakini hatuna nafasi kubwa sana. Katika kipindi cha Oktoba, tuna nafasi ya kukaa na Serikali juu ya Mpango mzima wa Serikali. Kwa hiyo, suala la vipaumbele ambavyo tulikuwa tukivilalamikia ndani ya Bunge hili, sasa tumepata fursa ya kupanga pamoja na Serikali. Kwa hiyo, hatuna nafasi tena ya kuweza kulaumu wakati tumeshirikishwa kikamilifu. Hiyo ni fursa muhimu na ningeomba tuitumie.

Mheshimiwa Spika, nilitaka niseme hili kwa sababu *experience* imeonesha katika Mabunge hasa kama Bunge la Dunia kwenye Kamati zile, ndiko ambako kazi kubwa sana inafanyika, mnapokuja kwenye *Full House* kwa kweli ni kufanya *endorsement* tu na hili ndilo jambo muhimu sana. Humu ndani tumekuwa tunachukua muda mwingi sana tunazungumza, lakini matokeo yake hatupati fursa ya kupata maamuzi ya lile tunalolikubali. Ombi langu kwa Wajumbe wa Kamati za Bunge ni kuitumia nafasi hii vizuri kwenye Kamati.

Tubanane na Serikali kwenye Kamati, tukitoka kwenye Kamati zetu tunaingia kwenye Kamati ya Bajeti, tukitoka hapo tutakuwa tumetoka na jambo moja, hata misuguano na mivutano itakuwa imepungua kwa kiwango kikubwa na yale ambayo tunayataka yatakuwa yamefanikiwa. Kwa hiyo, naomba tuitumie fursa hiyo. Mara hii tumechelewa kidogo, lakini kipindi kinachokuja tutaipata fursa hiyo vizuri, naomba tuitumie.

Mheshimiwa Spika, la pili ni kuhusu muda. Nimejifunza sana kwamba, bado *management of time* ni tatizo kwetu katika mazingira yoyote tuliyonayo, iwe ndani ya Bunge, nje ya Bunge, *time management* bado ni tatizo. Muda usipou-*manage*, utaku-*manage* wewe. Katika Mabunge mengine muda wa kuzungumza pengine ni dakika nane, mtu anayechangia ni dakika tatu.

Ukienda *Inter-Parliamentary Union* ndiyo utaratibu, *main speaker* dakika nane, mchangaji mwingine dakika tatu, una hoja umemaliza unaondoka. Bado sisi tunachukua muda mrefu sana kuzungumzia jambo hilohilo moja, wakati mwingine unakwenda nje ya ajenda. Watu wanao-*manage time* vizuri hawana muda huo. (*Makof*)

We need to manage time. Dakika kumi siyo ndogo hata kidogo, kama unajipanga vizuri unachotaka kukisema kinaeleweka, dakika kumi ni nydingi sana na ndiyo maana katika *International Forums* dakika unazopewa ni nane, tisa, *hardly* kumi, lakini kwenye mjadala watu wengine ni dakika tatu tu. Kwa hiyo, nilifikiri hili Wabunge tulikubali, tulisimamie vizuri na sasa tujielekeze kufanya kazi hii vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba tujitahidi sana kuliwezesha Bunge liwe na Wataalam watakaowasaidia Wabunge ili Mbunge atakapokuja kwenye Bunge, awe amehodhi, ameshiba *data* za kutosha kujenga hoja yake. Pengine nalo hilo limechangia watu kupoteza muda. Tukiweza kulifanya vizuri kwenye Tume yetu, tukiweza kulifanya vizuri, Serikali hatimaye ikaliwezesha Bunge kuwa na Mfuko wake kikamilifu, nafikiri sasa tunaweza tukalijengea uwezo ili Wabunge wanapofika ndani ya Bunge wazungumze kwa hoja, kwa sababu wamepata *data* za kutosha. Mimi nafikiri hilo tulifanyie kazi, tunaweza tukautumia muda huu vizuri na ninafikiri ni *opportunity* nzuri sana ya kuitumia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo limezungumzwa ni la ukomo wa Bajeti. Bado Katiba yetu inampa Rais madaraka ya kupandisha na kupunguza kodi, hajjalipa Bunge, labda Katiba mpya itakayotokea. Kwa hiyo, tutakwenda katika misingi hiyo ya Kikatiba, hatuwezi tukavunja Katiba. Kanuni haiwezi kuvunja Katiba, wala Sheria haiwezi kuvunja Katiba. (*Makof*)

Tutakwenda katika utaratibu huu wa Kikatiba, lakini jambo moja ambalo tumepata fursa hivi sasa ni kwamba, bado tuna nafasi ya kuishauri Serikali ndani ya mfumo wa kutumia Kamati yetu ya Bajeti, kuiambia Serikali hapa nafikiri

mapato yenu siyo mazuri. Mfano mzuri umetokea, Mheshimiwa Spika ameunda Kamati Ndogo huko nyuma ya kupendekeza utaratibu mzuri wa kuweza kupata mapato ya Serikali.

Kamati hiyo imefanya kazi nzuri, imeweza kuonesha maeneo mbalimbali imefikia mpaka *3.5 trillion* na kuonesha kwamba kuna maeneo mengine ambayo Serikali inaweza kupata mapato. Serikali imeitumia Ripoti hii na kwa taarifa ya Waziri wa Fedha alituambia si chini ya *650 billion* wameweza kuziona ndani ya kipindi kifupi tu na kwamba, kwa mapendekezo yale ya Kamati wanaweza kupata mapato. Nasema huo ni mwanzo mzuri, tukiitumia fursa hii vizuri, tukaishauri Serikali vizuri, ikakubaliana na vipaumbele ambavyo Wananchi wanavitaja; kwa mfano, shida ya maji iliyoko Tanzania leo, shida ya reli na kadhalika, nafikiri Serikali itaweza kuona kwamba, kuna mapato yanapatikana na Wabunge wameshauri vizuri na kwa hiyo, tutaondoka kama watu wa aina moja. Hii itatusaidia jambo moja kubwa sana, kujenga Utaifa wetu.

Itatusaidia sana katika kujenga Utaifa wetu, *differences* zinazotokea hizi za hovyo hovyo, zitakuwa zimepungua sana, kwa sababu kila mmoja atashirikishwa. Kwa maana hiyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, wala tusipoteze muda, tuyakubali mapendekezo haya na kama alivyosema Mheshimiwa Tundu Lissu, haya hayahusiani na mabadiliko ya Kanuni nyingine ambayo yataletwa baadaye. Sasa hivi tunashughulikia jambo moja tu la kupitisha utaratibu mzima wa Bajeti Kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, naomba kuunga mkono hoja na naomba Waheshimiwa Wabunge wakubaliane na hoja hii. Ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hili Azimio ni *in house*, yaani tunatengeneza mikakati ya namna ya kuendesha shughuli zetu sisi. Kwa hiyo, hayo yanayosemwa ni elimu kwa Wananchi kwamba tuna kitu cha namna hiyo. Kwa hiyo, namwita Mheshimiwa Naibu Spika.

MHE. JOB Y. NDUGAI - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KANUNI ZA BUNGE NA NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Spika, naomba kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii niweze kuhitimisha hoja niliyoleta mbele ya Bunge lako Tukufu.

Nianze kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, ambao wamechangia hoja yangu. Nipende kusema kwamba, madhumuni makubwa ya pendekezo hili ni kutoa fursa kwa Bunge, Bunge na Serikali, ili kufanya kazi nzuri zaidi kwenye suala zima la *budget circle*, kuhakikisha kwamba utaratibu umekaa vizuri tuweze kuitendea vyema Bajeti yetu ya Serikali, kuhakikisha kwamba baadhi ya malalamiko yaliyokuwepo siku za nyuma tumeyapunguza kwa kiasi kikubwa kadiri iwezekanavyo.

Katika wachangiaji kwa njia ya maandishi, nimepata maswali kuhusu Nyongeza ya Nane ya Mabadiliko ambayo yalikuwemo kwenye baadhi ya rasimu. Niseme tu kwamba, mimi nilichoagizwa na Kamati ya Kanuni ambayo wewe Mheshimiwa Spika ni Mwenyekiti, kuwasilisha hapa ni mabadiliko ya Sehemu ya Tisa tu basi na siyo mabadiliko mengine yoyote kama Wajumbe wenzangu walivyosaidia kufafanua kwamba kilichotuleta hapa ni hicho.

Waheshimiwa Wabunge, nikumbushe kilichomo na kinachozungumzwa hapa; katika mabadiliko ambayo tumepependekeza na ambayo tunaomba myakubali, tumejitahidi sana kujaribu kuainisha na kupunguza malalamiko kuhusiana na usawa wa uchangiaji ndani ya Bunge na namna ya kupata nafasi za kuchangia kuhakikisha kwamba, kuna suala la uwiano mzuri zaidi. Kwa hiyo, hilo limo katika Kanuni zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia tumesitisiza suala la uchangiaji kuwa ni dakika kumi kwa kipindi hiki tu cha Bajeti, kwa vipindi vingine vya Bunge zitaendelea dakika kumi na tano mpaka mtakapoelekezwa vinginevyo, lakini kwa madhumuni ya kipindi hiki cha Bajeti tunaomba kwenye Kanuni hizi tuzingatieve dakika kumi.

Tumesema kwamba, vyama vinaweza kuomba katika dakika hizo kumi kugawanya muda kwa Wabunge wasiozidi wawili, wakaongea ndani ya dakika hizo kumi wakagawa katika muda wao wakafanya dakika tano tano, ndiyo, imo pia.

Waheshimiwa Wabunge, katika Kanuni hizi nilimsikia Mheshimiwa Tundu Lissu anasema, Kiti cha Spika kilikuwa kinaruhusu sana baadhi ya watu wanatoka nje kidogo wanapongeza, maneno ya utangulizi kibao, salamu za pole, shukrani na kadhalika. Niseme tu wakati mwingine siyo vizuri sana kwa Kiti cha Spika kumkatiza Mbunge kila wakati anaposimama, maana Mbunge ni Mwakilishi wa Wananchi. (*Makof*)

Tukubaliane kwamba, jambo hili hata kwenye Kanuni za sasa linakatazwa, hivi sasa tumesitiza zaidi kwenye mabadiliko haya. Kwa hiyo, ndugu zangu, ukisimama unakwenda moja kwa moja kwenye hoja. Kwa mapendekezo haya, kama huna cha kusema bora ukae chini usiongee. (*Makof*)

Inasisitizwa humu masuala ya utangulizi, utambulisho, salamu za pole, pongezi, shukrani, kutaja majina ya Wabunge waliochangia, Waheshimiwa Mawaziri hawatasema tena waliochangia akina fulani, walioniandikia kwa maandishi akina fulani, ni kwenye hoja moja kwa moja. Waheshimiwa Wabunge vivyo hivyo. (*Makof*)

Wakati wa kushughulika na mshahara wa Waziri umewekwa utaratibu wa namna ya kupata nafasi kwa masuala yanayohusu Sera peke yake, ni kujielekeza kwenye Sera kweli kweli. Naomba msome kila mmoja aweze kuelewa kilichopo pale ndani.

Vilevile kwenye Kanuni zetu hizi, mabadiliko ambayo tunafanya imetolewa fursa kwa Kamati ya Uongozi, kwa maana ya Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za Bunge, kuweza kukaa pamoja na Kamati ya Bajeti, kwa pamoja kushauriana na baadaye Kamati ya Bajeti itafanya kazi na

Serikali. Baada ya hapo watarudi tena kwenye Kamati ya Uongozi kwa niaba ya Kamati zetu zote na kuweza kutoa *feed back*. Zimewekwa kabisa taratibu mbalimbali za kwenda mbele na kurudi nyuma, kuhakikisha kwamba mwisho wa siku inapokuja kusomwa Bajeti ya Serikali na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, inakuwa ni kitu ambacho kwa kweli kwa kiwango kikubwa kina *consensus* kubwa.

Waheshimiwa Wabunge, kwa maelezo hayo, ningeliomba tuyaunge mkono mapendekezo ya mabadiliko ambayo nimeyapendekeza. Ninawaomba tu kwa mara nyingine mzisome kwa makini sana Kanuni hizi, na hasa hilo Fungu la Tisa la Kanuni zetu. Nawaomba sana mzizingatie, ni mabadiliko muhimu na yanatusaidia sana kusonga mbele, endapo sote tutayaelewa. Naomba sana kila Mheshimiwa Mbunge asome mabadiliko hayo na ayaelewe.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Mwongozo wa Spika.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba kupata Mwongozo wako; katika Kanuni ambazo zimechapishwa Toleo la Aprili, 2013, Nyongeza ya Nane imechapishwa kama jinsi ambavyo ililetwa kama marekebisho lakini hayajawahi kuitishwa na kikao chochote. Katika nyongeza hiyo, mwisho kabisa imeandikwa kwamba, nyongeza hizi zimepitishwa kwa mujibu wa Azimio la Bunge la tarehe 9 Aprili, 2013. Tarehe 9 njana, hatujadili nyongeza hizo, leo ni tarehe 10, mjadala huu hauna nyongeza hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba mwongozo wako ya kwamba, nyongeza hizi zisiwe sehemu ya Kanuni mpya kama jinsi ambavyo Msemaji Mkuu na Mnadhimu wa Kambi ya Upinzani alivyosema, kwa sababu zina kasoro nyingi sana. Kwenye majukumu ya Kamati za

10 APRILI, 2013

Bunge na hasa Kamati ya Hesabu za Serikali, kuna kasoro nydingi sana.

SPIKA: Mheshimiwa, ungepata mwongozo halafu ungeendelea na hizo habari nyingine.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako.

SPIKA: Ninachokisema, nadhani Mheshimiwa Tundu Lissu ni Mjumbe wa Kamati ya Kanuni, hicho kitabu nadhani wewe umekichukua *somewhere* huko, sicho tunachozungumza. Tunachozungumza sisi ni hizo karatasi mlizopewa ambazo Naibu Spika amesoma sasa.

WABUNGE FULANI: Hatuna!

SPIKA: Atagawa! Anagawa! Nasema wakati wanaingia hawa wanamalizia kugawa hizo *documents*. Kwa hiyo, hiyo anayosema Mheshimiwa Tundu Lissu, siyo Tundu Lissu, Mheshimiwa Zitto ni katika kupitapita Ofisi ya Spika amechukua hiyo. Hiyo siyo tunayoshughulika nayo. (*Makof*)

Kwa maana hiyo, tunagawa pia nyongeza ya shughuli za Bunge kwa sababu hiki tutakachopitisha kama Azimio kina hatua zake ambazo lazima zifuatwe; kuna kgazette, kuna vitu vyote hivi. Sasa kuanzia hivi sasa mpaka saa kumi na moja wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapohutubia, hizo hatua zingine zitakuwa zimefanyika. Tunacho-gazette ni sehemu ya mabadiliko, siyo hiyo aliyoisoma Mheshimiwa Zitto. Hiyo nafikiri ameikusanya kusanya Ofisi ya Bunge huko, lakini haijagawiwa.

Sasa namwita Mheshimiwa Cheyo.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Umelijibu karibu nusu. Naomba tu kwamba, hivi ni sawa na baada ya kuhitimisha utuhoji na sisi hatujapata kitu chochote tunachohojiwa. Itakuwa ni kama unatuuzia mbuzi kwenye gunia. (*Kicheko/Makof*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ukweli ni kwamba, hivi vitu vyote mmejadili siku mbili mpaka jana tumetoka saa mbili na nusu na Kamati yangu ya Kanuni imeanza saa mbili, walijaribu kuridhia yote mliyowaambia katika vile vikao vya mahojiano.

Nimesema hili suala ni *in house*, ndiyo maana tukatumia muda mwangi sana katika Kikao chetu cha *Briefing*, kwa sababu *in house* ni mambo yetu sisi wenyewe. Kwa hiyo, hii itatolewa na wamechukulia kwa kiwango kikubwa kabisa yale mliyoyaagiza na kwa mujibu wa Kanuni zetu.

Kamati yetu ya Kanuni imefanya kazi kubwa sana, tena *sleepless nights*. Kwa hiyo, muwaamini hawa na msome, hajabadilisha yale mliyotaka kuyafanya. (*Makofii*)

Kwa hiyo, nitawahoji muiamue hoja hiyo. (*Makofii*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamualiwa na Kuafikiwa*)

(*Azimio la Marekebisho ya Kanuni za Bunge
liliridhiwa na Bunge*)

SPIKA: Kwa hiyo, kitakachotokea kuanzia sasa, wanaendelea kuhitimisha hatua zingine kufuatana na Kanuni zetu zile, Kanuni ya 152 mpaka ya 154. Mtapewa pia Orodha ya Nyongeza ya Shughuli.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nasitisha Kikao cha Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

(*Saa 5.16 asubuhi Bunge lilifungwa hadi saa 11.00 jioni*)

10 APRILI, 2013

(Saa 11.00 jioni Bunge lilitrudia)

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE):

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Idara na Taasisi zilizo chini ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):

Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2012/2013 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA - MWENYEKITI WA KAMATI YA TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:

Taarifa ya Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2012/2013 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

MHE. DIANA M. CHILOLO (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MASUALA YA UKIMWI):

Taarifa ya Kamati ya Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu juu ya Masuala ya UKIMWI kwa mwaka 2012/2013 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

MHE. VICK P. KAMATA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA):

Taarifa ya Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu juu ya Uwekezaji na Uwezeshaji kwa mwaka 2013/2014.

MHE. KABWE Z. ZITTO – (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI JUU YA OFISI YA WAZIRI MKUU):

Taarifa ya Msemadi Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

MHE. KABWE Z. ZITTO – (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI JUU YA OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI):

Taarifa ya Msemadi Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2013/2014
Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa
na Serikali za Mitaa**

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na Taarifa zilizowasilishwa leo na Wenyeiti wa Kamati za Katiba, Sheria na Utawala; Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; na Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara na Kamati ya Masuala ya UKIMWI na Dawa za Kulevyaa ndani ya Bunge lako Tukufu ambazo zimechambua Bajeti ya Mafungu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge lako sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa mwaka 2012/2013 na Mwelekeo kwa mwaka 2013/2014. Vilevile, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa

na Serikali za Mitaa, Taasisi zilizo chini yake pamoja na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa anayoifanya kwa maslahi ya nchi yetu. Mheshimiwa Rais, ameiletea Tanzania sifa, heshima na kuiwezesha kutambulika zaidi Kimataifa katika nyanja mbalimbali. Ziara ya kihistoria ya Mheshimiwa Xi Jinping, Rais wa Jamhuri ya Watu wa China aliyofanya nchini tarehe 24 hadi 25 Machi, 2013 ni ushahidi tosha wa kazi nzuri ya Mheshimiwa Rais ya kukuza ushirikiano wenye maslahi ya kiuchumi kati ya nchi yetu na nchi nyingine. Katika ziara hiyo, Mikataba 16 ya ushirikiano katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ilitiwa saini. Utekelezaji wa Miradi hiyo utachochaea uwekezaji na hivyo kuongeza kasi ya ukuaji uchumi na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa kuwa Wenyeleviti na Makamu Wenyeleviti wa Kamati za Kudumu za Bunge. Vilevile, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa kuiwakilisha Tanzania katika Taasisi mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa. Ni matumaini yangu kwamba, wote walioeteuliwa na kuchaguliwa watatumia nafasi hizo kwa manufaa ya Bunge na kwa maendeleo ya Watanzania kwa ujumla. Hongereni Sana.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala inayoongozwa na Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge wa Viti Maalum na Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla, Mbunge wa Nzega. Nawashukuru pia Wajumbe wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara, inayoongozwa na Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini na Kamati ya Masuala ya UKIMWI na Dawa za Kulevy, inayoongozwa na Mheshimiwa Lediane Mafuru Mng'ong'o, Mbunge wa Viti Maalum.

Kamati hizo zimetoa mchango mkubwa wakati wa uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Mafungu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Mfuko wa Bunge. Aidha, nawashukuru Wajumbe wa Kamati zote za Kudumu za Bunge lako Tukufu, kwa ushauri waliota wakati wa kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara, Mikoa, Wakala, Idara za Serikali Zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Maoni na ushauri wao utazingatiwa wakati wa kukamilisha mjadala wa Bajeti ya Serikali na utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2012/2013, kumekuwa na majanga na matukio mbalimbali yaliyosababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa mali. Miongoni mwa matukio hayo ni ajali mbaya ya Jahazi la *Sunrise* iliyotokea Wangwi katika Bahari ya Hindi mwezi Januari, 2013 na ajali mbalimbali za vyombo vingine vya usafiri ambapo watu walipoteza maisha na wengine kupata majeraha. Hivi karibuni pia tumeshuhudia ajali mbaya ya kuporomoka kwa jengo la ghorofa 16 Jijiini Dar es Salaam, ambalo limesababisha vifo vya watu 34 na tukio lingine ni vifo 13 vilivytokana na kufukiwa na kifusi cha *moram* katika machimbo ya Mushono Jijini Arusha. Aidha, tumempoteza ghafla Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, aliyekuwa Mbunge wa Chambani na baadhi yetu tumepoteza Ndugu, wakiwemo Wazazi na Watoto kutokana na sababu mbalimbali. Wote nawapa pole sana.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka wa fedha 2013/2014, tumekubaliana kuanza Mzunguko Mpya wa Bajeti ambaao utatuwezesha kukamilisha Mjadala wa Bajeti ya Serikali mapema. Lengo ni kwamba, ifikapo tarehe 30 Juni ya kila mwaka, taratibu zote za kuandaa, kuchambua na kupitisha Bajeti ya Serikali ziwe zimekamilika na utekelezaji wa Bajeti kuanza ifikapo tarehe 1 Julai. Tofauti na miaka ya nyuma ambapo Bajeti ya Serikali ilikuwa ikijadiliwa na kupitishwa kwanza na kufuatiwa na Bajeti za Kisekta, sasa makadirio na matumizi ya Wizara yatajadiliwa kwanza na hatimaye kuhitimishwa na majadiliano ya kina ya Bajeti ya Serikali. Moja ya faida kubwa ya utaratibu huu mpya ni

kwamba, mwaka mpya wa fedha unapoanza, utekelezaji wa kazi za Serikali unaanza mara moja. Utaratibu huo utawawezesha Waheshimiwa Mawaziri na Wabunge pamoja na Watendaji wa Serikali, kurejea katika kazi zao na kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Bajeti na Mpango wa Maendeleo. Kwa kuwa tunaanza kwa mara ya kwanza kutumia utaratibu huo, hazitakosekana dosari chache ambazo zitafanyiwa kazi kadiri tunavyoendelea kuutumia.

Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutumia fursa hii kutoa maoni na ushauri utakaosaidia kuboresha Bajeti ya Serikali ili iwe bora zaidi na yenye maslahi makubwa kwa Wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya Bajeti yamezingatia llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2010; Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano; Malengo ya Maendeleo ya Milenia na Awamu ya Pili ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini. Katika mwaka 2013/2014, Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi wa rasilimali chache tulizonazo ili kutekeleza Miradi ya Maendeleo ya Kipaumbele ambayo itachochea ukuaji wa haraka wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza sana Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Bwana Ludovick Utouh, pamoja na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kusimamia rasilimali za Serikali. Matunda ya kazi hii yameonekana hadi nje ya nchi na ndiyo maana Ofisi hii sasa imepandishwa hadhi kutoka Daraja la Kwanza hadi la Tatu kwa vigezo vinavyotumiwa na Muungano wa Ofisi za Ukaguzi wa Hesabu za Serikali katika Bara la Afrika kwa Nchi zinazotumia Kiingereza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya siasa, nchi yetu imepiga hatua ya kuridhisha katika kuimarisha Demokrasia ya Vyama Vingi. Kwa ujumla hali ya kisiasa nchini ni tulivu na Vyama vya Siasa vinaendelea kutekeleza majukumu yake. Idadi ya Vyama vya Siasa vyenye usajili wa kudumu imefikia

20 baada ya Chama cha *Alliance for Democratic Change (ADC)* kupata usajili wa kudumu. Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMA), kilipata usajili wa muda na zoezi la uhakiki wa Wanachama linaendelea. Chama cha *Movement for Democratic and Economic Change* kilifutwa baada ya kukosa sifa za kupata usajili wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, ili Demokrasia nchini izidi kuimarika na Wananchi washiriki kikamilifu kwenye siasa, Viongozi wote wa Vyama vyta siasa wana wajibu mkubwa wa kuendesha Siasa za kistaarabu, zinazozingatia maadili ya Kitanzania na kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu. Wito wangu kwa Vyama vyote ni kuendelea kuvumiliana na kutohamasisha siasa za chuki au vurugu ambazo zitatugawa na kuhatarisha Amani, Utulivu na Umoja wetu ambao umewekezwa kwa miaka mingi. Mwenye Macho haambiwi Tazama! Wote ni mashahidi wa matatizo makubwa ambayo yamezikumba nchi zilizoingia katika siasa za chuki na vurugu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Ofisi ya Msajili wa Vyama vyta Siasa itaandaa mapendekezo ya kufanya mapitio ya Sheria ya Vyama vyta Siasa ya Mwaka 1992 na Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya Mwaka 2010. Aidha, itaendelea na usajili wa Vyama vyta Siasa, kutoa elimu ya demokrasia kwa Wananchi na kuboresha Baraza la Vyama vyta Siasa. Hatua hizo zitazidi kuimarisha Demokrasia ya Vyama Vingi Nchini.

Mheshimiwa Spika, ulinzi na usalama wa hali ya mipaka ya nchi yetu kwa ujumla ni shwari na Wananchi wanafanya shughuli zao bila vikwazo. Katika kuimarisha usalama wa mipaka yetu, Viongozi wa Mikoa ya Kagera, Kigoma, Rukwa na Tanga, wamefanya vikao vyta ujirani mwema na wenzao wa Mikoa ya mipakani mwa nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Rwanda, Burundi, Zambia na Kenya. Pamoja na hali nzuri ya usalama wa mipaka yetu, bado tunakabiliwa na changamoto ya Wahamiaji haramu wanaotumia nchi yetu kama mapito ya kuelekea nchi nyingine au kufanya makao nchini. Ili kukabiliana na tatizo hilo, Serikali inaendesha misako ya kuwabaini, kuwakamata

na kuwafikisha kwenye Vyombo nya Sheria. Serikali pia, imeendelea kutoa elimu kwa Wananchi wa Mikoa ya mipakani ili kutoa taarifa za Wahamiaji haramu. Natoa wito kwa Wananchi wote kushirikiana na Serikali kuwabaini na kuwafichua wahamiaji haramu na wale wanaowasafirisha ili wachukuliwe hatua stahiki za Kisheria.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na jamii kuititia dhana ya Ulinzi Shirikishi inafanya kazi nzuri ya kudhibiti vitendo nya uhalifu nchini. Jumla ya makosa makubwa ya jinai yaliyotolewa taarifa katika vituo nya polisi nchini yalipungua kutoka 69,678 mwaka 2011 hadi 66,255 mwaka 2012. Katika kipindi cha Januari hadi Februari, 2013 makosa ya jinai yalikuwa 10,548 ikilinganishwa na makosa 10,989 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2012. Jeshi la Polisi pia limedhibiti kwa kiasi kikubwa uingizaji wa silaha haramu ambapo jumla ya silaha 405 zillikamatwa katika operesheni mbalimbali kati ya Januari na Desemba, 2012. Natumia fursa hii kulipongeza Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri ya kutekeleza kikamilifu dhana ya Ulinzi Shirikishi na kuwahamasisha wananchi kuhusu utii wa sheria bila shuruti. Aidha, napenda kuwakumbusha Wananchi wote kwamba, suala la ulinzi na usalama wa nchi yetu ni jukumu letu sote. Ni wajibu wetu kutoa taarifa za vitendo nya uhalifu kwa Jeshi letu ili hatua za kudhibiti vitendo hivyo zichukuliwe. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudzi za Serikali za kuwahudumia Wazee na Watu Wenye Ulemavu, siku za karibuni kumeibuka tena dalili za vitendo nya ukatili dhidi ya wazee, wanawake na walemavu wa ngozi katika baadhi ya mikoa kwa sababu za kishirikina. Ukatili huo siyo tu unyama uliopindukia kwa binadamu wenzetu bali pia unaondoa sifa kubwa ya jamii yetu ya kupendana pasipo kujali rangi, dini au kabila. Nitumie fursa hii kuwahakikishia ndugu zetu wenyе ulemavu wa ngozi, akina mama na wazee kwamba, Serikali haitavumilia kuona ukatili wowote unafanywa dhidi yao.

Naziagiza Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya zote nchini kwa kushirikiana na jamii, kuwabaini na

kuwafikisha kwenye Vyombo vy'a Sheria wale wote wanaojihusisha na vitendo hivyo viovu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetoa uhuru kwa Wananchi wake kuabudu, kila mtu kwa dini anayoitaka. hata hivyo, hivi karibuni kumejitokeza migongano na chokochoko za kidini ambazo zimeanza kueneza chuki mionganoni mwetu. Chokochoko zinazojitokeza si dalili nzuri kwa mustakabali wa nchi yetu inayopenda kudumisha Amani, Utulivu na Umoja wa Kitaifa.

Uzoefu wa Mataifa mbalimbali umeonesha kwamba, chokochoko za Kidini zimesababisha machafuko makubwa na kutoweka kwa amani katika Nchi hizo. Tukumbuke kwamba, yakinjua machafuko ya namna hiyo na kuvurugika kwa amani na utulivu, hakuna atakayesalimika. Hivyo, natoa wito kwa Viongozi wa Madhehebu ya Dini kuelimisha Waumini wao kuthamini na kuheshimu Dini za wengine na kuepuka vitendo vyovoyote vinavyoamsha hisia za chuki mionganoni mwa Wafuasi wa Dini mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Serikali iliahidi kukarabati na kujenga Makambi kwa ajili ya kuchukua Vijana watakaojiunga na Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa Sheria. Ninayo furaha kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imetekeleza ahadi ilizotoa mwaka jana kwa ufanisi mkubwa. Mafunzo ya JKT kwa mujibu wa Sheria yameanza mwaka huu kwa kuchukua Vijana 4,711, sambamba na Vijana 5,893 wa kujitolea, wakiwemo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge. Nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge Vijana waliojiunga na Mafunzo ya JKT mwaka huu. Katika mwaka 2013/2014, Serikali itaendelea kuchukua Vijana kwa ajili ya Mafunzo ya JKT kwa Mujibu wa Sheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliendesha Chaguzi Ndogo za Madiwani katika Kata 29 Tanzania Bara ili kujaza nafasi wazi za Viti vya Udiwani. Katika chaguzi hizo, Chama cha Mapinduzi kilishinda Viti 22, CHADEMA Viti vitano na CUFna TLP Kiti kimoja kimoja.

Vilevile, Tume ilifanya teuzi 15 ili kujaza nafasi zilizokuwa wazi za Udiwani wa Viti Maalum. Katika uteuzi huo, CCM ilipata viti 10, CHADEMA viti vinne na *TLP* kitiko mmoja. Katika mwaka 2013/2014, Tume ya Taifa ya Uchaguzi itaboresha Daftari la Wapiga Kura, ambapo Awamu ya Kwanza itakamilika mwezi Desemba, 2013. Uboreshaji huo utawezesha kuchapishwa kwa Daftari la Wapiga Kura kwa ajili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2014 na Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, uchaguzi wa Serikali za Mitaa ngazi ya Vitongoji, Vijiji na Mitaa unatarajiwa kufanyika mwezi Oktoba 2014. Kazi za awali za uchaguzi huo zinaendelea kufanyika ikiwa ni pamoja na kupitia upya Kanuni za Uchaguzi zitakazojumuisha maoni ya wadau mbalimbali. Ili kufanikisha uchaguzi huo, Halmashauri zote Nchini zinatakiwa kuanza maandalizi mapema kwa kupitia na kuhakiki orodha ya vitongoji, vijiji na mitaa. Baada ya kuhakiki orodha hiyo, maombi mapya ya kugawa vitongoji, vijiji au mitaa yawasilishwe katika ngazi husika kabla ya tarehe 31 Desemba, 2013 kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Bunge limeendelea kutekeleza majukumu yake ya kuisimamia na kuishauri Serikali katika nyanja mbalimbali. Aidha, Bunge limefanya Mikutano mitatu, kupitisha Miswada minne ya Sheria na kuridhia Maazimio manane. Katika kuboresha utendaji wa Kamati za Kudumu za Bunge, Wajumbe wa Kamati hizo walipatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo ili kumudu majukumu yao vizuri katika nyanja za utafiti, uchambuzi wa Miswada, Sera na Bajeti, utunzaji wa kumbukumbu na taratibu za uendeshaji wa Bunge. Vilevile, kuanzia tarehe 4 hadi 7 Desemba, 2012 Bunge liliandaa kwa mafanikio Mkutano wa Umoja wa Mabunge Duniani uliofanyika Dar es Salaam ukiwa na kaulimbiu ya "Vita Dhidi ya Ukatili wa Wanawake."

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha utendaji na kuongeza ufanisi, Kamati za Kudumu za Bunge zimefanyiwa mabadiliko makubwa kwa kuunda Kamati mpya ya Bajeti na kugawanya baadhi ya Kamati. Iliyokuwa Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama

imegawanywa mara mbili na kuwa Kamati ya Mambo ya Nje na Kamati ya Ulinzi na Usalama. Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala imegawanywa na kuwa Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala na Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Vilevile, Kamati zilizokuwepo awali nazo zimeundwa upya na baadhi kuongezewa majukumu. Ni imani yangu kwamba, Kamati hizo zitatekeleza wajibu wake kikamilifu kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Serikali imeendelea kuratibu masuala yote ya Muungano na yasiyo ya Muungano, kwa lengo la kudumisha Muungano na ushirikiano wa Serikali zote mbili. Katika kudumisha ushirikiano huo, Kikao cha Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ cha kushughulikia Masuala ya Muungano kilifanyika na kujadili hoja zinazohusu utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilla; ushiriki wa Zanzibar katika Taasisi za Nje na katika Jumuiya ya Afrika Mashariki; Ongezeko la gharama za umeme wa *TANESCO* kwa *ZECO*; Usajili wa vyombo vy'a moto, malalamiko ya Wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili na mgawanyo wa mapato.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mabadiliko ya Katiba inaendelea kuratibu, kukusanya na kuchambua maoni ya Wananchi ili kupata Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayotokana na ridhaa ya Wananchi wenyewe ifikapo mwaka 2014. Katika mwaka 2012/2013, Tume imekusanya maoni ya Wananchi kuititia njia mbalimbali na kuanza uchambuzi wa maoni yaliyotolewa ili kuanda Rasimu ya Katiba.

Tume pia, imeanza maandalizi ya kuunda Mabaraza ya Katiba katika Ngazi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Mabaraza ya Katiba yanayojumuisha Asasi, Taasisi na Makundi Maalum ya Watu. Mabaraza hayo yatakuwa na jukumu la kuititia na kutoa maoni juu ya Rasimu ya Katiba ilioandaliwa na Tume. Mabaraza ya Katiba yatawashirikisha na kuwakutanisha wawakilishi kutoka makundi mbalimbali ya Wananchi katika jamii.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Tume itaratibu Mikutano ya Mabaraza ya Katiba Mpya, kuchambua maoni ya Mabaraza ya Katiba na kuandaa Rasimu ya Katiba Mpya itakayowasilishwa katika Bunge Maalum la Katiba. Vilevile, itachapisha Katiba iliyotokana na maoni ya Bunge Maalum la Katiba kwa ajili ya kupigwa Kura ya Maoni. Naipongeza sana Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwa kazi nzuri waliyoifanya hadi sasa. Nawashi Watanzania wote kuendelea kutoa ushirikiano kwa Tume ili iweze kukamilisha kazi hii muhimu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2012 ulikuwa ni Mwaka wa Sensa ya Watu na Makazi ambayo ni ya tano kufanyika tangu kuasiwiwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Matokeo yanaonesha kuwa, idadi ya watu nchini imeongezeka kutoka watu milioni 34.5 mwaka 2002 hadi milioni 44.9 mwaka 2012. Hilo ni ongezeko la watu milioni 10.4 kwa kipindi cha miaka kumi, sawa na ukuaji wa wastani wa asilimia 2.7 kwa mwaka. Kwa ujumla, matokeo ya Sensa yanaonesha kasi ya ongezeko la watu ni kubwa ikilinganishwa na kasi ya ukuaji wa Pato la Taifa. Kwa kutambua changamoto hiyo, Serikali pamoja na mambo mengine inaendelea kutekeleza Sera ya Idadi ya Watu ya Mwaka 2006 kwa kuelimisha Wananchi kuhusu umuhimu wa uzazi wa mpango.

Nitumie fursa hii kulikumbusha Bunge lako Tukufu na Watanzania, kazi ya uchambuzi wa takwimu inaendelea ili kupata mchanganuo wa kina zaidi utakaoiwezesha Serikali kupanga vizuri Mipango yake ya Maendeleo. Katika mwaka 2013/2014, Serikali itasambaza taarifa mbalimbali za Sensa ya Watu na Makazi zenye mchanganuo wa kitakwimu na kuhamasisha matumizi yake katika tafiti na kuandaa Mipango ya Maendeleo katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, tarehe 7 Februari 2013, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alizindua rasmi Mfumo wa Utambuzi na Usajili wa Watu, Jijini Dar es Salaam. Vilevile, tarehe 13 Februari, 2013, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, alizindua

zoezi hilo kwa upande wa Zanzibar. Kuzinduliwa rasmi kwa mfumo huo ni mwanzo wa utoaji wa Vitambulisho vya Taifa ambavyo vitasaidia kuwatambua na kuwahudumia Wananchi ipasavyo. Zoezi la utoaji wa Vitambulisho vya Taifa linaendelea kwa Watumishi wa Umma waliokuwa wamesajiliwa na kuhakikiwa.

Zoezi la kuingiza taarifa za Wananchi 220,000 kwa ajili ya kupatiwa Vitambulisho vya Taifa katika Wilaya ya Kilombero iliyoteuliwa kuwa Wilaya ya mfano limekamillka na uchambuzi wa taarifa za Wakazi wa Dar es Salaam 2,159,822 waliojiandikisha zinaendelea. Aidha, Wakazi wa Zanzibar 160,645 na Wageni 180 wameandikishwa. Kazi ya Utambuzi na Usajili wa Watu katika Mikoa mbalimbali nchini inaendelea, sambamba na utoaji wa vitambulisho kwa wale walioandikishwa na kuhakikiwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012, Pato halisi la Taifa lilikuwa kwa asilimia 6.9 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.4 mwaka 2011. Sekta zilizochangia zaidi katika ukuaji huo ni pamoja na Mawasiliano, Fedha, Viwanda, Ujenzi, Madini, Biashara na Utalii. Kutokana na ukuaji huo, Wastani wa Pato la Mtanzania umeongezeka kutoka Shilingi 869,436 mwaka 2011 hadi Shilingi 995,298 mwaka 2012, sawa na ongezeko la Asilimia 12.6. Mfumko wa Bei umepungua kutoka asilimia 19.4 mwezi Februari, 2012 hadi asilimia 9.8 mwezi Machi, 2013. Kupungua kwa Mfumko wa Bei kumechangiwa na jitihada za Serikali za kuongeza usambazaji wa vyakula kwenye masoko, kupunguza ujazi wa fedha kwenye soko, kudhibiti upandaji wa bei ya mafuta ya petroli na kuimarika kwa upatikanaji wa umeme viwandani ikilinganishwa na mwaka 2011/2012. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambao ulipitishwa na Bunge lako Tukufu mwaka 2011/2012. Katika kutekeleza Mpango huo, Tume ya Mipango imeweka utaratibu wa kuchambua kwa kina maandiko ya Miradi yote ya Kisekta ili kuhakikisha kwamba imezingatia vipaumbele ambavyo sote tumekubaliana. Baada ya uchambuzi huo, ndipo fedha

hutolewa kwa ajili ya utekelezaji. Pamoja na utaratibu huo, Serikali imeona ni muhimu kuongeza kasi ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kuanzisha mfumo imara zaidi wa kupanga Vipaumbele, kufuatilia na kutathmini Utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati ya Maendeleo. Mfumo huo ambao utasimamiwa na Chombo Maalum (*President's Delivery Bureau*), chini ya Ofisi ya Rais, Ikulu, unazingatia uzoefu wa Nchi ya Malaysia. Chini ya mfumo huo, Miradi ya kipaumbele itakayotekelawa itatengewa fedha za kutosha na usimamizi wa kina utafanyika kuhakikisha kwamba malengo yaliyowekwa yanafikiwa.

Mheshimiwa Spika, ili mfumo huo ufanikiwe, inabidi kwanza wadau wote wakubaliane kimsingi vipaumbele ambavyo vitatoa matokeo makubwa na ya haraka na kisha Wataalamu kutoka Serikalini, Sekta Binafsi na Mashirika yasiyo ya Kiserikali, kukaa pamoja na kuchambua kwa undani vipaumbele hivyo, namna ya kuvitekeleza, kubaini watekelezaji na kuibua viashiria vyatupu matokeo.

Tayari zoezi hilo la awali limefanyika ambapo maeneo sita ya kwanza ya kipaumbele yamefanyiwa uchambuzi wa kina kwa utaratibu unaojulikana kama Maabara (*Labs*). Utaratibu huo wa maabara unatoa fursa kwa wataalam na watunga sera kukaa pamoja, kufikiri na kuendesha majadiliano ya wazi hadi pale wanapokubaliana kwamba ufumbuzi wa tatizo umepatikana. Maeneo yaliyojadiliwa katika awamu ya kwanza ni Nishati na Gesi Asilia, Uchukuzi, Kilimo, Elimu, Maji na Kupanua wigo wa Mapato ya Serikali. Baada ya uchambuzi huo kukamilika, matokeo yake ikiwemo Miradi iliyoandalialiwa pamoja na Bajeti ya utekelezaji, itawekwa hadharani ili kila Mtanzania ajue kitakachofanyika, kutoa maoni na kufuatilia kwa kina utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba kunakuwepo na uwajibikaji wa kutosha katika kutekeleza vipaumbele vyatupu Kitaifa, Chombo kitakachoanzishwa (*President's Delivery Bureau*), kitakuwa na jukumu la kuhakikisha kwamba kila Waziri wa Kiseka na Watendaji Wakuu wanawajibika kusimamia utekelezaji wa Miradi ya

kipaumbele na pia kufanya tathmini za mara kwa mara kupima matokeo. Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Mawaziri wanaosimamia maeneo sita ambayo tumeanza nayo, walitoa ahadi kwamba watakuwa mstari wa mbele kusimamia kwa weledi utekelezaji wa Miradi ya Sekta zao. Ahadi hizo walizitoa wakati wa uzinduzi wa awamu ya kwanza ya mfumo wa maabara uliofanywa na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 22 Februari, 2013. Ni matumani yangu kuwa, utaratibu huo utasaidia sana kuimarisha uwajibikaji, ufuatiliaji na hatimaye kupata matokeo ya haraka ambayo yatasaidia uchumi kukua kwa kasi zaidi na hivyo kupunguza umaskini mionganoni mwa watu wetu. Ni vyema ieleweke wazi kwamba, maeneo ya kipaumbele yaliyochaguliwa yatapata sehemu kubwa ya fedha za maendeleo.

Hii ndiyo maana ya dhana ya kupanga ni kuchagua na haina maana kwamba kazi nyingine za uendeshaji wa Serikali zitasimama. Katika Mwaka 2013/2014, kutafanyika uchambuzi wa kina wa maeneo mengine ya kipaumbele ambayo yatasaidia Serikali kupanga Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji Nchini. Lengo ni kuimarisha ushiriki wa Sekta Binafsi katika shughuli za uwekezaji na biashara nchini. Katika utekelezaji wa Mpango Kazi huo, Serikali imeazimia kupunguza muda unaotumika kuitisha mizigo bandarini na mipakani kwa kuanzisha utaratibu wa kubadilishana taarifa zinazohusu mizigo kwa njia za kielektroniki kabla mizigo haijafika kwenye vituo vya forodha.

Vilevile, Kamati za Pamoja (*Joint Border Post Committees*), zimeundwa kwenye Vituo vya Mipakani vya Tunduma, Kabanga, Mutukula, Holili, Sirari na Namanga. Kupitia Kamati hizo, Wadau wote wanaoshughulika na utoaji huduma mipakani hufanya kazi kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha Mkakati na Mpango Kazi wa Utekelezaji wa Sera ya Ubina baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*PPP*). Vilevile, Mwongozo wa Utendaji kwa ajili ya kutekeleza Sera, Sheria na Kanuni za Ubina baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi umekamilika. Aidha, Serikali imefanya tathmini ya Sera zinazohusu Uwekezaji kwa kutumia Mfumo wa Tathmini unaotumiwa na Shirika la Kimataifa la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (*OECD*). Taarifa ya tathmini ya Sera hizo itachangia katika kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya mwaka 1996 pamoja na Sheria yake ya mwaka 1997. Nazihimiza Wizara na Taasisi za Serikali kuongeza juhudini katika kuainisha Miradi inayokidhi vigezo vya kutekelezwa kwa utaratibu wa *PPP* ili nchi iweze kunufaika na fursa zinazotokana na utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuratibu majadiliano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi illi kuibua fursa zilizopo na kupata ufumbuzi wa changamoto za kisera, kisheria na kitaasisi zinazokwamisha biashara na uwekezaji. Kutowa na umuhimu wa majadiliano hayo, Tanzania itakuwa mwenyeji wa Mkutano wa Kimataifa wa Majadiliano ya Ushirikiano kwa Manufaa ya Wote wa mwaka 2013 (*Global 2013 Smart Partnership Dialogue*), utakaofanyika mwezi Julai, 2013, Jijini Dar es Salaam. Maandalizi ya mkutano huo yanaendelea ambapo mkutano maalum kwa Wakuu wa Mikoa, Wilaya na Makatibu Tawala wa Mikoa ulifanyika Mjini Dodoma mwezi Novemba, 2012. Katika Mkutano huo, washiriki walipata uelewa wa pamoja wa dhana ya majadiliano ya ushirikiano kwa manufaa ya wote yatakayowasaidia kusimamia majadiliano katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetoea mwongozo kwa Mabaraza ya Biashara ya Mikoa na Wilaya kuendesha majadiliano katika maeneo yao ili matokeo ya majadiliano hayo yatumike kikamilifu wakati wa majadiliano ya Kimataifa mwezi Julai, 2013. Uzoefu wa Nchi ambazo zimeandaa majadiliano kama hayo umeonesha kwamba kuna manufaa makubwa yakiwemo kubaini wagunduzi na wabunifu, kuibua fursa mpya za teknolojia na uwekezaji na pia kupata usoefu

wa Mataifa mengine katika masuala mbalimbali. Natoa wito kwa Mabaraza ya Biashara ya Mikoa na Wilaya kuendesha majadiliano katika maeneo yao na kujilandaa kikamilifu kushiriki katika mkutano huo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari 2012 hadi Desemba 2012, Kituo cha Uwekezaji Tanzania kilisajili Miradi 869 yenye thamani inayokadiriwa kufikia Shilingi Bilioni 30,866. Kati ya Miradi hiyo, Miradi 469 sawa na asilimia 54 ni ya Wawekezaji wa ndani, Miradi 195 sawa na asilimia 22 ni ya ubia kati ya Wawekezaji wa ndani na nje na Miradi 205, sawa na asilimia 24 ni ya Wawekezaji kutoka Nje. Usajili wa Miradi hiyo umeongeza ajira nchini ambapo zaidi ya Watanzania 174,412 walipata ajira kwenye Miradi hiyo.

Tathmini ya thamani ya uwekezaji Kisekta inaonesha kwamba, katika mwaka 2012 Miradi ya Sekta ya Kilimo inaongoza ikiwa imechangia Shilingi Bilioni 14,226, ikifuatiwa na Sekta ya Uzalishaji Viwandani iliyochangia Shilingi Bilioni 4,672. Sekta hizo zinafuatiwa na Sekta ya Mawasiliano iliyochangia Shilingi Bilioni 4,663 na Sekta ya Nishati iliyochangia Shilingi Bilioni 2,110. Pamoja na mafanikio hayo, bado kuna changamoto kubwa ya kufanya kazi kama Timu moja katika kuvutia Wawekezaji. Ili kuweza kuvutia wawekezaji katika hali endelevu, ni muhimu sana Sera na Sheria za Uwekezaji zikatoa mwongozo amba o unatabirika kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeratibu na kufanya tathmini ya Mifuko mbalimbali ya Uwezesaji Wananchi Kiuchumi. Mifuko hiyo ni pamoja na Mfuko wa Uwezesaji wa Mwananchi, Mpango wa Uwezesaji Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira, *SIDO, SELF, Agriculture Input Trust Fund* na *Presidential Trust Fund*. Mifuko mingine ni Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, Mfuko wa Udhamini wa Mikopo kwa Mauzo ya Nje na Mfuko wa Kudhamini Taasisi za Fedha Kutoa Mikopo kwa Miradi Midogo na ya Kati. Makubaliano yaliyofikiwa baina ya Serikali na Taasisi za Fedha zilizoteuliwa kutoa mikopo kwa Wajasiriamali ni kwamba, Taasisi hizo zikopeshe mara tatu

zaidi ya dhamana iliyotolewa na Serikali. Katika kutekeleza makubaliano hayo, hadi Desemba, 2012 Mpango wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira ulitoa mikopo kwa Wajasiriamali 76,546 yenye thamani ya Shilingi Bilioni 50.06.

Urejeshaji wa mikopo hiyo umefikia wastani wa asilimia 82. Aidha, katika kipindi hicho, Mfuko wa Uwezeshaji wa Mwananchi umetoa mikopo ya Shillingi Bilioni 8.6 kwa Mikoa 11, Wilaya 27, Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOs) 49 na Wajasiriamali 8,497. Ufutiliaji wa maendeleo ya Mifuko mbalimbali ya uwezeshaji unaonesha kuwa Wananchi waliopata mikopo wameweza kupiga hatua za kimaendeleo kwa kuongeza tija na uzalishaji katika shughuli zao na hatimaye kuongeza kipato na kuboresha hali zao za maisha.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa awamu ya pili ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*) ulikamilika mwaka 2012. Tathmini ya utekelezaji imeonesha kwamba, *TASAF* imetoa mchango mkubwa katika kuwezesha utekelezaji wa Miradi mingi ya Maendeleo Vijiji iliyoibuliwa na Wananchi. Katika utekelezaji wa awamu hiyo, jumla ya Miradi 1,010 yenye thamani ya Shilingi Bilioni 20 ililibuliwa na kuwezesha katika Wilaya za Tanzania Bara na Zanzibar. Aidha, mafunzo ya ujasiriamali yalitolewa kwa vikundi 1,778 vyenye Wanachama 22,712 katika Halmashauri 44 kwa lengo la kuviiimarisha ili kuongeza ufanisi zaidi katika shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mafanikio hayo, tarehe 15 Agosti, 2012, Awamu ya Tatu ya *TASAF* ilizinduliwa Mjini Dodoma na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Awamu hiyo itakayogharimu jumla ya Shilingi Bilioni 440 inatekeleza Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini Zilizo Katika Mazingira Hatarishi. Mpango huo unalenga kuziwezesha kaya maskini kupata chakula na kujlongezea fursa za kipato kwa kuzipatia fedha ili kumudu mahitaji ya msingi kama vile lishe bora, huduma za afya na elimu. Mpango huo utakaotekelezwa kwa awamu katika Halmashauri zote Tanzania Bara na Zanzibar, umeanza kwa utambuzi wa Kaya maskini katika vijiji

20 vya Halmashauri ya Bagamoyo ambapo jumla ya Kaya 3,056 zimetambuliwa. Zoezi hilo linaendelea kwenye Halmashauri nyingine 13 na ifikapo Juni, 2014, Halmashauri zote Nchini zitafikiwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mipango na mikakati mbalimbali ya kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Hatua hizo ni pamoja na kutekeleza Azma ya KILIMO KWANZA, Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP), Mpango wa Utoaji wa Ruzuku ya Pembejeo na Dawa za Kilimo, Programu ya Kuendeleza Kilimo katika Ukanda wa Kusini mwa Tanzania (*SAGCOT*), Programu Kabambe ya Kuendeleza Kilimo Barani Afrika (*Comprehensive Africa Agriculture Development Programme – CAADP*) na kuboresha huduma za ugani na utafiti katika Sekta ya Kilimo. Hatua nyingine ni pamoja na kuvutia Wawekezaji katika Sekta ya Kilimo, kuhimiza Kilimo cha Umwagiliaji, kuongeza fursa za upatikanaji wa zana bora za kilimo hasa matrektu, kuimarisha masoko na kurahisisha upatikanaji wa mitaji kutoka vyombo vya fedha, hususan kupitia Dirisha la Kilimo katika Benki ya Maendeleo Tanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge Iako Tukufu kuwa, jitihada za kuendeleza Kilimo zimeanza kuleta matumaini hasa katika kuongeza upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo na kuongeza tija na uzalishaji. Kwa mfano, katika mwaka 2012/2013, Tani 226,092 za mbolea zillifikishwa kwa Wakulima 3,792,000 nchini na upatikanaji wa mbegu bora ulifikia Tani 30,443 ikilinganishwa na Tani 28,612 zilizozalishwa mwaka 2011/2012. Kutokana na ongezeko la matumizi ya mbolea na Wakulima kuzingatia Kanuni za Kilimo Bora, tija anayopata mkulima katika Zao la Mahindi Chotara kwa sasa ni wastani wa tani 3.9 kwa hekta na tija ya uzalishaji wa Zao la Mpunga ni tani 3.8 kwa hekta katika maeneo ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianza kutekeleza Mpango wa utoaji ruzuku ya mbolea na mbegu bora kwa kutumia utaratibu wa Vocha mwaka 2008/2009. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana kutokana na utaratibu huo, hasa kuongezeka

kwa upatikanaji na matumizi ya mbolea na mbegu bora pamoja na tija katika uzalishaji wa mazao ya kilimo, mpango huo umekuwa na changamoto kadhaa. Changamoto zilizojitokeza ni pamoja na mbolea na vocha kuchelewa kufika kwa walengwa; uteuzi wa mawakala usiozingatia vigezo na udanganyifu uliofanywa na baadhi ya Mawakala kwa kushirikiana na Watumishi wasio waaminifu pamoja na Wajumbe wa Kamati za Pembejeo katika ngazi mbalimbali za utekelezaji. Serikali imechukua hatua kwa kufanya ukaguzi maalum kwenye maeneo yaliyokuwa na upungufu huo na wallobainika kuhusika na udanganyifu wamefikishwa kwenye vyombo vyanya sheria.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Serikali iliahidi kufanya mapitio ya Mfumo wa utoaji wa mbolea ya ruzuku na mbegu bora kwa kutumia utaratibu wa Vocha ili kuondoa upungufu ullojitokeza. Napenda kullarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imeboresha mfumo huo na kuanzia mwaka 2013/2014 ruzuku ya pembejeo za kilimo itatolewa kwa mikopo kupitia vikundi vyanya wakulima.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Serikali imepanua eneo la kilimo cha umwagiliaji nchini. Miongoni mwa kazi zilizotekelawa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu katika skimu 21 za umwagiliaji zenyenye eneo la hekta 19,567. Kazi nyiningine zinazoendelea ni kukamilisha ujenzi wa mabwawa matano ya umwagiliaji ya Mahiga (Kwimba); Inala (Tabora); Lwanyo (Mbarali); Mesaga (Serengeti) na Dongobesh (Mbulu). Miradi mingine iliyotekelawa ni Skimu 34 zenyenye eneo la Hekta 17,824 kwa kutumia Mfuko wa Wilaya wa Kuendeleza Umwagiliaji. Katika mwaka 2013/2014, Serikali itaanza ujenzi wa mabwawa matatu ya Idodi (Iringa); Manyoni (Singida) na Masengwa (Shinyanga Vijijini).

Mheshimiwa Spika, kilimo cha matunda na mboga kina mchango mkubwa katika ukuaji uchumi, fursa za ajira, lishe na kupunguza umaskini. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Serikali inatekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kuendeleza Mazao ya Bustani wa Mwaka 2010/2011 – 2020/2021. Utekelezaji wa Mkakati huo unaolenga kukuza uwekezaji katika mnyororo

wa thamani wa mazao ya bustani; ujenzi wa miundombinu; uhifadhi bora wa mazao ya bustani; ujenzi na utafutaji wa masoko; na ukuzaji rasilimali watu, umeanza kuonesha matokeo mazuri. Uzalishaji wa mazao ya bustani umeongezeka kutoka Tani milioni 4.1 mwaka 2009/2010 hadi Tani milioni 5.1 mwaka 2012/2013 na mauzo ya mazao hayo nje ya nchi yameongezeka kutoka Shilingi Bilioni 159.8 mwaka 2009 hadi Bilioni 602.1 mwaka 2012. Mafanikio haya ni ya kuridhisha ingawa bado kuna fursa kubwa ya kuongeza tija na ufanisi katika Sekta hii. Tayari tunao Mwongozo wa Kilimo cha Embe ambao utatuwezesha kuongeza tija na uzalishaji wa zao hilo. Miongozo ya Uzalishaji bora wenye tija kwa mazao mengine ya bustani itaandaliwa. Katika mwaka 2013/2014, Serikali itatoa mafunzo ya teknolojia za uzalishaji wa miche bora ya mazao ya bustani hususan kwa vikundi vya vijana.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa bei za Mazao Makuu ya Biashara Nchini ambayo ni Pamba, Kahawa, Chai, Tumbaku, Korosho, Katani na Pareto umekuwa ukibadilika mara kwa mara kwa kutegemea bei za Soko la Dunia. Mabadiliko hayo yanawaathiri sana wakulima wetu pale bei zinaposhuka. Kutokana na hali hiyo, Serikali ilikutana na Wadau wa Mazao Makuu Asilia ya Biashara Nchini ili kuangalia uwezekano wa kuanzisha Mfuko Maalum wa Kufidia bei za Mazao kwa Wakulima pale zinaposhuka (*Price Stabilization Fund*). Lengo ni kuwawezesha Wakulima kupata bei nzuri ya mazao na kuwaepusha na hasara inayotokana na kushuka kwa bei hizo katika Masoko ya Kimataifa na pia kuwahamasisha Wakulima kuendelea kulima mazao husika. Serikali kwa kushirikiana na Wataalam kutoka Bodi sita za Mazao, inayafanya kazi maoni ya Wadau kuhusu kuanzisha Mfuko Maalum wa Kufidia Bei za Mazao.

Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba na Novemba 2012, niliongoza Mikutano mikubwa iliyolenga kuwaleta pamoja Watunga Sera, Washirika wa Maendeleo na Wawekezaji ili kujadili fursa na changamoto mbalimbali za Sekta ya Kilimo. Katika mikutano hiyo, Wadau waliandaa na kukubaliana Mpango Kazi ulioainisha majukumu

yatakayotekelawa na kila mdau ili kuongeza uwekezaji katika Ukanda wa *SAGCOT*. Majukumu ya Serikali ni pamoja na upimaji ardhi kwa ajili ya kilimo, ujenzi wa miundombinu ya msingi na kuondoa vikwazo vinavyokwamisha uwekezaji katika Sekta ya Kilimo. Serikali imechukua hatua kwa kuainisha na kuweka mipaka ya ardhi kwa kuanzia na Wilaya za Kilombero, Ulanga na Rufiji. Zoezi hilo la kuainisha ardhi limelenga kutoa kipaumbele cha kwanza katika upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya Wakulima Wadogo. Hadi sasa ardhi ya vijiji 100 katika Wilaya ya Kilombero imepimwa.

Mheshimiwa Spika, Wawekezaji wengi wa ndani na nje ya Nchi wameonesha mwamko mkubwa wa kuwekeza katika Ukanda wa *SAGCOT*. Msisitizo wa Serikali ni kwamba, kila Mwekezaji Mkubwa atakayewekeza atalazimika kuwa na mpango wa kuendeleza na kushirikiana na Wakulima Wadogo. Hatua hiyo itamsaidia Mkulima Mdogo kupata teknolojia mpya, uhakika wa pembejeo, miundombinu ya umwagiliaji pamoja na soko la uhakika. Tayari utaratibu wa namna hiyo umeanza kuonesha matokeo mazuri Wilayani Kilombero.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Washirika wa Maendeleo ambao ni Shirika la Maendeleo la Marekani, Umoja wa Ulaya na Shirika la Maendeleo la Uingereza, wamekubali kusaidia ujenzi wa barabara yenye urefu wa Kilometra 103 kwa kiwango cha lami, ambayo itaunganisha Mikumi na Ifakara katika Bonde la Kilombero. Hatua za awali za ujenzi wa barabara hiyo zimeanza. Kukamilika kwa barabara hiyo muhimu kutafungua fursa zaidi za uwekezaji na kurahisisha usafiri na usafirishaji wa mazao ya Wakulima. Nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati Washirika wetu hao wa Maendeleo kwa kukubali kusaidia utekelezaji wa Mradi huo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuendeleza miundombinu ya masoko ya mazao kama moja ya mkakati madhubuti wa kumrahisishia Mkulima kufikisha mazao yake sokoni na kuongeza bei ya mazao hayo. Chini ya Programu ya Miundombinu ya Masoko, Uongezaji Thamani

na Huduma za Kifedha Vijijiini, Serikali imekamilisha usanifu na kutangaza zabuni za ujenzi wa barabara zenyе jumla ya Kilometra 210.8 katika Halmashauri za Mbulu, Njombe, Iringa Vijijiini, Kahama, Lushoto, Rufiji, Songea Vijijiini na Singida Vijijiini. Aidha, zabuni kwa ajili ya ujenzi wa maghala mawili katika Halmashauri za Wilaya ya Iringa Vijijiini na Njombe zimetangazwa na taratibu za ujenzi wa ghala katika Halmashauri ya Mbulu zinakamilishwa. Katika mwaka 2013/2014, Serikali itaendelea na ujenzi wa barabara na miundombinu mingine ya masoko Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Serikali imeanza kutekeleza Programu ya Miaka Mitano ya Kuendeleza Sekta ya Mifugo (2011/2012 – 2015/2016). Programu hiyo inalenga kuwa na Sekta ya Mifugo ya kisasa itakayoongeza ukuaji wa Sekta kutoka asilimia 2.3 hadi 4.5 kwa mwaka ifikapo mwaka 2016. Ili kufikia malengo hayo, Serikali pamoja na mambo mengine, imezielekeza Halmashauri zote nchini kufanya tathmini ya uwezo wa ardhi katika maeneo yao ili kufuga kulingana na uwezo wa eneo liliopo.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeboresha huduma za uhamilishaji pamoja na kutoa Ruzuku ya Dawa za Kuogesha Mifugo lita 92,323 zenyе thamani ya Shilingi Bilioni 1.5 ambazo zimesambazwa katika Mikoa yote ya Tanzania Bara. Hatua hiyo imekwenda sambamba na kujenga majosho mapya 14 na kukarabati majosho 20 katika Mikoa ya Arusha, Iringa, Kagera, Lindi, Mara, Mbeya, Mwanza, Katavi, Rukwa, Ruvuma, Simiyu, Singida, Geita na Tanga. Vilevile, Serikali imetoa mafunzo ya unenepeshaji mifugo kwa Wafugaji wanaozunguka Ranchi za Taifa. Pia, Miradi 13 ya unenepeshaji mifugo imeibuliwa kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya katika Mikoa ya Arusha, Dodoma, Manyara, Mwanza, Shinyanga na Singida. Hatua hiyo imeongeza idadi ya Ng'ombe walionenepeshwa kutoka 132,246 mwaka 2011 hadi ng'ombe 150,000 mwaka 2012. Aidha, vijiji 781 vya Halmashauri za Wilaya 80 katika Mikoa ya Iringa, Mbeya, Morogoro, Pwani, Katavi, Rukwa, Ruvuma na

Singida vimepimwa ili kuepusha migogoro ya mara kwa mara kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Serikali itaendelea kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Mifugo ili itoe mchango mkubwa zaidi katika uchumi. Aidha, itakamilisha ujenzi wa Mfumo wa Utambuzi na Ufutiliaji Mifugo ambao unatarajiwa kuanza kazi mwezi Agosti, 2013. Vilevile, itaimarisha uhamilishaji nchini kwa kuzalisha dozi za mbegu bora za uhamilishaji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Serikali imeanza kupitia Sera ya Taifa ya Uvuvi ya mwaka 1997 na kuandaa mkakati wa utekelezaji. Lengo ni kuihuisha Sera hiyo ili iendane na mabadiliko ya kiuchumi na kijamii yaliyojitozea pamoja na kuzingatia maendeleo ya Sayansi na Teknolojia katika Sekta ya Uvuvi. Katika mwaka 2013/2014, Serikali itakamilisha kupitia Sera ya Taifa ya Uvuvi ya mwaka 1997 na kuendelea kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi. Aidha, Vikundi vya Ulinzi Shirikishi vya Kudhibiti Uvuvi Haramu na Vituo vya Doria vitaimarishwa. Serikali pia itaendelea kusimamia shughuli za ukuzaji wa viumbwe kwenye maji ikiwa ni pamoja na kuanzisha vituo vipyta vya kuzalisha vifaranga vya samaki.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa asali na nta kwa miaka ya hivi karibuni unatupa moyo kwamba, ufungaji wa nyuki unaweza kuwa ni shughuli ya kiuchumi inayoweza kuwaongezea Wananchi wetu kipato na kuwaondolea umaskini. Katika kipindi cha miaka minne iliyopita (2009 - 2012), uzalishaji wa asali ulifikia wastani wa Tani 8,747 na nta Tani 583. Katika juhudzi za kuongeza uzalishaji, Serikali imetoa elimu ya ufungaji nyuki katika Wilaya za Kahama (Vijiji 7), Chunya (Vijiji 4), Same (Vijiji 2), Manyoni (Vijiji 3), Singida (Vijiji 2) na Kibondo (Vijiji 13). Aidha, Mizinga 500 imesambazwa katika Wilaya za Ruangwa, Mtwara, Newala, Tunduru na Namtumbo ambapo kila Wilaya ilipata Mizinga 100. Pamoja na juhudzi hizo, Hekta 56,290 zimepimwa kwa ajili ya kutenga hifadhi za nyuki katika vijiji mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa Sekta

Ndogo ya Ufugaji Nyuki kwa maendeleo ya Wananchi, niliahidi kwamba, yatafanyika Maonesho Maalum ya Ufugaji Nyuki. Maonesho hayo yamefanyika Kitaifa Jijini Dar es Salaam, kuanzia tarehe 4 - 7 Oktoba, 2012 katika Viwanja vya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambapo yalitanguliwa na Kongamano lillifanyika tarehe 3 Oktoba, 2012. Kaulimbiu ya Maonesho ilikuwa ni "ASALI KWA AFYA NA USTAWI". Maonesho hayo yameleta chachu na matumaini makubwa ya kukua kwa biashara ya mazao ya nyuki kwani tangu kumalizika, wafugaji nyuki wa Tanzania wamepata soko la kuza zaidi ya Tani 100 za asali nchini Ujerumani. Aidha, Wajasiriamali wengi wamepata Alama ya Utambulisho wa Biashara (*Barcode*) kwa ajili ya kutambulisha asali yao. Vilevile, kutokana na Wananchi kuhamasika kufuga nyuki, Serikali imeanza kutengeneza mizinga bora ipatayo 70,000, kuiwekea chambo na kuisambaza kwa Wananchi kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa Sekta ya Nyuki, kwa mara ya kwanza Tanzania iliadhimisha Siku ya Kitaifa ya Kutundika Mizinga, tarehe 4 Machi, 2013 katika Hifadhi ya Aghondi iliyopo Wilayani Manyoni Mkoa wa Singida. Katika uzinduzi huo, wadau walipata nafasi ya kutambua fursa kubwa zilizopo katika Sekta hiyo na kujenga mahusiano ya karibu ya kibiashara. Katika mwaka 2013/2014, Serikali itafanya mapitio ya Sera ya Ufugaji Nyuki ya Mwaka 1998 ili iendane na mabadiliko yanayotokea. Aidha, mafunzo na vifaa kwa ajili ya ufugaji nyuki yatatolewa kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa asali na nta.

Mheshimiwa Spika, mchango wa Sekta ya Viwanda kwenye Pato la Taifa uliongezeka na kufikia asilimia 9.7 mwaka 2012 ikilinganishwa na asilimia 9.0 mwaka 2011. Viwanda vinavyoendelea vizuri katika uzalishaji na kutoa mchango mkubwa ni pamoja na viwanda vya saruji, bia, unga wa ngano, vinywaji baridi, sukari, rangi, nyaya za umeme na usindikaji wa ngozi. Kwa upande wa *SIDO*, jumla ya Wajasiriamali 4,766 wamepatiwa mafunzo mbalimbali ya kukuza ujuzi wao hususan katika usindikaji wa mafuta ya kupikia, ngozi, ubanguaji wa korosho pamoja na kuhifadhi

na kusindika vyakula vya aina mbalimbali. Aidha, *SIDO* ilitoa huduma za ugani kwa Wajasiriamali 6,779 ili kuboresha shughuli za uzalishaji. Katika mwaka 2013/2014, Serikali itaendelea kubuni mikakati mipyä yenye lengo la kuendeleza na kuviwezesha viwanda vidogo na vya kati vya wajasiriamali wa ndani pamoja na kuweka mazingira wezeshi ya ukuaji wa viwanda nchini.

Mheshimiwa Spika, ili kuhamasisha usindikaji wa ngozi hapa nchini na kuongeza thamani ya Zao la Ngozi, mwezi Julai, 2012, Serikali iliongeza ushuru wa ngozi ghafi zinazouzwa nje ya Nchi kutoka asilimia 40 hadi 90 kwa kilo. Kutokana na hatua hiyo, ngozi zinazosindikwa Nchini zimeongezeka kutoka vipande vya ngozi za Ng'ombe 166,773 na vipande vya ngozi za Mbuzi na Kondoo 778,023 kipindi cha Januari - Juni, 2012 hadi vipande vya ngozi za Ng'ombe 343,860 na vipande vya ngozi za mbuzi na kondoo 1,173,875 kipindi cha Julai - Desemba, 2012. Ongezeko hilo linathibitisha kwamba hatua zilizochukuliwa na Serikali zimeongeza usindikaji wa ngozi na kupanua wigo wa uzalishaji wa mazao ya ngozi nchini. Serikali itaendelea kusimamia mafanikio hayo na kuchukua hatua zaidi zitakazoongeza usindikaji wa ngozi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa Mpango Mkakati wa kuifanya Mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Mtwara na Tanga kuwa Vituo vya Utalii wa Fukwe. Mikoa hiyo ina fukwe za kipekee zinazovutia Watalii na pia zinatafaa kwa uwekezaji wa kitalii. Vilevile, Serikali imevitangaza Vivutio vya Utalii katika soko la ndani na nje ya nchi kupitia Vyombo vya Habari na Maonesho ya Ndani na Kimataifa. Kutokana na hatua hiyo, idadi ya Watalii walioingia nchini mwaka 2012 iméongezeka na kufikia watalii 930,753 ikilinganishwa na watalii 867,994 mwaka 2011. Aidha, mapato yatokanayo na utalii yameongezeka kutoka Shilingi Bilioni 2,119 mwaka 2011 hadi Shilingi Bilioni 2,183 mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, matunda ya juhudzi za kutangaza vivutio vya utalii na pia kuhamasisha utalii wa ndani yamedhihirika baada ya Taasisi ya *The Seven Natural Wonders*, yenye makao yake nchini Marekani, kuijumuisha

Tanzania katika zoezi la kutafuta Maajabu Saba ya Asili katika Bara la Afrika. Zoezi hilo liliishirikisha Wataalam wengi Duniani na kupigwa kura na watu kutoka sehemu mbalimbali, wakiwemo Watanzania kwa kutumia tovuti. Matokeo ya zoezi hilo yalitangazwa tarehe 11 Februari, 2013, Jijini Arusha, ambapo Tanzania iliibuka mshindi kwa vivutio vitatu vya Maajabu Saba ya Asili ya Afrika yakijumuisha Mlima Kilimanjaro, Ngorongoro Crater na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti.

Napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Watanzania wote wa ndani na nje ya nchi, walioshiriki kupiga kura na hatimaye kutuwezesha kupata ushindi huo. Aidha, namshukuru Dkt. Philip Imler, ambaye ni Mwanzilishi wa Taasisi ya *The Seven Natural Wonders*, aliyesimamia zoezi hilo. Pia, nayashukuru Makampuni yote yaliyofadhili mashindano hayo na kutangaza vivutio vya Tanzania Barani Afrika na Duniani kote. Natoa wito kwa Watanzania wote kuhakikisha kwamba tunavilinda, tunavitunza na kuviendaole vivutio hivyo kwa manufaa ya Taifa letu. Tutumie pia ushindi huo kutangaza zaidi utalii wetu ili rasilimali hizi nzuri tulizo nazo ziendelee kuvutia watalii wengi na kuongeza mapato yetu.

Mheshimiwa Spika, Wachimbaji Wadogo wa Madini wana mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa nchi yetu. Ili kuwaendeleza wachimbaji hao, Serikali imekamilisha Mkakati, Mpango Kazi na Programu ya Mafunzo pamoja na kuwatengea maeneo wachimbaji wadogo kwa mujibu wa sheria. Maeneo hayo ni Mpambaa (Singida), Kilindi (Tanga), Dete na Melela (Morogoro), Winza (Dodoma), Songwe (Mbeya), Nyakunguru (Mara), Nyamilonge na Ilagala (Kigoma), Mihamna (Katavi), Mwajanga (Manyara), Makanya (Kilimanjaro) na Mbesa (Ruvuma). Aidha, Serikali imekusanya takwimu na taarifa muhimu za Wachimbaji Wadogo kote nchini kwa lengo la kuwatambua, kufahamu changamoto walizonazo na kujenga kanzidata (*database*).

Mheshimiwa Spika, Tanzania imekuwa mwanachama kamili wa Mpango wa Kimataifa Unaohimiza Uwazi katika Sekta ya Madini (*Extractive Industries Transparency Initiatives*-

EITI) baada ya kutimiza vigezo vilivyowekwa kimataifa katika Sekta ya Madini. Hatua hiyo imeiwezesha Tanzania kuwa na mfumo thabit wa utoaji taarifa za malipo na mapato kutoka katika kampuni zinazojishughulisha na uchimbaji wa madini, gesi asilia na mafuta, ambao unamwezesha mwananchi kufahamu na kujadili mchango wa Kampuni hizo katika Pato la Taifa. Katika mwaka 2013/2014, Serikali itaimarisha ukaguzi kwenye uzalishaji na biashara ya madini pamoja na kuimarisha *STAMICO* ili itekeleze majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuongeza fursa za ajira kwa Vijana wengi wanaoingia kwenye soko la ajira kila mwaka. Kwa mujibu wa matokeo ya Utafiti wa Ajira na Kipato Nchini wa mwaka 2010/2011, ajira ziliongezeka kutoka 1,276,982 mwaka 2010 hadi ajira 1,362,559 mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 6.7. Ili kuongeza kasi ya ukuaji wa ajira, Serikali inakamilisha Programu ya Kitaifa ya Kukuza Ajira kwa Vijana. Programu hiyo ya miaka mitatu itaongeza fursa za Vijana 301,100 kuweza kujajiri au kuajiriwa. Msukumo zaidi utawekwa katika Miradi ya Kilimo, Viwanda Vidogo, Maeneo Maalum ya Kiuchumi (*EPZ* na *SEZ*), Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Sambamba na hatua hiyo, Serikali itaendelea kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa Wanafunzi wa Vyuo vya Ufundji na vya Elimu ya Juu ili kuwawezesha kujajiri baada ya kuhitimu mafunzo yao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nchi yetu kuwa na ardhi ya kutosha na inayofaa kwa kilimo na uwekezaji mwingine, bado hatujakamilisha zoezi la uwekaji mipaka, kupima na kutoa hati kwa matumizi mbalimbali. Hali hiyo inachangia migogoro ya ardhi na kukwamisha uwekezaji kwa kiasi kikubwa. Serikali imechukua hatua muhimu kwa kutumia teknolojia ya kisasa itakayoharakisha zoezi la upimaji ardhi. Katika kutekeleza kazi hiyo, awamu ya kwanza ya usimikaji wa Mtandao wa Alama za Msingi za Upimaji Ardhi Nchini (*Geodetic Control Network*) imekamilika. Mikoa iliyohusika ni Pwani, Morogoro, Mara, Mwanza, Kagera, Shinyanga, Lindi, Tabora na Dodoma. Tayari majoribio ya matumizi ya alama hizo yamefanyika katika Wilaya za Ngorongoro na Kilombero na kudhihirisha kuwa gharama na muda wa kupima ardhi

zimepungua. Awamu ya Pili ya Usimikaji wa Alama hizo utaendelea katika Mikoa iliyobaki na kuanza upimaji wa viwanja na mashamba kwa kutumia utaratibu mpya wa upimaji wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, ili kuwa na mfumo endelevu wa utunzaji wa kumbukumbu za ardhi, Serikali imeanza ujenzi wa Mfumo Uganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi. Mfumo huo utakaounganisha Ofisi za Ardhi nchini unategemewa kukamilika mwaka 2014 na utaiwezesha Tanzania kuwa na kumbukumbu sahihi za ardhi. Vilevile, utaharakisha na kurahisisha utoaji wa maamuzi, upimaji na utoaji wa Hati Miliki na hivyo kupunguza migogoro ya ardhi. Katika mwaka 2013/2014, Serikali itaendelea na ujenzi wa Mfumo Uganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi na kurahisisha upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kusogeza huduma ya nishati ya umeme karibu na Wananchi ili kuharakisha maendeleo yao. Katika kutekeleza azma hiyo, gharama za kuunganisha umeme vijijini na mijini zimepunguza kwa kati ya asilimia 30 na 77. Kwa mfano, gharama za kuunganisha umeme wa njia moja kwa umbali wa meta 30 kwa wateja wadogo wa vijijini zimepungua kutoka shilingi 385,682 hadi 150,000 na mijini kutoka shilingi 385,682 hadi 272,000 bila kodi. Hatua hiyo imeweza Wananchi wengi kumudu gharama ya kuunganisha umeme na kuongeza kasi ya usambazaji umeme nchini. Serikali pia, imefikisha umeme katika Makao Makuu ya Wilaya za Nkasi na Namtumbo, hivyo kufanya idadi ya Makao Makuu ya Wilaya zenye umeme kuwa 117, sawa na asilimia 88 ya Wilaya zote Nchini.

Vilevile, Serikali inatekeleza Programu Kabambe ya Kusambaza Umeme Vijijini ambapo wateja 8,046 wamelipiwa gharama za kuunganishiwa umeme kuititia Mfuko wa Nishati Vijijini. Aidha, kazi ya kusambaza na kuboresha miundombinu ya umeme katika Mikoa ya Mtwara na Lindi inaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Spika, Sekta ndogo ya Gesi Asilia inakua kwa kasi ambapo hadi kufikia Januari, 2013, kiasi cha futi za ujazo Trilioni 35 zimegundulika nchini. Ili kusimamia rasilimali hiyo muhimu, Serikali imeandaa rasimu ya Sera ya Gesi Asilia na kupata maoni kutoka kwa Wadau mbalimbali. Aidha, tarehe 8 Novemba, 2012, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alizindua Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Gesi Asilia kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam. Mradi huo utaongeza uzalishaji wa umeme na kupunguza gharama za umeme nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Serikali itaendelea na ujenzi wa mradi wa bomba la gesi asilia kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam na ujenzi wa Mitambo ya kuzalisha umeme wa Kinyerezi (MW 200). Vilevile, itaanza kutekeleza Awamu ya Pili ya Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini na kufikisha umeme wa gridi kwenye Makao Makuu ya Wilaya zisizokuwa na umeme.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza Mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa wenye Awamu Tano. Awamu ya Kwanza na ya Pili ya Ujenzi wa Mkongo huo wenye urefu wa Kilomita 7,560 imekamilika na kuunganisha Makao Makuu ya Mikoa 24 ya Tanzania Bara. Kazi ya kuunganisha Kisiwa cha Unguja na Mkongo huo kuititia Dar es Salaam itakamilika mwaka 2013. Tayari Makampuni ya Simu na Mawasiliano ya hapa nchini yameunganishwa kwenye Mkongo, hatua ambayo imewezesha upatikanaji wa huduma bora za mawasiliano katika eneo kubwa zaidi na kwa gharama nafuu. Sambamba na hatua hiyo, Serikali imeanza ujenzi wa Mfumo wa Kuratibu Huduma za Mawasiliano Nchini (*Traffic Monitoring System*). Mfumo huo utasaidia kuhakikisha mapato yanayotokana na huduma katika Sekta ya Mawasiliano yanajulikana ili makampuni ya mawasiliano nchini yalipe kodi stahiki kwa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania pamoja na nchi zote Duniani kuititia Umoja wa Mawasiliano Duniani (*ITU*), zimekubaliana kusitisha matumizi ya teknolojia ya utangazaji

kutoka Mfumo wa Analojia na kuanza Matumizi ya Teknolojia ya Dijitali ifikapo Juni, 2015. Hapa nchini, usitishaji wa matumizi ya mfumo wa mitambo ya analojia umeanza kutekelezwa tarehe 31 Desemba, 2012 kwa awamu kwa kuanzia na Jiji la Dar es Salaam na kufuatiwa na Mikoa ya Dodoma, Tanga na Mwanza. Matangazo ya analojia yataendelea kusitishwa katika mikoa mingine nchini kulingana na ratiba iliyowekwa. Natambua kwamba, kuna changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa zoezi hilo la mabadiliko. Hata hivyo, mabadiliko hayo yanalenga kuimarisha mawasiliano na kuiwezesha nchi yetu kuendana na hali halisi ya mabadiliko ya teknolojia Duniani. Katika mazingira ya sasa, sisi kama Taifa siyo vyema kubaki kama kisiwa wakati tumeunganishwa na mifumo ya teknolojia ya kidunia.

Hivyo, ni busara tuendelee na mabadiliko hayo sasa kuliko kusubiri na hatimaye tukajikuta tuko nyuma na nje ya mstari. Natoa wito kwa Watanzania wote kuyaona mabadiliko hayo kwa mtazamo chanya na kuyakubali kama hatua kubwa sana ya maendeleo ya teknolojia nchini. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya jitihada kubwa za kuendeleza Sayansi na Teknolojia kama njia ya kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi. Jitihada hizo ni pamoja na kutenga fedha za kutosha kila mwaka kwa ajili ya utafiti na maendeleo ya kisayansi. Serikali pia, imekamilisha ujenzi wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela iliyopo mkoani Arusha, ambayo ilizinduliwa rasmi tarehe 2 Novemba, 2012. Kukamiliika kwa ujenzi wa Taasisi hiyo kumeongeza udahili wa wanafunzi wa Shahada ya Uzamili na Uzamivu kutoka wanafunzi 83 mwaka 2011/2012 hadi wanafunzi 135 mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Serikali itaendelea kueneza Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kupanua matumizi yake katika maeneo mbalimbali Nchini na nchi jirani. Vilevile, Serikali itaendelea na zoezi la kuhama kutoka katika mfumo wa analojia kwenda dijitali na kupanua

na kuboresha Mtandao wa Huduma za Mawasiliano ya simu na intaneti Nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imewekeza kwa kiwango kikubwa katika kujenga, kukarabati na kuboresha mtandao wa Barabara Kuu za Mikoa, Wilaya pamoja na za Vijijini ili zипитике wakati wote wa mwaka. Lengo ni kuwa na mtandao bora wa barabara utakaowezesha Wananchi, hasa Wakulima, kusafirisha mazao yao hadi kwenye masoko ya ndani na nje ya nchi. Katika mwaka 2012/2013, Serikali imejenga jumla ya Kilometra 294.4 za kiwango cha lami katika barabara kuu na za mikoa na kukarabati kwa kiwango cha lami jumla ya Kilometra 111.8 katika barabara hizo. Aidha, kazi za ujenzi na ukarabati wa barabara kuu na za mikoa zenye urefu wa Kilometra 179 kwa kiwango cha lami unaendelea katika maeneo mbalimbali Nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Nne imedhamiria kujenga na kukamilisha ujenzi wa madaraja makubwa na ya kisasa mawili ambayo ni Daraja la Mto Malagarasi na Daraja la Kigamboni. Ujenzi wa Daraja la Mto Malagarasi unaojumuisha ujenzi wa Daraja kubwa lenye urefu wa Meta 200 na Madaraja mengine madogo katika Bonde la Mto Malagarasi unaendelea vizuri. Hadi mwezi Machi, 2013, Mkandarasi amekamilisha ujenzi kwa asilimia 85. Sambamba na hatua hiyo, taratibu zimekamilika za kupata mkopo wa nyongeza kutoka Mfuko wa Ushirikiano wa Maendeleo ya Kiuchumi wa Korea kwa ajili ya ujenzi wa barabara kiungo za daraja hilo zenye urefu wa Kilometra 37 kwa kiwango cha lami. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Daraja la Kigamboni lenye urefu wa Meta 680 linalojengwa kuunganisha eneo la Kurasini na Kigamboni katika Bahari ya Hindi, tayari Mkandarasi amekamilisha kazi za maandalizi kwa asilimia 90. Kazi ya ujenzi wa Daraja la Kudumu na Barabara zake inatarajiwa kuanza wakati wowote kuanzia sasa. Daraja hili linajengwa kwa Ubia kati ya Serikali na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*). Lengo ni kukamilisha ujenzi wa daraja hilo mwanzoni mwa mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Serikali itajenga Barabara Kuu kwa kiwango cha lami zenyе urefu wa Kilometa 495 na kukarabati Barabara zenyе urefu wa Kilometa 190 na Madaraja 11. Serikali pia, itajenga barabara za Mikoa za lami zenyе urefu wa Kilometa 54.3 na kukarabati Kilometa 855 kwa kiwango cha changarawe na Madaraja 36. Aidha, matengenezo ya kawaida na matengenezo ya muda maalum ya Barabara Kuu na za Mikoa yataendelea kufanyika katika kipindi kijacho.

Mheshimiwa Spika, Usafiri wa Barabara katika Jiji la Dar es Salaam: Msongamano wa magari katika barabara za Jiji la Dar es Salaam ni moja ya changamoto ambayo Serikali inaendelea kuifanyia kazi. Jitihada zinazofanyika kupunguza msongamano wa magari barabarani ni pamoja na kujenga miundombinu zaidi ya barabara mpya za kuingia na kutoka katikati ya Jiji; kuanzisha usafiri wa Treni ya Abiria; kuharakisha utekelezaji wa Mradi wa Mabasi yaendayo Haraka (*DART*); na kuimarisha usimamizi wa Sheria za Usalama Barabarani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa barabara mpya za kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam, hadi Machi, 2013 ujenzi wa Barabara ya kiwango cha lami yenye urefu wa Kilometa 6.4 kutoka Kituo Kikuu cha Mabasi Ubungo - Kigogo hadi mzunguko wa barabara ya Kawawa imekamilika na barabara yenye urefu wa Kilometa 2.7 kutoka Barabara ya Kawawa – Bonde la Msimbazi hadi Makutano ya Jangwani na Twiga imekamilika kwa asilimia 70. Aidha, ujenzi wa Barabara yenye urefu wa Kilometa 10.3 kutoka Jet Corner - Vituka hadi Davis Corner imekamilika kwa asilimia 90. Vilevile, utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka unaendelea ambapo kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa Barabara za *DART* na za magari mchanganyiko na baiskeli katika Barabara ya Morogoro na ujenzi wa Miundombinu ya Mifumo ya Maji, Vituo vya Mabasi na Madaraja. Katika mwaka 2013/2014, Serikali itaendelea na ujenzi wa barabara nyingine za kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam pamoja na ujenzi wa miundombinu ya *DART*.

Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba 2012, Serikali ilianzisha huduma ya usafiri wa treni ya abiria Jijini Dar es Salaam kuitia Kampuni ya Reli (*TRL*) na *TAZARA*, kwa lengo la kukabiliana na tatizo la msongamano wa magari na abiria. Wastani wa idadi ya Abiria wanaosafiri kwa treni ya *TAZARA* ni abiria 4,500 kwa siku na *TRL* ni abiria 5,000. Takwimu zinaonesha kuwa, abiria 9,500 wanaosafiri kila siku kwa njia ya treni wangehitaji kutumia mabasi zaidi ya 380 yenyewe uwezo wa kubeba abiria 25 kila moja.

Kwa ujumla, mwitikio wa Wananchi wa kutumia huduma ya treni ya abiria ni mkubwa ikilinganishwa na uwezo wa kutoa huduma hiyo. Kwa kuzingatia mahitaji hayo makubwa, Serikali imeunda Kamati Maalum ya Wadau wa usafiri Jijini Dar es Salaam kwa lengo la kuchambua, kuainisha na kushauri mipango na mikakati ya baadaye ya kuboresha huduma hiyo illi iwe endelevu na salama. Ni mategemeo yangu kwamba, Kamati hiyo itaandaa Mpango mzuri zaidi wa kupanua huduma hiyo muhimu kwa Jiji la Dar es Salaam ambalo kwa mujibu wa Takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012 lina idadi ya watu Milioni 4.36, sawa na asilimia 10 ya Wakazi wote wa Tanzania Bara. Ongezeko hilo ni kubwa na hivyo linahitaji mpango kabambe wa usafiri na usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya Reli ya Kati kwa kujenga na kukarabati maeneo mbalimbali illi kuiwezesha kuitika wakati wote. Pamoja na ukarabati huo, usanifu wa kina wa mradi wa uendelezaji na ujenzi wa reli kutoka Dar es Salaam - Isaka - Keza - Kigali na Keza - Musongati kwa kiwango cha Kimataifa umekamilika mwezi Februari mwaka 2013. Serikali pia, imekamilisha mchakato wa kumpata Mshauri Mwelekezi atakayefanya upembuzi yakinifu wa kuinua kiwango cha reli kuwa katika kiwango cha kimataifa kutoka Tabora hadi Kigoma, Kaliua hadi Mpanda na Isaka hadi Mwanza. Lengo ni kuwezesha reli hiyo ifanane na inayotarajiwa kujengwa kutoka Dar es Salaam - Isaka - Kigali/Musongati. Upembuzi yakinifu wa reli ya kutoka Dar es Salaam hadi Rwanda na Burundi na kutoka Arusha hadi Musoma unatarajiwa kuanza mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba, mwezi Machi, 2012, Serikali ya Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China zilitia saini Itifaki ya 15 ya Kuboresha Reli ya TAZARA. Tayari Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China imetoa jumla ya Shilingi Bilioni 38.2 kwa ajili ya kutekeleza Miradi iliyo chini ya Itifaki hiyo, ambayo inajumuisha kufanya upembuzi yakinifu wa kuboresha reli hiyo, kukarabati njia ya reli, kununua vichwa vipyta vya treni na kukarabati mabehewa ya abiria. Hatua hizi zikikamilika zitaboresha kwa kiwango kikubwa usafiri wa Reli ya TAZARA.

Mheshimiwa Spika, Serikali inachukua hatua mbalimbali za kuongeza uwezo na ufanisi wa bandari zake kwa kutekeleza Mpango Kabambe wa Mamlaka ya Bandari. Baadhi ya Miradi inayotekelawa chini ya mpango huo ni upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuimarisha na kuongeza kina cha maji katika Gati Namba 1 hadi 7 katika Bandari ya Dar es Salaam na kuanza Awamu ya Pili ya Mradi wa Ujenzi wa Matanki ya Kuhifadhia Mafuta. Mradi mwingine ni kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa kituo kikubwa cha kuhifadhia mizigo ya kwenda nchi jirani katika eneo la Kisarawe.

Mheshimiwa Spika, kutokana na nafasi ya nchi yetu kijigrafia na ongezeko kubwa la biashara na uingizaji wa mizigo ya hapa nchini na nchi jirani ambazo hazina bandari, uwezo wa Bandari ya Dar es Salaam kuhimili ongezeko hilo unapungua. Pamoja na jitihada zinazoendelea za kupanua miundombinu ya bandari hiyo, Serikali imeona umuhimu wa kuwa na Bandari mpya ya Bagamoyo ili isaidiane na Bandari zilizopo kukabiliana na ongezeko hilo.

Mheshimiwa Spika, tarehe 24 Machi, 2013, Serikali ya Tanzania na China zimetia saini makubaliano ya kujenga bandari mpya ya Bagamoyo ambayo itakuwa kubwa kuliko zote katika Ukanda wa Nchi za Afrika Mashariki na Kati. Makubaliano hayo yanajumuisha pia ujenzi wa eneo huru la biashara na miundombinu mingine muhimu ikiwemo reli itakayounganisha Bandari ya Bagamoyo na Reli ya Kati na ya TAZARA pamoja na barabara ya lami kutoka Bagamoyo

hadi Mlandizi. Huu ni Mradi mkubwa na wa kimkakati ambao utabadili kabisa mfumo wa uendeshaji wa Bandari na usafirishaji Nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imetekeleza kwa mafanikio Awamu ya Kwanza ya Uboreshaji na Upanuzi wa Viwanja vya Ndege vya Tabora, Kigoma na Bukoba. Ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege kwa kiwango cha lami katika Kiwanja cha Ndege cha Tabora umekamilika na kazi za ujenzi zinazoendelea katika Kiwanja cha Kigoma zinatarajiwा kukamilika mwezi Juni, 2013. Kwa upande wa Kiwanja cha Ndege cha Bukoba, ukarabati wa njia ya kuruka na kutua ndege kwa kiwango cha lami unaendelea. Aidha, Kiwanja kipyā cha Kimataifa cha Songwe, Mbeya, kilianza kutoa huduma tarehe 13 Desemba, 2012. Kiwanja hicho ambacho kijirofia kipo karibu na Nchi za Zambia, Malawi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Nchi nyingine za Kusini mwa Afrika ni kichocheo muhimu cha shughuli za uchumi na kijamii zikiwemo utalii na kilimo hasa cha matunda, mbogamboga na maua kwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Ni muhimu sana Wananchi wa maeneo hayo na mengine wahamasishwe na kujipanga kutumia fursa za kiuchumi zitakazoambatana na kukamilika kwa kiwanja hicho.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Serikali itaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Upanuzi na Uboreshaji wa Viwanja vya Ndege. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa ukarabati kwa kiwango cha lami wa njia za kuruka na kutua ndege kwa Viwanja vya Iringa, Kilwa Masoko, Ziwa Manyara, Musoma, Mtwara, Njombe, Songea, Singida na Tanga.

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Sekta ya Elimu, Elimu ya Msingi; Serikali ilianza kutekeleza programu kubwa za kuendeleza elimu nchini mwaka 2001 kwa lengo la kuongeza idadi ya Wanafunzi wa rika lengwa wanaojunga na shule na kuboresha elimu. Utekelezaji wa Awamu ya Kwanza na ya Pili ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM I & II) umeleta mafanikio makubwa katika kuboresha miundombinu ya elimu, kuandikisha wanafunzi wa

rika lengwa na kupunguza pengo la uandikishaji kati ya wanafunzi wa kike na wa kiume. Mafanikio hayo yaliambatana na changamoto za upungufu wa walimu, vifaa vya kujifunzia na kufundishia pamoja na madawati. Kwa kutambua changamoto hizo, llani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 inaelekeza Serikali kulinda mafanikio yaliyopatikana pamoja na kuweka msisitizo mkubwa katika ubora wa elimu.

Mheshimiwa Spika, ili kuendeleza kasi tulioanza nayo, Serikali inatekeleza Awamu ya Tatu ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM III) unaolenga kuboresha elimu kwa kuongeza idadi ya walimu, vitabu vya ziada na kiada na vifaa vya kujifunzia *na kufundishia*. Jitihada za Serikali za kuajiri walimu zinaendelea ambapo walimu wapya 13,568 wameajiriwa katika Shule za Msingi mwaka 2012/2013. Serikali itaendelea kuweka msisitizo katika kuboresha Elimu ya Msingi nchini kwa kuzingatia manufaa makubwa yanayopatikana katika ngazi hiyo muhimu ya elimu.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Sekondari; mafanikio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi Nchini ambayo ni pamoja na kuongezeka kwa idadi ya wahitimu wanaofaulu ngazi hiyo, yameongeza mahitaji ya nafasi zaidi katika Shule za Sekondari. Kutokana na hali hiyo, Serikali ilianza kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES) mwaka 2006. Mpango huo umesaidia sana kukabiliana na changamoto ya nafasi zaidi katika shule za sekondari kwa kujenga shule nyingi za sekondari na hivyo kuwa na wanafunzi wengi zaidi. Ni dhahiri kuwa ongezeko hilo la Wanafunzi lilihitaji walimu wengi zaidi, maabara, vitabu na vifaa vingine muhimu. Aidha, Serikali iligatua usimamizi wa Shule za Sekondari kutoka Serikali Kuu kwenda katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuboresha usimamizi wa shule hizo pamoja na kuanzisha programu kabambe ya kufundisha walimu zaidi ili wafundishe katika shule zinazoongezeka.

Katika mwaka 2012/2013, Serikali imeajiri jumla ya

Walimu 12,969 ambao watafundisha katika shule mbalimbali za sekondari nchini. Hatua hizo zote ni uwekezaji mkubwa ambao matokeo yake yatawezesha kuboresha elimu nchini hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Spika, sote tumehuzunishwa sana na matokeo yasiyoridhisha ya Mtihani wa Kidato cha Nne kwa mwaka 2012. Matokeo hayo siyo tu kwamba yamewahuzunisha wazazi ambao wamewekeza rasilimali kwa watoto wao, bali pia Serikali ambayo imetumia rasilimali nydingi kwenye Sekta ya Elimu. Huu siyo wakati wa kulaumiana ama kutafuta mchawi wa matokeo hayo yasiyoridhisha. Lazima tutafute suluhisho, kusonga mbele na kubuni mikakati na hatua za haraka za kusaidia watoto hao ambao wamepata matokeo mabaya. Tumeanza kwa kuunda Tume yenyewe watu makini ambayo itachunguza chanzo cha matokeo hayo mabaya na kutoa mapendekezo ya namna ya kutatua tatizo hilo katika muda mfupi, kati na mrefu na pia kupendekeza suluhisho la haraka kwa wale waliopata Daraja la IV na sifuri. Napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwamba, matokeo ya Tume hiyo yatawekwa bayana na hatua zitakazopendekezwa zenyewe lengo la kuimarisha elimu Nchini zitachukuliwa. Hata hivyo, ni vyema tukumbuke kwamba, sote tuna wajibu wa kutoa mwongozo na mapendekezo yatakayosaidia kutoka hapa tulipo. Wazazi, Wanafunzi na Jamii nzima, wana nafasi yao pia katika kuboresha elimu ya nchi hii. Hili siyo suala la Serikali pekee.

Mheshimiwa Spika, Elimu Maalum; Serikali inaendelea kuweka msukumo wa kipekee katika kutoa elimu maalum kwa watu yenyewe ulemavu wakiwemo yenyewe ulemavu wa ngozi, uoni hafifu na usikivu. Katika mwaka 2012/2013, Serikali imeandaa mwongozo wa kufundishia wanafunzi yenyewe ulemavu wa ngozi na uoni hafifu. Aidha, Serikali imenunua na kusambaza vifaa maalum na visaidizi ya kufundishia na kujifunzia kuanzia ngazi ya Elimu ya Awali hadi Chuo Kikuu. Kazi nydingine zilizofanyika ni kukarabati na kujenga majengo rafiki kwa walemavu katika Chuo cha Ualimu Patandi. Katika mwaka 2013/2014, Serikali itaendelea kuboresha utoaji wa

Elimu Maalum hususan baada ya kupata takwimu sahihi za walemauvu kutokana na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Juu; Serikali inatekeleza Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Juu kwa kupanua na kuongeza Taasisi za Elimu ya Juu za Serikali na Binafsi. Katika kipindi takribani cha miaka minane, idadi ya wanafunzi wanaosoma Vyuo vya Elimu ya Juu nchini imeongezeka kutoka 40,993 mwaka 2005/2006 hadi 166,484 mwaka 2012/2013, sawa na ongezeko la asilimia 306. Serikali pia, inatoa mikopo kwa Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu vya Umma na vile vya Mashirika ya Dini na vya Sekta Binafsi. Katika mwaka 2012/2013, Serikali imetoa mikopo ya Shilingi Bilioni 345 kwa wanafunzi 98,772 ikilinganishwa na mikopo ya Shilingi Bilioni 291 kwa wanafunzi 93,784 mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Serikali itaendelea kuongeza kiasi cha fedha kwa ajili ya Mikopo ya Elimu ya Juu na kuimarisha usimamizi wa urejeshaji wa mikopo ili wanafunzi wengi zaidi waweze kunufaika. Nitumie fursa hii kuwakumbusha wale wote walionufaika na mikopo ya elimu ya juu kulipa mikopo hiyo yenye masharti nafuu sana ili wanafunzi zaidi waweze kunufaika nayo. Aidha, waajiri watimize wajibu wao kwa kuwataka waajiriwa walionufaika kulipa mikopo hiyo. Vilevile, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu iongeze kasi ya kukusanya madeni na kuchukua hatua stahiki kwa wale wasiolipa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Sekta ya Afya; Vituo vya Utoaji wa Huduma za Afya Nchini; Serikali imeweka jitihada kubwa za kuhakikisha kwamba Vituo vya Utoaji wa Huduma za Afya katika ngazi zote Nchini vinapatiwa dawa muhimu na vifaa vya Teknolojia ya kisasa vya kuchunguza na kutibu magonjwa. Katika mwaka 2012/2013, Serikali imenunua dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi na kuvisambaza kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali zote za Serikali nchini. Serikali pia, imeongeza uwezo wa ndani wa kutibu maradhi mbalimbali. Mathalani, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili imewezeshwa kutoa Huduma za Afya za

Ubingwa wa Juu, ikiwa ni pamoja na upasuaji wa moyo ambapo hadi sasa zaidi ya Wagonjwa 450 wamepatiwa huduma hiyo. Vilevile, huduma ya usafishaji damu kwa Wagonjwa wa Figo na Upasuaji kuititia tundu dogo pamoja na uchunguzi wa magonjwa kwa kutumia mashine za kisasa unafanyika hapa nchini. Hatua hiyo imewezesha Serikali na Wananchi kuokoa fedha nyingi zinazotumika kupeleka wagonjwa kutibiwa nje ya Nchi. Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza madaktari, wauguzi na wataalam wengine wa Afya kwa kuliwezesha Taifa letu kupiga hatua kubwa katika kutibu magonjwa hayo na mengine yanayohitaji utaalami na ubingwa wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeimarisha huduma ya tiba ya saratani nchini kwa kukamilisha ujenzi wa jengo la kulaza wagonjwa katika Hospitali ya Saratani ya *Ocean Road* na hivyo kuongeza uwezo wake kutoka vitanda 120 hadi 270. Aidha, Serikali imesogea huduma ya tiba ya saratani karibu na wananchi kwa kukamilisha ujenzi wa jengo maalum la kutoa huduma hiyo katika Hospitali ya Bugando. Hatua hiyo itapanua wigo wa kutoa huduma ya tiba ya saratani na kupunguza msongamano wa wagonjwa wa saratani kutoka mikoa mbalimbali waliokuwa wanalazimika kufuata huduma hiyo katika Hospitali ya Saratani ya *Ocean Road* Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012, Serikali ilifanya Utafiti kuhusu Viashiria vya UKIMWI na Malaria. Taarifa ya matokeo ya utafiti huo inaonesha kuwa kiwango cha Malaria nchini kwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano kimepungua kutoka asilimia 18 mwaka 2007 hadi asilimia tisa mwaka 2012. Hali hii imechangiwa zaidi na ongezeko kubwa la matumizi ya vyandarua viliviyowekwa viuatilifu vya muda mrefu, ambapo zaidi ya Vyandarua milioni 34 vimesambazwa katika Kaya zenye Watoto walio na umri chini ya miaka mitano na Wanawake Wajawazito. Kutokana na usambazaji huo, matumizi ya vyandarua yameongezeka kutoka asilimia 26 mwaka 2007 hadi asilimia 72 mwaka 2012 kwa Watoto wenye umri chini ya miaka mitano; kwa wanawake wajawazito, matumizi ya Vyandarua yameongezeka kutoka

asilimia 27 mwaka 2007 hadi asilimia 75 mwaka 2012. Ni dhahiri kupungua kwa kiwango cha malaria nchini ni jitihada za kipekee za Serikali ya Awamu ya Nne kwa kushirikiana na Wananchi na Washirika wa Maendeleo kuititia kampanye mbalimbali za kudhibiti malaria.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza wananchi na wadau wote walioshirikiana na Serikali katika kupata mafanikio haya ambayo yanatokana na utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria Nchini na Mpango wa Hati Punguzo kwa Wanawake Wajawazito ulioanza kutekelezwa mwaka 2008 hadi 2012. Natoa wito kwa Wananchi wote kuendeleza juhudhi za kujikinga na malaria, hususan kwa kutumia Vyandara vyenye Viuatilifu vya muda mrefu na kutokomeza mazalia ya mbu.

Mheshimiwa Spika, juhudhi za Serikali za kupambana na Ugonjwa wa UKIMWI nchini pia zimeanza kuzaa matunda. Kwa mujibu wa Utafiti wa Mwaka 2011 – 2012 wa Viashiria vya Malaria na UKIMWI, maambukizi ya Virusi vya UKIMWI yamepungua kutoka asilimia 5.7 mwaka 2007/2008 hadi asilimia 5.1 mwaka 2011/2012 kwa Wanawake na Wanaume wa umri wa miaka 15 – 49. Ili kuendelea kupunguza kasi ya maambukizi ya UKIMWI Nchini, Serikali inaendelea kutoa elimu ya UKIMWI; kutoa ushauri nasaha na kuhamasisha upimaji wa hiari. Katika mwaka 2013/2014, Serikali itaanza kutekeleza Mkakati Mpya wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI wa mwaka 2013 hadi 2017 unaolenga kuwa na sifuri tatu, yaani kutokuwa na maambukizi mapya; kukomesha vifo vitokanavyo na UKIMWI na kuondoa kabisa unyanyapaa na ubaguzi. Lengo hilo litatimia iwapo sote tutabadili tabia zinazosababisha maambukizi mapya.

Mheshimiwa Spika, Serikali inachukua hatua thabiti za kupambana na utapiamlo hususan udumavu unaoathiri watoto wenye umri chini ya miaka mitano. Katika hotuba yangu ya mwaka 2012/2013 nilieleza kwamba, Serikali imezindua Mkakati wa Kitaifa wa Lishe wa mwaka 2010/2011 hadi 2014/2015. Mkakati huo umeanza kutekelezwa kwa

kuandaliwa mpango wa utekelezaji ulioainisha gharama na majukumu ya kila mdau katika kupunguza Utapiamlo Nchini. Pamoja na mambo mengine, mpango huo umesisitiza umuhimu wa kutoa elimu kwa umma kuhusu lishe bora hasa kwa mama wajawazito na watoto wachanga, kuongeza viini lishe kwenye vyakula pamoja na kuingiza masuala ya lishe kwenye Sera na Mipango mbalimbali ya Serikali.

Tayari hatua zimechukuliwa ambapo masuala ya lishe yameingizwa kwenye Mpango wa Taifa wa Uwekezaji katika Kilimo na Chakula (*Tanzania Agriculture and Food Security Investment Plan - TAFSIP*). Vilevile, Serikali inaendelea na zoezi la kuhuisha Sera ya Usalama wa Chakula na Lishe ya Mwaka 1992 ili iendane na Mkakati wa Taifa wa Lishe wa mwaka 2010/2011 hadi 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, tunayo kazi kubwa mbele yetu ya kupambana na tatizo la lishe duni katika maeneo yote nchini. Takwimu zinabainisha kwamba, hakuna tofauti kubwa ya kiwango cha udumavu katika mikoa inayozalisha chakula kwa wingi na ile yenye uhaba wa chakula. Napenda kusisitiza tena kwamba, hali ya udumavu humtokea mtoto katika siku elfu moja za kwanza za uhai wake, yaani tangu kutungwa mimba hadi umri wa miaka miwili. Hivyo, tunahitaji kuimarisha utoaji elimu ya lishe kwa wajawazito na akina mama wanaonyonyesha ili wapate mlo kamili na kunyonyesha watoto wao kikamilifu hususan miezi sita ya mwanzo tangu kuzaliwa.

Natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge zaidi kujunga na Kikundi cha Wabunge kinachohamasisha umuhimu wa Lishe Bora ili kuongeza kasi na chachu ya kutoa elimu ya lishe katika maeneo yetu ya uwakilishi.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa maji ya uhakika na ya kutosha kwa Wananchi Vijijini bado ni changamoto inayohitaji nguvu zaidi na mbinu mpya kwa kuzingatia ongezeko kubwa la watu pamoja na mabadiliko ya Tabianchi. Katika kukabiliana na changamoto hizo, Serikali imetenga na kupima maeneo ya vyanzo vyta maji na

kuyawekea mipaka ili kuzuia uchafuzi na uharibifu wa vyanzo hivyo. Aidha, vituo mbalimbali vya kuchotea maji vimeainishwa katika Halmashauri 122 na kuwekwa kwenye ramani ili vifahamike. Ujenzi wa Miradi mipyä, upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya maji vijijini pia umefanyika katika maeneo mbalimbali ili kusogeza huduma ya maji karibu na Wananchi. Kutokana na juhudhi hizo, idadi ya wananchi wanaoishi vijijini ambao wanapata huduma ya majisafi, salama na ya kutosha karibu na makazi imeongezeka kutoka watu milioni 16.3 mwaka 2006 hadi milioni 20.6 mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, Huduma ya Maji Mijini inasimamiwa na kutekelezwa na Mamlaka 19 za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Miji Mikuu ya Mikoa, Mamlaka 109 katika ngazi za Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Maji ya Kitaifa. Serikali kupitia Mamlaka hizo, imeongeza kiwango cha upatikanaji wa maji kwa wakazi wa Miji hiyo kutoka asilimia 84 mwaka 2010/2011 hadi asilimia 86 mwaka 2011/2012. Katika Jiji la Dar es Salaam, Serikali inaboresha upatikanaji wa huduma ya maji kwa kupanua uwezo wa mtambo wa maji wa Ruvu Chini ambapo ujenzi umefikia asilimia 85. Kazi ya kulaza bomba kuu la pili lenye kipenyo cha Meta 1.8 na urefu wa km 55.5, kutoka Ruvu Chini hadi kwenye matanki ya kuhifadhi maji yaliyopo eneo la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, inatarajiwa kukamilika mwezi Februari, 2014. Aidha, kazi ya usanifu wa Mradi wa Kuchimba Visima Virefu 12 katika maeneo ya Kimbiji na Visima vinane katika eneo la Mpera imekamilika na Wananchi waliohamishwa wamelipwa fidia. Katika mwaka 2013/2014, Serikali itaendelea kukarabati na kujenga Miradi ya Maji Mijini na Vijijini pamoja na kujenga mabwawa kwa ajili ya matumizi ya majumbani na mifugo hususan katika maeneo kame.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha taratibu za kuanzisha Halmashauri mpya 31 ili kusogeza huduma karibu na Wananchi. Halmashauri hizo ni Jiji la Arusha, Manispaa ya Illemela, Manispaa ya Lindi na Halmashauri za Miji ya Kahama, Masasi, Makambako, Geita na Bariadi. Vilevile, imeanzisha Halmashauri za Wilaya ya Kalambo, Busega, Nsimbo, Bumbuli, Mlele, Ushetu, Msalala, Momba, Mbogwe, Kyerwa, Busokelo

na Buhigwe. Halmashauri nyingine zilizoanzishwa ni Nyangh'wale, Wanging'ombe, Chemba, Mkalama, Gairo, Nyasa, Kakonko, Itlima, Uvinza, Ikungi na Kaliua. Serikali itaendelea kuzipatia Halmashauri mpya vitendea kazi, Watumishi pamoja na kujenga miundombinu muhimu hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kukabiliana na tatizo la rushwa kwa kuuelimisha umma kuhusu athari za Rushwa, kuziba mianya ya rushwa na kuwasih Wananchi kuijepusha na vitendo vya rushwa. Aidha, vyombo vya dola vimechunguza tuhuma za makosa ya rushwa na kuwafikisha watuhumiwa mbele ya vyombo vya kisheria. Hadi kufikia Desemba, 2012, tuhuma 2,911 zilichunguzwa ambapo uchunguzi wa tuhuma 390 umekamilika na Kesi 121 zimefunguliwa Mahakamani. Katika mwaka 2013/2014, TAKUKURU itaendelea na uchunguzi wa tuhuma zilizopo na mpya zitakazojitokeza, kuendesha Kesi nyingine zilizopo Mahakamani na zitakazoendelea kufunguliwa kutokana na kukamilika kwa chunguzi mbalimbali. Serikali pia itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu athari za rushwa.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa ilioikumba Nchi yetu kwa mwaka 2012/2013 ni ukame uliosababisha upungufu mkubwa wa chakula katika baadhi ya maeneo nchini. Kutokana na hali hiyo, Serikali ilifanya tathmini za kina za Hali ya Chakula na Lishe Nchini na kubaini kwamba Watu 1,615,440 katika Halmashauri 47 nchini wanahitaji msaada wa chakula. Katika kukabiliana na hali hiyo, kuanzia mwezi Julai, 2012 hadi Machi, 2013, Serikali imetoa Tani 69,452 za chakula cha msaada chenye thamani ya Shilingi Bilioni 26.39 kwa walengwa katika maeneo yenye upungufu. Serikali pia imetoa Shilingi Bilioni 4.6 kwa ajili ya usafirishaji wa chakula hicho.

Mheshimiwa Spika, katika kurejesha hali ya kawaida kwa waathirika wa Mabomu eneo la Gongolamboto, Serikali imekamilisha ujenzi wa Nyumba 36 eneo la Msongola Wilayani llala na Nyumba moja eneo la Mbweni Wilayani Kinondoni.

Zoezi hilo kwa ujumla limegharimu kiasi cha Shilingi Bilioni 1.75. Nyumba hizo ambazo zimewekewa huduma za msingi za maji na umeme zilikabidhiwa kwa walengwa na Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 11 Desemba, 2012.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba, mafuriko yaliyotokea Dar es Salaam mwezi Desemba, 2011 yalisababisha kaya 1,007 za waathirika waliokuwa wanaishi katika maeneo hatarishi zaidi kuhamishiwa katika eneo la Mabwepande Wilayani Kinondoni. Serikali kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuwapatia huduma mbalimbali za kijamii na kuwajengea miundombinu muhimu ikiwemo barabara, maji, umeme, shule, zahanati na Kituo cha Polisi. Aidha, hivi karibuni Serikali imetoa mifuko 100 ya saruji kwa kila kaya ili kuziwezesha kujenga nyumba bora na za kudumu. Napenda kutoa wito kwa Wananchi ambao bado wanaishi mabondeni kuhama ili kuepuka athari zinazoweza kuwapata. Aidha, Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini ziendelee kutenga maeneo yenye usalama kwa ajili ya kuwahamisha wananchi wanaokaa katika maeneo hatarishi.

Mheshimiwa Spika, biashara na matumizi ya Dawa haramu za Kulevyta bado ni tatizo nchini. Hali hii inadhihirishwa na idadi kubwa ya watumiaji walio mitaani na wale wanaojitokeza kupata tiba. Hata hivyo, kutokana na jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali kwa kutumia Kikosi Kazi Maalum cha Kitaifa cha Udhibiti wa Dawa za Kulevyta, jumla ya Kilo 255 za *Heroine* na Kilo 151 za *Cocaine* zilikamatwa mwaka 2012 na watuhumiwa 45 walikamatwa. Vilevile, jumla ya ekari 184 za mashamba ya bangi na kilo 3,200 za Bangi kavu zilitketezwa na Kilo 4,840 za mirungi zilikamatwa. Katika kipindi hicho, Waathirika wa dawa za kulevyta wapatao 20,426 walijitokeza katika vituo mbalimbali vya tiba. Hospitali ya Taifa ya Magonjwa ya Akili ya Mirembe imekuwa ikipokea wastani wa waathirika 400 kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Serikali itakamilisha Sera ya Taifa ya Udhibiti wa Dawa za Kulevyta Nchini na kuandaa mkakati wake wa utekelezaji. Serikali pia

itaendelea kutoa elimu kwa umma juu ya madhara ya Dawa za Kulevyaa na kupanua huduma za matibabu kwa waathirika wa Dawa za Kulevyaa. Wito wangu kwa jamii nzima ni kuendelea kupambana kwa nguvu zote na tatizo la biashara na matumizi ya dawa za kulevyaa ili kunusuru vijana wetu. Wasafirishaji na watumiaji wa dawa hizo tunaishi nao mitaani na ni wajibu wa kila mmoja wetu kuwabaini na kutoa taarifa katika Vyombo vya Dola.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya Manispaa ya Dodoma kwa kujenga barabara zenyenye jumla ya Kilometra 20.6 kwa kiwango cha lami katika maeneo ya Kisasa, Chang'ombe, Kikuyu na Area A. Aidha, imekarabati mtandao wa maji wenye urefu wa Kilometra 17.5 na kusambaza umeme wa msongo mkubwa wenye urefu wa Kilometra 13.5 katika eneo la uwekezaji la Njedengwa. Vilevile, viwanja 1,098 vimepimwa katika maeneo ya Ndachi, Ilazo C-centre, Nala Mizani, Mwangaza, Ipagala, Kizota Relini pamoja na lyumbu *New Town Centre*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Serikali imepanga kukamilisha ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami katika maeneo ya Kisasa, Chang'ombe, Kikuyu na Area A. Vilevile, itaendelea na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami, usambazaji wa umeme wa msongo mkubwa pamoja na usambazaji wa mabomba ya maji safi katika eneo la Uwekezaji la Njedengwa. Pia, itapima Viwanja vipyta 4,476 katika maeneo ya Nzuguni, Mkonze, Ndachi na maeneo ya Viwanda. Pamoja na kazi hizo, kazi iliyoanza ya kuimarisha utendaji wa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma itaendelea.

Mheshimiwa Spika, nimeelezea kwa muhtasari baadhi ya shughuli ambazo Serikali imetekeleza kwa kipindi kilichopita. Aidha, nimetoa Mwelekeo wa Kazi zitakazofanyika mwaka 2013/2014. Kwa kuhitimisha, napenda kusisitiza mambo machache yafuatayo:-

- (a) Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya

mwaka 2012 yameonesha kuna ongezeko la watu milioni 10.1 kutoka watu milioni 34.4 mwaka 2002 hadi milioni 44.5 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 30. Ni dhahiri ongezeko hilo kubwa linahitaji juhudzi za pamoja kati ya Serikali, sekta binafsi, wadai wa maendeleo na wananchi kwa ujumla kuongeza uwekezaji katika huduma mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Rai yangu kwenu ni kuzitumia takwimu hizo kikamilifu katika kupanga mipango ya maendeleo kwa ajili ya watu wetu.

(b) Tumbakiza miaka takriban 12 kabla ya kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, miaka miwili kufikia malengo ya Maendeleo ya Milenia na miaka miwili ya kukamilisha utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Miaka Mitano. Mfumo mpya ulioanzishwa na Serikali wa kufuatilia na kusimamia kikamilifu utekelezaji wa miradi ya kipaumbele na kufanya tathmini ya mara kwa mara ya kupima matokeo utasidia kuharakisha kufikiwa kwa malengo hayo mapema. Serikali itahakikisha kwamba mfumo huo unaimarisha uwajibikaji na kuleta matokeo makubwa na ya haraka katika kipindi kifupi.

(c) Jitihada za Serikali ya Awamu ya Nne katika kuvutia uwekezaji katika kilimo hususan katika Ukanda wa Kilimo wa Kusini mwa Tanzania (*SAGCOT*) zimeleta mwamko na matumaini makubwa. Azma ya Serikali ni kuona kwamba, wawekezaji wakubwa wanashirikiana kwa karibu na Wakulima Wadogo ili waweze kuondoka kwenye kilimo cha kujikumu na kuingia katika kilimo cha kisasa chenye tija na cha kibiashara. Nawahakikisha Watanzania wote kwamba, upatikanaji wa ardhi iliyopimwa kwa ajili ya mkulima mdogo ndicho kipaumbele cha Serikali.

(d) Mchakato wa kuandaa Katiba Mpya umeingia katika hatua ya kuunda Mabaraza ya Katiba katika ngazi mbalimbali yatakayopitia Rasimu ya Katiba Mpya na kutoa maoni. Tume baada ya kuzingatia maoni ya Mabaraza itaandaa Rasimu ya Katiba Mpya itakayowasilishwa katika Bunge Maalum la Katiba. Natoa wito kwa Wananchi watoe

ushirikiano kwa Tume iweze kukamilisha zoezi hilo muhimu kwa ufanisi na kwa wakati.

(e) Amani iliyopo Nchini imetujengea heshima kubwa katika Bara la Afrika na Duniani kote. Sote tuna wajibu wa kuienzi na kuisimamia isitoweke. Serikali ya Awamu ya Nne itahakikisha kwamba, Amani na Umoja wa Kitaifa vinadumishwa ili kuwawezesha Wananchi kuendelea kufanya shughuli zao za maendeleo bila hofu. Serikali haitavumilia kuona mtu au kikundi cha watu wenye dhamira mbaya wakivuruga amani, umoja na mshikamano uliopo nchini kwa kisingizio chochote. Sote tuna wajibu wa kuheshimu utawala wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumalizia hotuba yangu, nimwombe Mheshimiwa Hawa Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, atoe taarifa zilizofanyika katika mwaka 2012/2013 na mwelekeo wa kazi za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka 2013/2014.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa rehema zake, kunipa afya na uzima na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu leo. Awali ya yote, napenda kuwapongeza na kuwashukuru Viongozi wetu Wakuu, Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Mheshimiwa Makamu wa Rais Dkt. Mohamed Gharib Bilal na Mheshimiwa Waziri Mkuu Mizengo Peter Pinda (Mb), kwa uongozi wao imara wenye mafanikio makubwa ambayo wote tunayashuhudia.

Mheshimiwa Spika, pili, nikupongeze na kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika Anna Semamba Makinda (Mb), Naibu Spika, Job Yusto Ndugai (Mb) na Wenyeviti wa Bunge wote, kwa uongozi imara wa shughuli za Bunge katika kipindi hiki. Rai yangu kwa Watanzania wote tuendelee kuimarisha heshima ya nchi yetu na kuhakikisha kuwa tunayalinda mafanikio tuliyoyapata na pia kuimarisha ulinzi na usalama

wa nchi yetu ili amani tuliyonayo isije ikatuponyoka kwani kuirudisha itakuwa ni vigumu.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa mimi mwenyewe pamoja na wasaidizi wangu Manaibu Mawaziri; Mheshimiwa Aggrey Mwanri (Mb) na Mheshimiwa Kassimu Majaliwa (Mb), tunapenda kumshukuru Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maelekezo anayotupatia katika utendaji kazi wetu wa kila siku na hivyo kuifanya kazi yetu kuwa rahisi zaidi. Tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hamis Andrea Kigwangalla, Mbunge wa Nzega pamoja na Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kwa kuchaguliwa kwao kuwa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa kwanza wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Pia, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa kazi kubwa iliyofanyika ya kuchambua Bajeti ya Ofisi yetu na kutupatia maoni, ushauri na maelekezo. Tunaiahidi Kamati kuwa tutafanya kazi kwa ushirikiano wakati wote na tutaendelea kuzingatia ushauri wanaotupatia ili tufikie malengo tunayokusudia.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kuwashukuru Wananchi wa Mtwara Vijijiini kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuhakikisha kuwa eneo letu la Mtwara Vijijiini linafikia maendeleo tuliyokusudia, nawaomba tuendelee na mshikamano na ushirikiano tulionao ili tutimize malengo yetu ya maendeleo. Amani na utulivu kiwe ni kigezo kikubwa cha kutusaidia kuendeleza Wilaya yetu. Aidha, nawashukuru Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Aggrey Joshua Mwanri, Mbunge wa Siha na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge wa Ruangwa, kwa kunipa ushirikiano unaoniwezesha kutekeleza ipasavyo majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, mambo ya habari ya pongezi naomba ufute, tunafahamiana wote hao.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Watumishi walio katika Mamlaka za Serikali za Mitaa wameendelea kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu. Watumishi hawa wameweza kushirikiana na Madiwani katika maeneo yao na Wananchi kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya Sekta za Elimu, Afya, Maji na Barabara na Sekta zingine zote.

Mheshimiwa Spika, aidha, wamesimamia vyema utendaji wa kazi wa siku hadi siku wa Mamlaka hizo na kuziwezesha kufanya vizuri katika upimaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya kufuzu kupata ruzuku ya maendeleo kupitia mfumo wa kuzipatia Mamlaka ruzuku ya maendeleo isiyo na masharti pamoja na ruzuku ya kujenga uwezo. Napenda kuchukua nafasi hii kupitia Bunge lako Tukufu, niwashukuru na kuwapongeza Wananchi, Waheshimiwa Madiwani na Wataalam wote, kwa kutimiza wajibu wao na kuwezesha kupata mafanikio yaliyo dhahiri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, bado iko changamoto kwa baadhi ya watumishi wanaofanya kazi katika ngazi hiyo, wasiozingatia Dhana ya Utawala Bora. Serikali inaendelea kuchukua hatua kwa Watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ambao kwa njia moja au nyingine wanashindwa kuzingatia Sheria, Kanuni na taratibu katika utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa kuanzia Aprili 2011/2012 hadi Februari, 2013 ni pamoja na; Wakurugenzi wa Halmashauri tisa wamevuliwa madaraka, wawili wamesimamishwa kazi na mashauri yao yapo Mahakamani. Aidha, baadhi ya Wakuu wa Idara katika Halmashauri 73 wamechukuliwa hatua za kinidhamu kutohana na tuhuma mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha Utumishi wa Serikali za Mitaa, hivi sasa Halmashauri zote zinatumia Mfumo wa Lawson ambao unasaidia kuweka taarifa zote za watumishi ikiwa ni pamoja na utaratibu wa ulipaji wa

mishahara. Hivyo, matatizo yaliyokuwa yanajitokeza kuhusu mishahara ya watumishi yatadhibitiwa kwa sababu Idara ya Utumishi katika Halmashauri ndio inayosimamia Mfumo huo na itakuwa rahisi kuwajibishwa yanapotokea matatizo ya aina hiyo. Napenda kuchukua nafasi hii kuwaagiza Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini kuhakikisha kuwa wakati wote anakuwepo mtaalam anayeweza kutumia mfumo huo ili kuepuka kukwamisha kazi za Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, eneo la mapato ni eneo lenye changamoto kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zenyewe lakini pia kwa Serikali kwa ujumla. Bado mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani vya Halmashauri yanachangia chini ya asilimia kumi ya fedha zote zinazotumika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikuwa zimekadiriwa kukusanya jumla ya shillingi 362,206,000,000.00 Hadi kuflibia mwezi Desemba, 2012 zilikusanya jumla ya shillingi 117,292,888,960.91 sawa na asilimia 38.4 ya malengo. Hatua mbalimbali zinachukuliwa ili kukabiliana na changamoto hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza programu ya uendelezaji Miji ya kimkakati katika Miji saba nchini, suala la jinsi ya kuimarisha mifumo ya ukusanyaji na utoaji taarifa wa mapato ya Halmashauri yatokanayo na vyanzo mbalimbali ikiwemo kodi ya majengo linafanyiwa kazi. Miji inayohusika na majaribio yanayofanyika ni Mtwara, Mbeya, Dodoma, Kigoma, Mwanza, Arusha na Tanga. Kazi hiyo inafanyika kwa kutumia Mtaalam Mshauri chini ya Ufadhilli wa Benki ya Dunia na *DANIDA*. Aidha, majaribio haya yameonesha kuwa na mafanikio na kwa sasa shughuli ya uunganishaji wa mfumo wa kuwa na takwimu za walipa kodi inaendelea.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo wa *GIZ-SULGO* imeanza kuimarisha mifumo ya ukusanyaji mapato kwa kusimika mfumo wa e-Tax katika Halmashauri za Wilaya za Mtwara na Bunda, Halmashauri za Manispaa za Kinondoni na Mtwara Mikindani na Halmashauri ya Jiji la Tanga. Juhudi hizi zina malengo mahususi ya

kuanzisha na kuimarisha mifumo madhubuti ya utambuzi wa walipa kodi na kiwango kinachopaswa kulipwa kwa wakati, utunzaji wa kumbukumbu na taarifa zote za Mapato na Walipa Kodi na uandaaji wa utoaji taarifa za ukusanyaji mapato.

Mheshimiwa Spika, kadhalika Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), imeanza kufanya utafiti wa kutambua uwezo wa kukusanya mapato kwa kulinganisha na uchumi wa kila Halmashauri. Kwa kuanzia, Utafiti unahusisha Mamlaka za Serikali za Mitaa zipatazo 30 kwa kuainisha na kupembua takwimu za vyanzo vikuu vya mapato kwa miaka mitano mfululizo. Kazi hiyo ilianza kufanyika mwezi Machi, 2013 chini ya Ufadhilli wa Progaramu ya Maboresho ya Menejimenti ya Fedha za Umma Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Spika, Utafiti huu utawezesha Serikali kuangalia njia rahisi ya ukusanyaji wa kodi na ada mbalimbali ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji na kuongeza wingi wa makusanyo. Vilevile, Serikali itaangalia uwezekano wa namna bora ya kupunguza idadi ya Kodi na Ada zisizo na ulazima ili iwe rahisi na kuondoa usumbufu kwa walipa kodi.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Hesabu za Serikali zinaandaliwa kwa kuzingatia viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma (*IPSAS*). Kwa hivi sasa udhibiti wa mapato na matumizi unafanyika ndani ya mfumo wa Usimamizi wa Fedha za Umma wa *IFMS - Epicor 9.05* ambapo Halmashauri zipatazo 133 zimeunganishwa na mfumo huu. Hatua hii ni muhimu kwa ajili ya udhibiti wa fedha za Umma pamoja na kupata taarifa zenye uhakika, sahihi na kwa wakati. Hali ya udhibiti wa fedha za Umma imeimarika kwa kiwango kikubwa baada ya mfumo huu kuanzishwa na tunategemea kuanganisha pia Mamlaka za Serikali za Mitaa mpya katika mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, katika dhana ya upelekaji wa madaraka kwa Wananchi, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapewa uhuru wa kufanya maamuzi mbalimbali yahusuyo utoaji wa huduma kwa Wananchi walio katika Mamlaka hizo

na kuwashirikisha Wananchi katika kujiletea maendeleo na ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupewa uhuru huo, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuutumia kwa kuzingatia Katiba na Sheria za Nchi. Endapo Mamlaka hizo zitakwenda kinyume chake, Serikali Kuu inao wajibu wa Kikatiba na Kisheria kuingilia kati na kuchukua hatua dhidi ya Mamlaka hizo.

Mheshimiwa Spika, matokeo yanayotarajiwa kutokana na utekelezaji wa Programu hii ni kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwa vyombo imara vya kusimamia na kuratibu shughuli za kijamii na kimaendeleo, utoaji huduma na kutekeleza ajenda ya kuondoa umaskini katika maeneo yao ikiwa ni pamoja na:-

(i) Wizara za Kisekta zitakuwa zimefanikiwa kuainisha majukumu yake chini ya mahusiano mapya kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ambapo Serikali Kuu itabaki na majukumu ya kutunga Sera, Sheria, kuweka viwango vya utekelezaji, kusimamia utekelezaji na kuingilia kati pale Serikali za Mitaa zinaposhindwa kutekeleza majukumu yake na kutofua Sera na Sheria za Nchi;

(ii) Sera na Sheria za Kisekta zitakuwa zinaendana na kuzingatia Sera ya Serikali ya Kupeleka Madaraka kwa Wananchi na hivyo kuondoa migongano ya utekelezaji kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa;

(iii) Uongozi na Menejimenti za Halmashauri zitakuwa zimejengewa uwezo wa kuibua mambo, kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Halmashauri na kuwasimamia Wananchi wake ipasavyo;

(iv) Uandaaji, utekelezaji, ufuatilajji, tathmini na utoaji taarifa za utekelezaji wa mipango utakuwa umeboreshwa;

(v) Shughuli za Hamashauri zitakuwa zimeboreshwa kutokana na matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano;

(vi) Kudumisha mafanikio, hamasa na mwitikio mzuri wa Wananchi katika kushiriki shughuli za maendeleo katika maeneo yao;

(vii) Wananchi kuwa na uelewa wa madaraka waliyonayo na wajibu wao katika kujilletea maendeleo katika maeneo yao;

(viii) Watendaji katika ngazi za msingi za Serikali za Mitaa watakuwa wamejengewa uwezo wa kuwaongoza na kuwahudumia Wananchi kwa misingi ya Utawala Bora;

(ix) Ngazi ya Mkoa itakuwa imelmarishwa na kupewa watumishi wenyewe uwezo, rasilimali fedha na rasilimali nyinginezo ili kuiwezesha ngazi hii ya utawala kuwa kiungo imara cha kusimamia kutekeleza kazi za Serikali za Mitaa na kuratibu shughuli za Serikali Kuu zinazofanyika katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, kuanzia Mwezi Julai hadi Desemba, 2012, shughuli zilizofanyika ni pamoja na:-

(i) Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kwa kushirikiana na Wizara za Kisikta na Sekretarieti za Mikoa iliandaa Mwongozo wa Upimaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mwongozo huu ultumika katika upimaji uliofanyika mwezi Desemba, 2012.

(ii) Wataalam 125 kutoka katika Sekretarieti za Mikoa walipatiwa mafunzo yaliyowawezesha kuendesha zoezi la upimaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya kufuzu kupata ruzuku ya maendeleo na kujenga uwezo.

(iii) Kuitisha kikao cha pamoja na Washirika wa Maendeleo na Wizara za Kisikta kwa madhumuni ya

kukubaliana juu ya mipango ya baadaye ya Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa.

(iv) Kufanya mapitio ya muda wa kati wa Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya upimaji uliofanywa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 132 kwa ajili ya kufuzu kupata ruzuku katika mwaka 2013/2014 umeonesha kwamba Halmashauri 104 zilifanya vizuri na hivyo zitapata asilimia 100 ya fedha za maendeleo, Halmashauri 27 zitapata asilimia 80 na Halmashauri ya Manispaa ya Tabora ambayo haikufanya vizuri itapata asilimia 50. Pamoja na kwamba, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali bado hajajumuishwa katika matokeo haya ya upimaji, Halmashauri nyingi zimefanya vizuri. Halmashauri itakayopata Hati Chafu, itapewa asilimia 25 tu ya fedha za maendeleo.

Kwa upande wa fedha za kujenga uwezo, Halmashauri zote zitapata asilimia 100 ya mgao wao. Kwa zile zitakazoshindwa kupata asilimia 100 ya fedha za maendeleo, hatua za kuimarisha utendaji wa Halmashauri hizo zitachukuliwa. Jumla ya shilingi bilioni 3.3 zimetumika kutekeleza shughuli hizo pamoja na gharama za kuwahudumia Wataalam Washauri wa Programu waliomaliza mikataba yao mwezi Desemba, 2012 kwa upande wa Makao Makuu au wale walio katika ngazi ya Mkoa ambao mikataba yao inamalizika mwezi Juni, 2013.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 kiasi cha shilingi bilioni 128.9 kutoka katika Mfuko wa Barabara zilitengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi kufikia mwezi Februari, 2013 jumla ya shilingi bilioni 57.039 zilikuwa zimepokelewa na kupelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya barabara. Utekelezaji ulihusisha matengenezo ya kawaida (*Routine Maintenance*) kilometra 1,618.39, sawa na asilimia 7.92 ya makadirio ya kilometra 20,424 kwa gharama ya shilingi milioni 1,571.41, matengenezo ya muda maalum (*Periodic Maintenance*) kilometra 164.44, sawa

na asilimia 6.09 ya makadirio ya kilometa 2,699 kwa shilingi milioni 1,403.00 na matengenezo ya dharura (*spot maintenance*) katika maeneo korofi kilometa 391.03, sawa na asilimia 5.41 ya makadirio ya kilometa 7,210 kwa shilingi milioni 920.05. Vilevile, matengenezo ya madaraja, makalvati na *drift* yamefanyika na kutumia kiasi cha shilingi milioni 515.31.

Mheshimiwa Spika, ufuatiliaji umefanyika katika Halmashauri 27 ambazo zilitakeleza Mpango Kazi wa barabara chini ya asilimia 50 ya fedha zilizopelekwa kutoka Mfuko wa Barabara kwa mwaka 2011/2012. Halmashauri hizo ni pamoja na Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Halmashauri za Manispaa za Moshi, Ilala, Kinondoni, Kigoma Ujiji, Sumbawanga, Mtwara na Lindi; Halmashauri ya Mji Kibaha pamoja na Halmashauri za Wilaya za Moshi, Kibondo, Kigoma, Ngorongoro, Kilindi, Korogwe, Pangani, Kibaha, Makete, Kyela, Mbozi, Mbeya, Mbarali, Mafia, Tandahimba, Nachingwea, Lindi na Kilwa. Katika maeneo hayo, upungufu ulioonekana katika ufuatiliaji ni pamoja na baadhi ya Halmashauri kutokamilisha kazi kwa wakati kwa sababu ya Wakandarasi kusimamishwa kutokana na kufanya kazi chini ya viwango na hivyo kupelekeea mchakato mpya wa kumtafuta Mkandarasi mwingine.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014 kiasi cha shilingi bilioni 151.3 kimetengwa kutoka Bodi ya Mfuko wa Barabara kwa ajili ya kutekeleza kazi mbalimbali. Kazi zitakazoendelea kutekelezwa ni: Matengenezo ya kawaida ya barabara, matengenezo ya muda maalum, matengenezo ya dharura na ujenzi wa miundombinu mingine ya madaraja na *drift* katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Uendelezaji Miji ya Kimkakati unalenga uboreshaji wa miundombinu katika Miji saba na Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu. Mradi unatekelezwa katika maeneo makuu matatu ambayo ni: Ujenzi na ukarabati wa miundombinu, uimarishaji wa Taasisi na usimamizi na utekelezaji wa Mradi pamoja na kuandaa Miradi mingine itakayotokana na Mradi huu.

Mheshimiwa Spika, Kandarasi za awamu ya kwanza utekelezaji wake ulianza mwezi Novemba, 2011 kwa gharama ya shilingi bilioni 81.12 na umefikia asilimia 60 na 95. Aidha, Kandarasi za awamu ya pili ambazo zimeanza kutekelezwa mwezi Juni, 2012 kwa gharama ya shilingi bilioni 74.78 utekelezaji wake umefikia katika asilimia 25 na 55. Mikataba ya Kandarasi za awamu ya tatu imesainiwa mwezi Novemba, 2012 na itatekelezwa kwa gharama ya shilingi bilioni 34.69 na wakazi walioathirika na utekelezaji wa Mradi katika mji husika wamelipwa fidia ya shilingi bilioni 2.41.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uimarishaji wa Taasisi, Miji imewezeshwa vitendea kazi na baadhi ya ofisi zimekarabatiwa na watumishi wamepatiwa mafunzo katika maeneo mbalimbali. Vilevile, Mfumo wa taarifa za kijigrafia (*Geographical Information System - GIS*), umeandalila kwa kutumia picha za *satellite* ambazo zimeboreshwa (*digitized and rectified*) kuititia Wizara ya ardhi, nyumba na maendeleo ya makazi. Lengo ni kuwa na kumbukumbu za walipa kodi za majengo pamoja na vyanzo vingine vya mapato. Aidha, Halmashauri zimeajiri Wataalamu washauri wa kufanya tafiti za kutambua wigo wa vyanzo vya mapato na utayari wa Wananchi kulipa kodi na ushuru. Maandalizi ya kuwapata wakandarasi watakaohusika na zoezi la ukusanyaji taarifa muhimu za walipa kodi yamekamilika na mikataba inasubiri kuwekewa saini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Serikali imeanza utekelezaji wa mradi wa kuimarisha miundombinu na uwezo wa kutoa huduma za jamii katika Halmashauri za Manispaa kumi na moja na Halmashauri za Miji saba. Manispaa zinazohusika ni Morogoro, Moshi, Musoma, Iringa, Bukoba, Shinyanga, Singida, Sumbawanga, Songea, Lindi na Tabora. Miji inayohusika ni Babati, Njombe, Bariadi, Korogwe, Mpanda, Kibaha na Geita. Matayarisho ya Programu yamekamilika katika mwaka wa fedha 2012/2013 na kazi zitaanza katika mwaka wa fedha 2013/2014. Mradi utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2013/14 hadi 2018/19. Mradi huu unategemea kugharimu jumla ya Dola za Kimarekani milioni 255, ambapo inakisiwa

kuwa Dola milioni 195 zitatumika kwa ajili ya kuboresha miundombinu kwenye Halmashauri za Miji husika na Dola milioni 60 zitatumika katika usimamizi wa Mradi na kujijengea uwezo Halmashauri hizo ili ziweze kukidhi vigezo vilivywerekwa na kutoa huduma bora za kijamii.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa uendelezaji wa Jiji la Dar es salaam ni sehemu ya juhudini zinazofanywa na Serikali katika kujijengea uwezo Miji ili iweze kutoa mchango wake katika Maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii. Halmashauri zote nne za Mkoa wa Dar es Salaam zimehusika katika kutayarisha mapendekezo ya miradi itakayotekelizwa kwa kuwashirikisha kikamilifu Wananchi na Sekta Binafsi. Utekelezaji wa mradi huu umeanza kwa matayarisho ya mradi na yatakamilika katika mwaka huu wa fedha 2012/2013 na utekelezaji wa mradi utaanza katika mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, TEHAMA, inasaidia upatikanaji wa taarifa sahihi na kwa wakati na kuwezesha utoaji wa huduma kupitia Serikali mtandao. Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) immeendelea kutoa ushauri na hivyo kuwezesha matumizi ya Serikali mtandao katika ngazi zote za Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI). Miundo ya Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa imehuushwa kwa kuzingatia mahitaji ya TEHAMA na kuna Vitengo vya TEHAMA kwenye ngazi hizo vinavyofanya kazi. Hadi kufikia mwezi Februari, 2013 kuna jumla ya Wataalamu wa TEHAMA 76 waliopo kwenye ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, ili kuendelea kuboresha mawasiliano, tumejenga Mtandao wa Ndani (*Local Area Network*) kwa ajili ya kuhifadhi takwimu na kupata *internet*. Vilevile, uko Mtandao wa kuunganisha Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (*Wide Area Network*). Katika mwaka wa fedha 2012/2013, mtandao huu umeendelea kuziunganisha Mamlaka za Serikali za Mitaa zote 133 na Mikoa 21. Kwa sasa mtandao huo unatumika kwa Mfumo wa *Epicor* na tayari matayarisho yanafanywa ili kuweza kutumia kwa ajili ya mifumo mingine ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), sambamba na ile ya Kisekta kwa kadiri ya mahitaji.

Maandalizi ya kuunganishwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mikoa mipyä kwenye mtandao huu yanaendelea. Mfumo wa *Epicor*, Toleo Na. 9.05, unatumiliwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa 133 nchini katika kuandaa malipo mbalimbali pamoja na kuingiza mapato.

Mheshimiwa Spika, Ofisi yangu imeanzisha maabara ya *computer* kwa ajili ya kufundishia watumishi wa ngazi zote programu mbalimbali na matumizi ya vifaa vya TEHAMA. Aidha, jumla ya watumishi 345 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa walijengewa uwezo wakiwamo watumishi 247 waliopata mafunzo kuhusu Mfumo wa Usimamizi Rasilimali Watu unaosimamiwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na watumishi 98 walijengewa uwezo kuhusu Mfumo wa Kudhibiti Mapato na Matumizi ya Serikali za Mitaa. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 tutaendelea na kuimarisha mifumo tulyo nayo ili iendelee kutuwezesha kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, tabia ya kuvamia maeneo ya shule za sekondari na msingi kwa kujenga vibanda vya biashara katika uzio wa shule na kujengwa na kuendeshwa kwa biashara za nyumba za kulala wageni na baa karibu na viwanja vya shule umeendelea kuwa changamoto katika uendeshaji wa shule zetu. Mwaka jana nililieza hili na leo narudia tena na kuwaagiza Makatibu Tawala wote wa Mikoa kulisimamia kwa nguvu zote kuhakikisha kuwa tatizo hili linaondoka. Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wasimamie upimaji wa ardhi na kudhibiti utaratibu mbaya unaofanyika wa kubadilisha matumizi ya viwanja vinavyotolewa kwa Wananchi. Vibali vyote vya biashara viliviyotolewa vya kujenga Nyumba za Kulala Wageni na uendeshaji wa baa karibu na viwanja vya shule visitishwe mara moja. Aidha, Halmashauri zihakikishe zinaweka na kutekeleza utaratibu wa kupima maeneo ya shule na kutoa hati miliki.

Mheshimiwa Spika, kati ya Wanafunzi 865,827 waliofanya mtihani wa darasa la saba katika mwaka 2012, wanafunzi 505,724 walichaguliwa kuijunga na Kidato cha

Kwanza katika Shule za Serikali. Naomba nichukue nafasi hii kupitia Bunge lako Tukufu, kuwaagiza Wakuu wa Wilaya wote nchini, kuendelea kusimamia na kuhakkisha kuwa Wanafunzi wote waliochaguliwa kujunga na Kidato cha Kwanza katika Wilaya zao wanaripoti shulenii. Aidha, wazazi watakaobainika kuwazuia watoto wao kujunga na Kidato cha Kwanza, wachukuliwe hatua kali za kisheria.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira ya Walimu, kwa mwaka 2013 Serikali imefanikiwa kuajiri idadi ya Walimu wapatao 26,537. Kati ya hao, 13,568 ni wa Shule za Msingi na 12,969 ni wa Shule za Sekondari. Rai yangu kwa Walimu wapya na wale wengine wote kuhakkisha kuwa wanatambua haki na wajibu wao katika kutoa elimu bora kwa Vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu mwaka 2010, Ibara ya 84 (a), Serikali imeendelea kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi (MMEM) Awamu ya Tatu, ambao umeanza mwaka 2011/2012 hadi 2015/2016. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, jumla ya shilingi bilioni 56.4 ruzuku ya uendeshaji wa shule za msingi zilipelekwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hadi kufikia Januari, 2013. Fedha hizo zimetumika kununua vifaa vya walimu na viandikio kwa wanafunzi, ukarabati wa majengo ya shule na kuendesha mitihani ya ndani. Serikali inaendelea kuboresha utoaji wa elimu kwa kununua vitabu vya kiada. Hadi Februari, 2013 pamefanyika mchakato wa ununuzi wa vifaa mbalimbali, vitabu vya kiada, Kamusi za Kiswahili na Kiingereza pamoja na vifaa kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum vyenye thamani ya Sh. bilioni 30.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2013/2014, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi umelenga kujenga miundombinu ya madarasa, nyumba za walimu, vyoo na kutengeneza madawati katika shule mbalimbali. Fedha za kutekeleza malengo haya zimetengwa katika bajeti za kila Mamlaka za Serikali za Mitaa husika. Aidha, fedha za ununuzi wa vitabu inayofikia kiasi cha shilingi bilioni 38 imetengwa kupitia Fungu 56 la Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI).

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipokea fedha zilizopatikana katika fidia ya Rada (*BAE System Funds Plc*) kiasi cha Paundi za Uingereza 29,000,000, sawa na shilingi za Tanzania 73,660,000,000. Kulingana na Mkataba wa Makubaliano (*MoU*), kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Uingereza kupitia Shirika la Maendeleo la *DFID*, ilikadiriwa kuwa sawa na asilimia 75 ya fedha zitatumika kununua vitabu vya kiada, viongozi vya walimu, mihtasari pamoja na miongozo ya mihtasari kwa ajili ya shule za msingi Tanzania Bara na asilimia 25 ya fedha hizo zitatumika kwa ajili ya ununuzi wa madawati katika Shule za Msingi. Kiasi hicho sasa kimeongezeka kutokana na kupanda kwa thamani ya fedha na riba ya Benki hadi kufikia shilingi 78,718,180,000; hivyo fedha itakayotumika kwa ununuzi wa vitabu imefikia shilingi 59,038,635,000.00 na fedha kwa ajili ya ununuzi wa madawati imefikia kiasi cha shilingi 19,679,545,000.00.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa ununuzi wa vitabu umekamilika ambapo Serikali imeingia mikataba yenye thamani ya shilingi 56,929,278,775.60 na Wachapishaji wa vitabu tisa pamoja na Taasisi ya Elimu Tanzania ambayo ina jukumu la kuchapisha Mihtasari na Miongozo yake. Kulingana na mikataba, kazi hii inategemewa kukamilika ndani ya miezi sita tangu tarehe ya kuweka saini mikataba tarehe 18 Machi, 2013. Muda huu umezingatia kuwa vitabu hivi ni vipyta na vinachapishwa nje ya nchi na pia vitabu hivi vinatakiwa kuwasilishwa katika kila shule hivyo muda utakaohitajika kwa ajili ya usambazaji umezingatiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ununuzi wa madawati, mchakato umeanza ambapo awali ilipendekezwa kuwa madawati yanunuliwe kwa ajili ya Halmashauri tisa zenye upungufu mkubwa wa madawati na matokeo dhaifu katika mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi. Lengo lilikuwa ni kumaliza tatizo la madawati katika Halmashauri hizo. Katika Kikao cha Bunge la Bajeti ya mwaka wa fedha 2012/2013 iliazimiwa kuwa madawati yanunuliwe na kusambazwa katika Halmashauri zote kwa usawa. Aidha, katika kikao cha Kamati Endeshi (*Steering Committee*) ya

matumizi ya fedha za *BAE System*, iliamuliwa kuwa aina ya dawati liwe ni la kukaliwa na mwanafunzi mmoja. Hii inatokana na kuhama katika mfumo wa ufundishai na kuwa mfumo shirkishi ambapo wanafunzi wanajifunza kwa kujadiliana zaidi na kuchangiana mawazo ya uelewa wao kuliko kumsikiliza mwalimu zaidi. Baada ya uchaguzi wa aina za madawati yatakayonunuliwa na kupata viwango (*specifications*), vya madawati hayo kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, zabuni zinatarajia kutangazwa mapema mwezi Aprili, 2013.

Mheshimiwa Awamu ya Pili ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) (2012 – 2014), umelenga kukamilisha ujenzi wa shule mbili katika kila Halmashauri kwa kuziwekea mahitaji yote muhimu kama madarasa, nyumba za walimu, maabara, vyoo, maji na samani. Kwa awamu hii kiasi cha shillingi billioni 56 zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa shule 264 ambazo uteuzi wake ulifanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Halmashauri zimetangaza zabuni na wazabuni walioshinda wapo katika hatua ya kuingia mikataba ili kuanza kazi ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, michezo ni muhimu kwa wanafunzi hivyo uratibu wa mashindano ya michezo ya shule za msingi na sekondari UMITASHUMTA na UMISSETA unaendelea kufanyika ili michezo hiyo ifanyike baada ya mwezi Juni, 2013 Mjini Kibaha. Michezo inayoshindaniwa ni pamoja na riadha, mpira wa miguu, mpira wa pete, wavu, netiboli na mpira wa meza. Mashindano ya taaluma na ubunifu hufanyika ili mashindano ya UMITASHUMTA yahusishe pia washiriki kutoka Zanzibar kama inavyofanyika kwa mashindano ya UMISSETA.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013 Mamlaka za Serikali za Mitaa zilitengewa jumla ya shilingi bilioni 64.9 kwa ajili ya utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 39.2 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya mazao, mifugo na uvuvi (*DADPs*) na shilingi bilioni 25.7 kwa miradi ya umwagililaji (*DIDF*) 140. Hadi kufikia Desemba, 2012, Halmashauri zimepokea jumla ya shilingi bilioni 6.9 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi

mbalimbali ya mazao, mifugo na uvuvi. Mwaka 2012/2013 ni mwaka wa mwisho wa utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP) kwa awamu ya kwanza (ASDP I).

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2012/2013 Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini zimeendelea kutekeleza na kukamilisha Miradi ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya, ambapo hadi kufikia Desemba, 2012 jumla ya malambo 365 yamejengwa na mengine kukarabatiwa kwa ajili ya matumizi ya maji ya mifugo. Masoko ya msingi ya Mifugo 34 na machinjio 77 yamejengwa na vituo vya kkusanya maziwa 24 vimejengwa na zaidi ya wakulima 72,271 pamoja na vikundi vya wakulima zaidi ya 523 vimenufaika. Majosho 429 na Vituo 43 vya Tiba za Mifugo vimejengwa na mifugo zaidi ya 10,545,104 imepatiwa chanjo dhidi ya magonja mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, eneo linalotumika kwa kilimo cha umwagiliaji limeongezeka kutoka hekta 264,388 mwaka 2006/2007 hadi 363,514 mwaka 2011/2012. Maghala ya kuhifadhi mazao 659 na masoko ya mazao 131 yamejengwa. Aidha, mashine za kukoboa na kusaga nafaka 2,067 zimenunuliwa hivyo, kunufaisha zaidi ya wakulima 215,092 na kilo 30,347 za mbegu bora za mazao zimegawiwa kwa vikundi 34,518 na kusambazwa kwa wakulima wengine. Pia, barabara zenye urefu wa kilomita 372 na madaraja 7 yamejengwa ambapo wazalishaji wa mazao ya kilimo zaidi ya 25,205 wamenufaika.

Mheshimiwa Spika, ng'ombe zaidi ya 23,187, kuku 3,224 na mbuzi 3,423 wamenunuliwa na kuboreshwa. Pia, wafugaji wamepatiwa madume bora ya ng'ombe yapatayo 986, mbuzi 1,487 na majogoo 8,643 kwa lengo la kuongeza uzalishaji ambapo wafugaji zaidi ya 9,821 wamenufaika. Idadi ya wataalam wa huduma za ugani imeongezeka kutoka 3,326 na kufikia Wataalam 10,891 ambapo 6,925 ni Wataalam wa Kilimo na 3,966 wa Mifugo.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha zana bora za kilimo hadi kufikia Desemba, 2012 matrekta ya kukokotwa

na mikono (Power tillers) 72 na matrekta makubwa 18 yamenunuliwa na kufanya jumla ya Power tillers zilizonunuliwa nchini hadi kufikia Desemba, 2012 kuwa 4,019 yenye thamani ya shilingi bilioni 26.7 na idadi ya matrekta makubwa kufikia 361 yenye thamani ya shilingi bilioni 12.1. Matrekta na Power-tiller hizo zimenunuliwa na vikundi mbalimbali vya wakulima kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa chini ya Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPs*). Aidha, Vituo 5 vya kutolea huduma za mafunzo kwa wakulima juu ya matumizi ya zana za kilimo vimejengwa na wakulima zaidi ya 10,117 wamenufaika. Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 Mamlaka za Serikali za Mitaa zimetengewa jumla ya shilingi bilioni 31 kwa ajili ya kukamilisha miradi inayoendelea katika kipindi cha mpito kabla ya kuanza kwa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (*ASDP II*).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 jumla ya shilingi 851,500,000 ziliidhinishwa kwa ajili ya Mamlaka za Serikali za Mitaa 65 Tanzania Bara na shilingi 42,500,000 katika Sekretariati za Mikoa 17 zinazotekeleza Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta ya Ngozi. Hadi kufikia Februari, 2013 hakuna fedha zilizopokelewa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2012/2013 Mamlaka za Serikali za Mitaa 65 nchini zimeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali za Mkakati kwa kutumia bakaa la fedha za mwaka 2011/2012 shilingi milioni 677 ambazo ziliipelekwa Mei 2012. Hadi kufikia Desemba, 2012 jumla ya wafugaji 2,522, wachinjaji na wachunaji ngozi 1,744, wawambaji na wachambuzi wa madaraja ya ngozi 818, wafanyabiashara wa ngozi 300, Maafisa Ugani 1,325 na Madiwani na Viongozi wengine wa Serikali 2,048 wamehamasishwa na kupewa mafunzo kuhusu shughuli za Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta na Viwanda vya Ngozi nchini. Aidha, mashine za kunyanyulia ng'ombe wakati wa kuchinja (*lifting equipment*) 112, computerndogo (*Laptop computer*) 22, Printers nne, Cherehani tano na Kamera za Digitali sita vimenunuliwa. Fremu za kukaushia ngozi mbili zimejengwa na machinjio 33 yamekarabatiwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Programu ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 4.3 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za usimamizi shirikishi wa Misitu katika baadhi ya Halmashauri za Mikoa ya Iringa, Mbeya, Njombe, Morogoro na Lindi. Aidha, hadi Februari, 2013 zimetolewa shilingi 671,728,117 ambazo zilipelekwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, hadi Februari 2013 zimetolewa shilingi 671,728,117 ambazo zilipelekwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, fedha za uratibu wa programu zilipelekwa katika Sekretarieti za Mikoa husika kwa ajili ya utekelezaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kazi ya kupitia upya andiko la Programu ya Taifa ya Misitu na Nyuki iliyokuwa inafanywa na Ubalozi wa Finland kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania imesababisha fedha shilingi 3,424,900,000 kuchelewa kutolewa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Programu ya Usimamizi Endelevu wa Ardh Oevu iliidhinishiwa shilingi 559,132,000.00 kwa ajili ya uratibu na utekelezaji wa shughuli katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazotekeleza Programu hiyo. Hadi Februari, 2013 shilingi 138,147,560.00 ziliikuwa zimetolewa na kupelekwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekretarieti za Mikoa kwa ajili ya utekelezaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazotekeleza Programu hiyo na uratibu kwa lengo la kuinua kipato cha jamii. Miradi inayohusika ni miradi ya umwagiliaji, ufugaji wa kuku na ukaushaji wa samaki.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kuzisaidia Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini katika kuimarisha mapato yake. Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imanzisha mazungumzo na Uongozi wa Benki ya Rasilimali (*Tanzania Investment Bank – TIB*) ambayo imeonesha nia ya kuzikopesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa masharti nafuu ili zitekeleze miradi itakayoziwesha kuongeza mapato na hatimaye kutoa huduma bora kwa Wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, katika mazungumzo na benki hiyo, Benki ya Rasilimali itazijengea uwezo Mamlaka za Serikali za

Mitaa wa kuandika maandiko ambayo yanakubalika kifedha kuziwezesha kukopa katika mabenki mengine. Aidha, Benki hiyo itasimamia utekelezaji wa Miradi hiyo ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa mapato hadi benki itakapokamilisha urejeshaji wa mkopo ndipo Mradi utakabidhiwa kwa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Rasilimali imeanza kuzishirikisha benki ya *CRDB* na *NMB* katika nyanja hii ili kuongeza nguvu katika utekelezaji. Benki hizi zimeonesha nia ya kushiriki. Miradi ambayo imeainishwa kuhusika ni upimaji wa viwanja, kuweka huduma muhimu kama maji, barabara na umeme na kuviuza kwa wananchi. Mradi mwiningine ni wa ujenzi wa masoko na stendi za mabasi. Hivi sasa Benki ya Rasilimali imeanza kufanya kazi na Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba katika ujenzi wa Soko na Stendi ya mabasi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo kimeendelea na mipango yake ya kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika kozi mbalimbali. Aidha, udahili wa wanafunzi umeongezeka kutoka wanafunzi 2,286 mwaka 2011/2012 hadi wanafunzi 2,437 katika mwaka wa masomo 2012/2013. Idadi hii ni ongezeko la wanafunzi 151 sawa na asilimia 6.6 ya wanafunzi waliodahiliwa mwaka wa masomo 2011/2012. Katika mwaka wa fedha 2012/2013 Chuo kilikadiria kuwa na mapato na matumizi ya shilingi 4,427,371,250 kwa ajili ya kulipia mishahara na matumizi mengine. Kati ya mapato hayo, ruzuku ni shilingi 1,923,371,250 na mapato kutokana na vyanzo vya ndani ni shilingi 2,504,000,000. Hadi Desemba, 2012 jumla ya shilingi 2,744,290,300 zilikuwa zimekusanywa na shilingi 2,025,179,579.34 kutumika.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizotekelwa ni pamoja na ununuzi wa kompyuta mpya 50, mashine za kudurufu na vifaa vya ofisi, usimikaji wa mtandao wa simu na mawasiliano ya TEHAMA, kulipa deni la samani zilizokuwa zimenunuliwa awali, kuwezesha zoezi la ajira kwa watumishi wapya 26 na kulipia gharama za uendeshaji wa chuo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Chuo kilitengewa kiasi cha shilingi milioni 650 ikiwa ni ruzuku ya miradi ya maendeleo kwa ajili ya kulipa fidia ya eneo lililotwaliwa na Chuo. Hadi kufikia Desemba, 2012 kiasi cha shilingi milioni 300 kilitolewa sawa na asilimia 46 ya bajeti iliyotengwa. Kiasi cha shilingi milioni 300 kimetumika kulipa fidia inayohusika. Kazi nyingine zilizofanyika ni ujenzi wa Kituo cha Afya kwa matumizi ya Chuo na jamii inayozunguka chuo, kukamilisha awamu ya kwanza ya mradi wa upanuzi wa chuo kwa mkopo kutoka Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa (*LAPF*) kwa gharama ya shilingi bilioni 35.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukuaji wa Chuo, bado Chuo kinakabiliwa na changamoto ya kutokuwa na huduma za kibenki karibu na eneo la Chuo ambazo zinahitajika kwa Watumishi wa Chuo, Wanachuo na Wananchi wa eneo hilo. Serikali inawakaribisha wadau waone fursa hiyo ili wajipange kutoa huduma kwa wanachuo na wananchi kwa ujumla. Serikali itaendelea kukiimarishe Chuo kwa kuongeza idadi ya wataalamu mbalimbali ili kiweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2012/2013, Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa (*LAPF*), ulikamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa Chuo cha Serikali za Mitaa – Hombolo, kukusanya michango ya wanachama shilingi bilioni 50.03, kulipa mafao ya wanachama kiasi cha shilingi bilioni 26.9 na kuandikisha wanachama wapya 4,495. Mfuko katika kipindi hicho umewekeza jumla ya shilingi bilioni 68.2 katika vitega uchumi na kukusanya shilingi bilioni 16.5 kutokana na mapato ya vitega uchumi vilivyoiva.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2013/2014 Mfuko umepanga kuandikisha wanachama wapya 20,000 na kufanya idadi ya Wanachama kuongezeka kutoka 103,860 Juni, 2013 hadi 123,860 ifikapo Juni, 2014; kukusanya jumla ya shilingi bilioni 319.31 kutoka katika vyanzo mbalimbali. Mapato hayo yanajumuisha jumla ya shilingi bilioni 156.26 zinazotarajiwa kukusanya kutokana na michango ya

wanachama na shilingi bilioni 147.1 kutohana na mapato ya vitega uchumi na vyanzo vingine.

Mheshimiwa Spika, Mfuko katika kutekeleza Sheria mpya ya Mamlaka ya Hifadhi ya Jamii, umepanga kuendelea na utafiti wa kubainisha utaratibu bora wa kutoa mafao ya elimu na njia mwafaka ya kupanua wigo kwa sekta isiyo rasmi.

Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kupambana na adui ujinga, kwa mwaka 2012/2013 elimu imetolewa kwa wanafunzi 2,686 ikijumuisha elimu ya msingi na sekondari na huduma ya maktaba kwa wadau takriban 48,112. Kati ya wanafunzi hao, 112 ni wanafunzi wa awali, 835 wa msingi na wanafunzi 1,739 wa Sekondari.

Mheshimiwa Spika, Shirika katika kupambana na adui umaskini lilitoa elimu ya nadharia na vitendo kupitia Chuo cha Maendeleo ya Wananchi na shamba la ng'ombe wa maziwa. Jumla ya wanachuo 425 walipata mafunzo ya muda mrefu ya fani mbalimbali ambazo ni Kilimo na Mifugo, Ujenzi na Useremala, Ushonaji na Upishi, Magari, Uundaji na Ufuaji vyuma na Umeme wa majumbani.

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya muda mfupi yalitolewa kwa wadau 260 katika fani za udereva, ujasiriamali, kilimo cha bustani, kilimo cha uyoga, kutengeneza tofali, kuchakata ngozi na udereva wa pikipiki. Aidha, wanachuo 59 wanaosoma mchepuo wa kilimo na mifugo walipata mafunzo kwa vitendo katika shamba la ng'ombe la Shirika na lita 84,367 za maziwa ya ng'ombe zilizalishwa na kuuziwa wananchi kwa ajili ya biashara ndogondogo na lishe bora.

Mheshimiwa Spika, huduma ya afya iliendelea kutolewa. Ili kujikinga na maradhi kwa mwaka 2012/2013 wagonjwa 6,171 walipewa ushauri nasaha, kupimwa UKIMWI na kupatiwa huduma ya afya majumbani. Aidha, wagonjwa 1,059 walisajiliwa katika kliniki ya kutoa huduma kwa wanaoishi na Virusi vya UKIMWI. Wanachuo 113 walipatiwa elimu ya utabibu kupitia Chuo cha Maafisa Tabibu Kibaha.

Katika kuboresha huduma ya afya, Shirika liliendelea na ujenzi wa upanuzi wa Hospitali Teule ya Tumbi awamu ya pili.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2013/2014 Shirika la Elimu Kibaha limepanga kuendelea kutoa elimu ya msingi na sekondari kwa wanafunzi 2,930 na kutoa huduma za maktaba kwa wadau 50,000; kuendelea kutoa elimu ya stadi mbalimbali katika Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha, kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wadau 300, kuendeleza shamba la ng'ombe wa maziwa na kufufua shamba la kuku. Aidha, Shirika litaendelea kutoa huduma ya afya kwa wagonjwa 450,000 katika Hospitali Teule ya Tumbi na kutoa elimu ya utabibu kwa Wanachuo 120; kuendeleza upanuzi wa Hospitali Teule ya Tumbi, kukarabati nyumba tano za watumishi na madarasa sita; na kuendelea na utekelezaji wa mpango kabambe wa matumizi ya ardhi ya Shirika.

Mheshimiwa Spika, jukumu la Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290, ni kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa Halmashauri kwa ajili ya kutekeleza Miradi ili kusaidia kuleta maendeleo. Shughuli za Bodi kwa mwaka 2012/2013, ilikuwa ni kuhakikisha kwamba, Halmashauri zinaendelea kupata na kunufaika na mikopo itolewayo na Bodi. Hadi Desemba, 2012 mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 1.0 imetolewa kwenye Halmashauri na kufanya mikopo yote iliyotolewa kufikia jumla ya shilingi bilioni 6.2 ikilinganishwa na maombi yaliyowasilishwa ya jumla ya shilingi bilioni 33.3.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho Michango ya Akiba ya jumla ya shilingi milioni 160.1 imewasilishwa kati ya shilingi milioni 585.0 zilizokadiriwa na kufanya Michango yote ya Akiba kufikia jumla ya shilingi bilioni 5.1 ikilinganishwa na kiasi kilichopaswa kuchangwa cha jumla ya shilingi bilioni 5.6. Kuhusu mikopo na riba, jumla ya shilingi milioni 276.1 zimerejeshwa na kulipwa kati ya shilingi milioni 830.7 zilizokadiriwa. Aidha, jumla ya shilingi milioni 102.5 zilipokelewa kama ruzuku kutoka Serikalini kati ya shilingi milioni 307.6 zilizokadiriwa. Uwasilishaji wa Michango na marejesho ya mikopo umekuwa si wa kuridhisha hata baada ya kurejeshwa

ruzuku ya fidia (*General Purpose Grant*) ambayo pia ilikuwa inatumika kulipia michango na kurejesha mikopo.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri nyingi zimeendelea kuonesha nia ya kukopa, lakini kwa upande mwingine urejeshaji wa mikopo na uwasilishaji wa michango nalo limeendelea kuwa ni tatizo. Hadi Desemba, 2012 Bodi inazidai Halmashauri 52 jumla ya shilingi bilioni 5.3 kwa viwango tofauti kutokana na Michango ya Akiba (MCR), Mikopo pamoja na Riba.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2013/2014, Bodi itaendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kutoa mikopo na pia kufanya ufuatiliaji ili kuhakikisha kuwa marejesho ya mikopo yanafanyika na Halmashauri zinawasilisha Michango ya Akiba kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa kwa lengo la kuongeza mtaji wa Bodii. Ili kuhakikisha kuwa Bodii inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi unaotakiwa, hatua za muda mfupi na muda mrefu zimeanza kuchukuliwa. Hatua za muda mfupi ni pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa kufanya malipo ya michango, marejesho ya mikopo na riba kuitia makato ya Benki, kufanya ufuatiliaji kwenye Mamlaka husika na kuhamasisha na kuelimisha Viongozi na Watendaji wa Halmashauri kuhusu umuhimu wa Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa. Hatua za muda mrefu zinahusu kufanya marekebisheso ya muundo wa Bodi ili iweze kutekeleza majukumu yake kama ilivyokusudiwa. Hatua za uchambuzi wa awali wa muundo wa Bodi zilikwishafanyika kwa kutumia Wataalam Washauri ambapo ilipendekezwa na kuamuliwa muundo wa Bodi ufanyiwe marekebisheso kuwa Benki ya Uwekezaji ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Muundo wa kibenki unaonekana kukubalika na wadau kwa kuwa unawaruhusu kuwekeza na kuchangia mtaji kwa njia ya hisa na mikopo kutokana na misingi ya usimamizi na uendeshaji wake ambayo iko wazi. Vilevile, inatarajiwa kuwa kuwepo kwa Benki ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa kutaleta matokeo ya kuwepo kwa mtaji wa kutosha kukidhi mahitaji ya wakopaji; kuchochea Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendeshwa kama “business

entities'; kuwafanya Viongozi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwa na mwamko zaidi wa kuibua shughuli za maendeleo katika maeneo yao; idadi ya mikopo na viwango vyta fedha kwa mikopo vitaongezeka na kuwepo kwa sera na miongozo madhubuti ya utoaji na usimamizi wa mikopo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua za awali za uchambuzi wa muundo, sasa hivi Wataalam Washauri wapo katika hatua ya uchambuzi wa kina wa muundo wa Bodi kwa lengo la kuifanya kuwa Benki ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa. Taarifa ya awali ilikwishawasilishwa na sasa Wataalam Washauri wapo katika hatua za mwisho za kuandaa taarifa kamili. Taarifa hiyo itakapokuwa tayari itawasilishwa Serikalini kwa lengo la kujadiliwa na kufanya uamuhi hatua ya kufuata kuhusu mchakato wa kurekebisha muundo.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa miundombinu katika Mradi wa Usafiri wa Haraka Dar es Salaam unaendelea. Kazi zilizofanyika katika kipindi cha Julai – Desemba, 2012 ni pamoja na: Ujenzi wa kilometa 20.9 za barabara ya Morogoro kwa zege ambao umeanza mwezi Machi, 2012 na utachukua miezi 36 hivyo utakamilika mwezi Machi, 2015 na unategemewa kugharimu kiasi cha shilingi bilioni 280.9. Kituo cha Maegesho ya Mabasi ya *DART* Jangwani ni sehemu kubwa ya ujenzi ambayo Mkandarasi alianza kazi mwezi Januari, 2012 baada ya kusimamishwa kwa muda wa miezi minane. Kazi inaendelea vizuri na ujenzi umefikia asilimia 19. Ujenzi wa kituo hicho utachukua miezi 24 na utagharimu shilingi bilioni 12.9.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine ambayo imeshafanyika ni ujenzi wa Kituo Kikuu cha Kivukoni ambacho majengo makuu yamejengwa. Kazi iko hatua za mwisho kwa kukamilisha maegesho ya Mabasi na miundombinu ya maji na umeme. Ujenzi umefikia asilimia tisini na tano. Mazungumzo ya kimkataba yanaendelea kati ya *TANROADS* na *BCEG*.

Mheshimiwa Spika, katika utaratibu mzima wa Usafiri

wa Haraka Dar es Salaam vinajengwa vituo Mlisho sita (6 *Feeder Stations*). Mkataba ulisainiwa tarehe 2 Juni, 2010 na kazi zinaendelea kwenye maeneo ya Shekilango kwa asilimia ishirini na tano, maeneo ya Magomeni kwa asilimia thelethini; eneo la Kinondoni 'A' kwa asilimia 40 na Mwinjuma kwa asilimia kumi. Mkandarasi amepewa eneo la Zimamoto na URAFIKI ili aendelee na kazi. Kazi imesimama kusubiri makubaliano ya kimkataba katika ya Mkandarasi na *TANROADS*. Utekelezaji utachukua miezi 24 na kugharimu kiasi cha shilingi bilioni 4.4.

Mheshimiwa Spika, uhamishaji na urekebishaji wa mfumo wa umeme kwenye maeneo ya miundombinu ya *DART* umekamilika na utekelezaji umechukua miezi sita na kugharimu shilingi bilioni 5.6. Aidha, katika kituo Kikuu cha Mabasi cha Ubungo, zoezi la ulipaji wa fidia linaendelea. Hadi kufikia tarehe 14 Februari, 2013 jumla ya wafanyabishara 229 kati ya 230, sawa na asilimia 99.9, walikuwa wamelipwa fidia zao na kuhamza kupisha ujenzi wa miundombinu ya *DART*. Utekelezaji utachukua miezi 24 na utagharimu shilingi bilioni 14.7. Kwa upande wa fidia ya Magomeni – Bondeni wakazi wote 42 wamelipwa fidia na kupisha shughuli za ujenzi. Vilevile, jumla ya wakazi 71 kati ya 106 wamekwishachukua fidia zao katika eneo la Gerezani. Bado kuna waliokuwa wakazi wa eneo la Kariakoo Gerezani ambao wanaendelea na shauri dhidi ya Wakala wa Nyumba wa Taifa (*TBA*). Jumla ya shilingi 9,662,012,547 zimetumika kulipa fidia kupitia Wakala wa *DART*. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Wakala hiyo itaendelea na shughuli zake kama zilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii sasa kuwashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri, kwa ushirikiano walionipa katika kipindi hiki. Aidha, nawashukuru Watumishi wote wa Serikali na Taasisi zake chini ya Uongozi wa Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Ombeni Yohana Sefue, kwa kusimamia Shughuli za Serikali vizuri. Nawashukuru Watanzania wote na

Washirika wetu wa Maendeleo, kwa michango yao ambayo imewezesha Serikali kutoa huduma mbalimbali kwa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, vilevile, napenda kuwashukuru Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu, Mbunge wa Hanang, Waziri wa Nchi (Uwezeshaji na Uwekezaji); Mheshimiwa William Vangimembe Lukovi, Mbunge wa Ismani, Waziri wa Nchi (Sera, Uratibu na Bunge); Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijiini, Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Mheshimiwa Aggrey Joshua Mwanry, Mbunge wa Siha, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; na Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Mbunge wa Ruangwa, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Elimu) kwa ushirikiano walionipa katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Nawashukuru pia Wakuu wa Mikoa na Wilaya kwa jithada walizoonesha katika kipindi hiki. Nawashukuru vilevile Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, chini ya Uongozi wa Katibu Mkuu, Bwana Peniel Moses Lyimo na Kaimu Katibu Mkuu, Bwana Jumanne Abdallah Sagini kwa kazi nzuri wanayoifanya. Niwashukuru Naibu Makatibu Wakuu, Bwana Charles Amos Pallangyo, na Bwana Alphayo Japan Kidata kwa ushauri wao wa Kitaalam ambaao wamenipa mimi na Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi katika kipindi hiki. Nawashukuru kwa kukamilisha maandalizi yote ya Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri na maelekezo anayonipatia katika kutekeleza majukumu yangu. Pia ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa ushirikiano wao mkubwa. Vilevile, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge, Viongozi wote wa Kitaifa na wa ngazi nyingine zote kwa

ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Niwashukuru sana Wapiga Kura wangu wa Jimbo la Katavi kwa ushirikiano wanaonipa katika kuleta maendeleo ya Jimbo letu. Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2013/2014, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 133,957,489,000. Kati ya fedha hizo, Shilingi 69,995,362,000 ni za Matumizi ya Kawaida na Shilingi 63,962,127,000 ni za Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Taasisi zake inaombewa jumla ya Shilingi 278,686,064,802. Kati ya fedha hizo, Shilingi 194,359,133,000 ni za Matumizi ya Kawaida na Shilingi 84,326,931,802 ni za Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi za Wakuu wa Mikoa zinaombewa jumla ya Shilingi 193,821,920,000. Kati ya fedha hizo, Shilingi 143,790,302,000 ni za Matumizi ya Kawaida na Shilingi 50,031,618,000 ni za Miradi ya Maendeleo. Aidha, Halmashauri zote zinaombewa jumla ya Shilingi 3,619,658,481,000 Kati ya fedha hizo, Shilingi 2,979,059,953,000 ni za Matumizi ya Kawaida na Shilingi 640,598,528,000 ni za Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano inaombewa jumla ya Shilingi 123,401,059,000 kwa ajili ya Mfuko wa Bunge ambapo Shilingi 114,501,459,000 ni za Matumizi ya Kawaida na Shilingi 8,899,600,000 ni za Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2013/2014, ya jumla ya shilingi 123,401,059,000, kwa ajili ya Mfuko wa Bunge. Jumla ya shilingi 4,226,123,954,802 kwa ajili ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi za Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ikiwa ni Matumizi ya Kawaida na Fedha za Maendeleo ya Ndani na Nje kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Hotuba hii, yapo majedwali ambayo yanafafanua kwa kina makadirio ya matumizi ya fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makof*)

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:
Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. (*Makof*)

Ningeweza kusema hoja hii tuiamue lakini dakika zilizobakia ni chache. Kwa hiyo, ningependa kufanya matangazo machache kama ifuatavyo:-

Kama tulivyokubaliana na mtakavyoona, suala la pongezi nani hakuna. Wakati wa bajeti hata utambulisho hakuna. Kwa hiyo, natambua Viongozi wa Mikoa wako pale lakini siwezi na Mikoa yao na kusimama na kuinama kwa Spika hiyo haipo.

Waheshimiwa Wabunge, mnaona fomu zinazunguka zunguka; fomu nyekundu hizi zinazosema maombi ya kuchangia Bajeti za Wizara. Tumeweka Wizara zote mpaka mwisho wa bajeti na tarehe zake. Ule utaratibu wa nyuma tulikuwa tunasema Waziri anaposoma mnaanza kuandika barua za kuomba kuchangia, tuliona kama hauna mshiko, kwa sababu mtu anaandika wakati Waziri anasoma, kumbe hii wewe ukikaa vizuri ukaandika vizuri *priority* zako unataka Wizara zipi, kwa kweli usikose kuzungumza kama ikibidi.

Kipindi hicho unapata muda wa kufanya *research* au *ku-consult* au kushauriana na wenzako, kusudi inapofika siku ya kuzungumza huku unaitwa, wewe unazungumza mambo.

Waheshimiwa Wabunge, taratibu zilikuwa mwanzo kabisa unaongea mambo ya Kitaifa, halafu baadaye unazungumza nya kwako au vya kule nyumbani, kwa sababu wewe ni Mbunge wa Taifa, siyo unaanza habari ya choo kule kwangu na nini kule kwangu. Jamani kile choo unachokitaja kijijini kwako kule sisi hatukijui. Kumbe ukijipanga vizuri kabisa unazungumza mambo ya Kitaifa, unakuja unashuka kwenye sehemu yako. Sasa hii inatupa nafasi ya kujiandaa.

Tulivyokubaliana maneno maneno ya kujipongenza akina nani hayapo, tunataka kutumia muda wetu vizuri. Hizi fomu zitaniwezesha mimi sasa, nilipewa shutuma nydingi sana, lakini Mungu anajua sikufanya hivyo; napendelea huku, napendelea kule, basi nitaona vizuri. Sasa mtakuwa mmenipa picha nzuri ya kujua wangapi wanachangia kutoka wapi, lakini kikubwa tujiandae vizuri na ndiyo maana ya hizi fomu.

Mtajaza sasa na mtazirudisha katika ofisi yangu na sisi tutaona watu wameomba katika sehemu gani. Mnaandika kipaumbele cha kwanza, cha pili na cha tatu. Tunajua kabisa kwa miaka yote, Mbunge hajawahi kuchangia zaidi ya Wizara sita, lakini anaweza akajiwekea Kipaumbele mpaka nne, tano, sita, inawezekana. Kwa hiyo, tunaomba hizi mztumie vizuri, mnarudisha Ofisi ya Katibu wa Bunge. Hilo ni moja tuliloliona.

Kesho, bahati mbaya Ofisi ya Waziri imekaa kidogo siyo vizuri; ukiangalia ile nyongeza ya *Order Paper*, tutakuwa na hotuba nydingi sana kesho. Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwa sababu pia yeye ndiyo Waziri Kivuli kwa Waziri Mkuu, tutampa saa moja kusoma hotuba yake. Wengine wote mlioko hapa ni nusu saa kwa mujibu wa Kanuni. Kwa hiyo, kesho asubuhi pia tujiandae kwa hotuba hizo, zitakuwepo nydingi labda watu kuchangia wataanza jioni.

Kwa hiyo, sasa hivi ninayo hesabu ya kila dakika za kila Wizara itakazotumia, ndiyo maana suala zima la kutumia muda hovyo litakuwa halikubaliki sana. Mkisoma vizuri Kanuni zetu, masuala ya miongozo, taarifa kama ni mwongozo ule

wenye nia hasa ya kufahamu, kawaida unachukua muda wa nusu dakika au dakika moja. Baada ya kuunga mkono mwongozo, hiyo haipo kwenye Kanuni.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake, mambo haya tumefanya mabadiliko. Kutakuwa na kasoro nyingi, changamoto sababu ya upya wa jambo lenyewe, tungetamani sana watu wakiwa na utaratibu wa kuandika kwamba tunafikiri jambo fulani halijakaa vizuri, hivyo naomba waweke vizuri. Hata katika kufanya kazi kama wanafikiri kuna dosari ya namna fulani walete maandiko, kusudi tuendelee kuimarisha utaratibu huu, hatimaye tutapata kitu kizuri zaidi kuliko vile tulivyoanza.

Kwa hiyo, tutavumiliana kwa mambo mengi ambayo yatakuwa yanaonekana pengine si vizuri labda kwa ajili ya upya wa jambo lenyewe.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naomba nahirishe Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. (*Makofii*)

*(Saa 1.25 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi,
Tarehe 11 Aprili, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*